Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Nne - Tarehe 4 Februari, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabuza Shirika la Usafiri Dar es Salaam *Limited (UDA)* kwa Mwaka 2001 *(The Annual Report and Accounts of Shirika la Usafiri Dar es Salaam Limited (UDA) for the year 2001).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kwa Mwaka wa Fedha 2001/2002 *(The Annual Report and Accounts of the National Institute of Transport for the year 2001/2002).*

Taarifa ya Mwaka ya Shirika la Usimamizi wa Mali na Madeni ya Shirika la Ndege Tanzania kwa Mwaka 2004 *(The Annual Report of Air Tanzania Holding Coorporation for the Year 2004).*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa James Musalika.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 32, kifungu cha kwanza cha Kanuni za Bunge lako Tukufu toleo la mwaka 2004 ukurasa wa 18, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lijadili Hati iliyowasilishwa mezani na Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi juu ya *Air Tanzania Holding Coorporation* .

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Hoja ya kujadili hesabu za Air Tanzania Holding Coorporation ilikubaliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na *agenda* inayofuata ningependa Waheshimiwa Wabunge kuwatambulisha wageni wa Kimataifa ambao wametutembelea leo hapa Bungeni ni Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Malawi na ni Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge hilo la Malawi, wako hapo kwenye *gallery* ya Spika. Nawakaribisha *(Makofi)*

Tunaendelea na *Order Paper, agenda* inayofuata Katibu.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 36

### Vigezo vya Kutenga Eneo la Nchi kuwa na Hadhi fulani ya Kiutawala

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:

Kwa kuwa nchi yetu ya Tanzania imegawanywa katika Vitongoji, Vijiji, Mitaa, Kata Wilaya, Miji Midogo, Miji, Manispaa, Jiji na Mikoa; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikitangaza maeneo mbalimbali kuwa na hadhi mojawapo katika ya hizo nilizozitaja:-

(a) Je, sasa hivi kuna Vitongoji, Vijiji, Mitaa, Kata, Wilaya, Miji Midogo, Miji, Manispaa, Jiji na Mikoa mingapi Tanzania Bara?

(b) Je, eneo limepewa hadhi ya kuwa Wilaya kwa kutumia vigezo gani na viliwekwa mwaka gani?

(c) Je, kuna eneo lolote lililowahi kufutiwa hadhi lililopewa kwa kupungukiwa na vigezo vilivyotumika kulipa hadhi eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shelukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuunda au kugawa maeneo ya kiutawala hapa nchini yanayotawaliwa na Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 (Mamalaka za Wilaya), Namba 8 (Mamalaka za Miji) ya mwaka 1982 na Sheria ya Taratibu za Uanzishaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994. Hivyo, kwa mujibu wa takwimu zilizopo, idadi ya maeneo mbalimbali ya kiutawala yaliyopo ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Vitongoji | - | 54,261 |
| Vijiji | - | 9,808 |
| Mitaa | - | 2,600 |
| Kata | - | 2,555 |
| Tarafa | - | 516 |
| Miji Midogo | - | 96 |
| Miji | - | 11 |
| Halmashauri za Wilaya | - | 92 |
| Manispaa | - | 12 |
| Majiji | - | 2 |
| Wilaya | - | 105 |
| Mikoa | - | 21 |

(b) Mheshimiwa Spika, mamlaka ya kugawa eneo la Tanzania kuwa Mikoa au Wilaya iko kwa Mheshimiwa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baadhi ya vigezo anavyoweza kuvitumia kugawa maeneo haya ni:-

- Ukubwa wa eneo linaloweza kuunda Wilaya au kugawanywa;

- Sababu za kijiografia;

- Uwezo wa Serikali wa kuanzisha maeneo mapya ya Utawala ambayo yanahitaji raslimali, watu, nyumba, magari na vifaa mbalimbali; na

- Mengineyo yoyote anayoyaona Rais yanafaa kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kusema katika majibu yangu ya awali, vigezo hivi viliainishwa wakati wa kutayarisha Sheria Na. 12 ya mwaka 1994 ya Taratibu za Uanzishaji wa Mikoa na Wilaya.

(c) Mheshimiwa Spika, maeneo mbalimbali ya ngazi za utawala wa Serikali za Mitaa yamekwishafutwa kutokana na sababu mbalimbali kama ifuatavyo:-

Tarafa ya Hanga, Wilaya ya Songea, Kata tatu za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ambazo ni Kanindo, Milambo na Igombemkulu, vijiji 98 ambavyo vilikuwa ndani ya maeneo ya Mamlaka za wamiliki wengine wa ardhi au kuwa kwenye hifadhi ya Mbuga za Wanyama au maeneo hayo kuwa yameendelezwa kimji, hii ina maana maeneo ya vijiji hasa aya mjini kugeuka na kujengwa kimji.

Mwisho ni vijiji 528 ambavyo vimefutwa kufuatia tangazo la Serikali Namba 353 la tarehe 17 Septemba, 2004 linaloanzisha Mamlaka za Miji midogo tisa.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa mji unapotapa hadhi ya mji kwa kutimiza vigezo vyote vinavyostahili wanastahili kupatiwa Ikama kwa maana ya Watendaji wa Idara mbalimbali ili kazi za utendaji katika mji huo uliopata hadhi uweze kufanya kazi zake kikamilifu na kupata migawo inayostahili kama mgawo wa *Road Toll* na migawo mingine yoyote.

Kwa kuwa mji wa Korogwe umepata hadhi hiyo na kule Manyara, Babati pamoja na Kibaha lakini mpaka sasa hivi hawajapata migao inayostahili na Ikama ya Watendaji inavyostahili na ni zaidi ya mwaka sasa. Je, ni kwa nini mpaka sasa halijatekelezwa na matokeo ni kuleta mgongano katika ya Mamlaka ya Mji na Halmashauri ya Mji katika Wilaya hizo ambazo nimezitaja? Naomba jibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wakati wa kipindi cha mpito baada ya uamuzi kama huo kufanywa na Serikali kunakuwa na kasoro za hapa na pale kabla ya Halmashauri mpya haijaweza kufanya kazi zake sawasawa, lakini naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Joel Bendera, vile vile na sehemu nyingine ambako tumeanzisha Mamlaka kama hizi kwamba jambo hili linafahamika na Ofisi yetu inajitahidi sana kujaribu kurekebisha kasoro hizo ili Mamlaka hizi ziweze baada ya muda si mrefu hata kuanzia Bajeti ya mwaka itakayofuata ziweze nazo kufanya kazi kama Halmashauri kamili.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa majibu yamekuwa kwamba kuna maeneo mengine yanafutwa na kwa kuwa kwa muda mrefu sasa kuna maeneo ambayo Wabunge tumepeleka Wizarani kuwa yapatiwe kuwa pengine vijiji au kata, je, ni lini tutapata majibu ya maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Ofisi ya Rais, Tawala la Mikoa na Serikali za Mitaa ilipokea maombi mbalimbali kutoka sehemu nyingi tu kuhusu uwezekano wa kupatiwa vijiji vipya, vitongoji vipya, kata mpya na katika baadhi ya maeneo hata Wilaya.

Lakini labda tuzungumze hili alililoliulizia, kwa upande wa vijiji na kata juhudi zilifanywa na tumeweza kuandikisha baadhi ya vijiji kadhaa pamoja na kata chache, lakini zoezi hili lilisitishwa kutokana na matatizo mengine ambayo tuliona tukiendelea katika juhudi hizo yangetuletea matatizo wakati wa uchaguzi tuliofanya wa Serikali za Mitaa, lakini orodha ya vijiji vyote vinavyostahili na kata zote zinazostahili vipo na tunaendelea kujaribu kuona namna gani tunaweza tukaendelea na zoezi baada ya sasa ya uchaguzi kumalizika.

Na. 37

**Ushuru wa Soko la Kariakoo**

**MHE MARTHA M. WEJJA** aliuliza:

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ilala inasimamia usafi, ulinzi na kadhalika katika soko la Kariakoo; na kwa kuwa tangu Jiji lilipogawanywa katika Halmashauri zake tatu mwaka 2000, Manispaa ya Ilala haikusanyi fedha za mapato/ushuru wa soko hilo:-

(a) Je, fedha hizo zinakwenda wapi?

(b) Kwa nini fedha hizo hazikusanywi na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala?

(c) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kuipatia ruhusa Manispaa hiyo kukusanya mapato ya soko hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Michael Wejja, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shirika la Masoko ya Kariakoo lilianzishwa kwa madhumuni ya kusimamia na kuendesha Soko Kuu la Kariakoo na masoko mengine yatakayosimamiwa na Shirika hilo pamoja na kujenga masoko mengine mapya Jijini Dar es Salaam na kuyasimamia. Shirika hili lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Shirika la Masoko ya Kariakoo *(The Market Corporation Act No. 36 of 1974)* na kama ilivyofanyiwa marekebisho kwa Sheria Na. 4 ya mwaka 1985. Serikali ilitoa asilimia 51 ya hisa zake ili zinunuliwe na Halmashauri ya Jiji mwaka 1985. Lakini kwa bahati mbaya hadi hivi sasa Jiji bado halijalipia hisa hizo.

Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kukusanya ushuru kutokana na shughuli za soko hilo ili kuweza kutekeleza majukumu yake yaliyowekwa kisheria na kujiendesha lenyewe pasipo kupata ruzuku toka Serikalini. Fedha hizo hutumika kwa ajili ya :-

- Kusimamia na kufanya usafi, kugharamia ulinzi na usalama katika Soko, kutoa huduma za umeme na maji.

- Kuboresha miundombinu ya Soko kwa mfano, mifumo ya umeme, majisafi na majitaka, mfumo wa hewa shimoni, tahadhari za moto na kadhalika.

- Kuendeleza Soko kwa kufanya matengenezo, kugharamia miradi ya Shirika kama vile Ujenzi wa maturubai na mambo mengine.

- Kulipia mishahara na posho za stahili mbalimbali kwa Wafanyakazi wa Shirika.

- Kulipia gharama za uendeshaji wa soko.

- Malipo ya kisheria na kodi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2001/2002 hadi 2003/2004, Shirika lilikusanya jumla ya shilingi 3,043,639,818/= na matumizi katika kipindi hicho yalikuwa ni shilingi 3,131,144,337/=. Kutokana na limbikizo la hasara linalofikia shilingi milioni 573, Shirika limeshindwa kulipa gawio yaani *Dividend* na kodi ya mapato tokea mwaka 1992. Hata hivyo, Shirika limeanza kupata faida kidogo. Kwa mfano, mwaka 2003/2004 limeweza kupata faida ya shilingi milioni 68 ambayo imesaidida kupunguza deni lililolimbikizwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala haikusanyi mapato katika Soko la Kariakoo kutokana na sababu ya matakwa ya kisheria yaliyounda Shirika la Masoko ya Kariakoo kama nilivyoeleza.

(c) Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 28 cha Sheria ya Masoko ya Kariakoo kinafafanua kwa uwazi kwamba Sheria za mamlaka za miji yaani Manispaa ya Ilala, Kinondoni, Temeke na Jiji la Dar es Salaam, hazitaingilia shughuli za Shirika hilo. Kwa kufanya vinginevyo ni kukiuka Sheria inayounda Shirika hilo. Ofisi yangu haijapokea malalamiko ya kuwepo kasoro za kiutendaji na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato na hivyo kuhitajika kuifanyia marekebisho Sheria iliyoanzisha soko hili.

**MHE MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini ndani ya majibu yake amejifunga mwenyewe kusema kwamba soko hilo au Shirika lilifikia kupata hasara na mimi napenda kumuuliza kwamba pamoja na kupata hasara hauoni kwamba soko sasa linahitaji kuwa chini ya Halmashauri ya Ilala?

Pili, pamoja na hayo, Manispaa ya Ilala ndiyo inayohudumia zaidi ulinzi wa nje na usafi chini ya soko la Kariakoo, je, haoni kwamba umefika wakati sasa Serikali ibadilishe kifungu ili Halmashauri ya Ilala iweze kusimamia na kupata mapato hayo ili kuwezesha usafi na uendelezaji wa Soko hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba tu niseme tu kwamba niliyoyaeleza siyo kwamba nilikuwa na nia ya kujifunga lakini nilitaka kueleza ukweli wa Shirika ambalo umeulizia swali hili na kazi ya Serikali ni kue- *expose* maelezo yote yatakayokuwezesha kujua linavyoendeshwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hili ni kuwa tunachoweza kusema hapa ni kwamba kama wenye hisa ambao Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam ni washiriki wakubwa wanaona wamefikia mahali sasa ambapo Shirika hili haliwezi ku-*function*

kama ilivyokuwa imedhamiria ni juu yao kukaa na kufanya maamuzi yoyote watakayoona yanafaa na kuyawasilisha Serikalini ili yaweze kufanyiwa kazi hiyo. Sisi kama Serikali hatuwezi ku-*cheep in* kwa kuwa wenye hisa wapo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine nakubaliana naye kwamba kuna huduma fulani fulani katika eneo hilo zinazofanywa na Manispaa ya Ilala kama jukumu lake la kawaida kama katika maeneo mengine yoyote, hili nafikiri ni sehemu ya maelezo niliyoyatoa katika sehemu ya kwanza wakati najibu swali lako la nyongeza. Kwa hiyo, pengine yote haya yakichanganywa pamoja yanaweza kuwezesha ujenzi wa hoja mpya kuhusiana na ufanisi na mwelekeo wa Shirika la masoko la Kariakoo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdulkarim Shah, swali la msingi linahusu soko la Kariakoo uliza swali la nyongeza.

**MHE. ABDULKARIM E. S. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Shirika la Masoko la Kariakoo huwa linakusanya mapato na baada ya kukusanya mapato unashughulikia miundombinu yote inayoshughulikia katika soko lile la Kariakoo ikiwepo ulinzi, usalama, usafi na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa naomba kuuliza na kwa kuwa Shirika la Masoko la Kariakoo huwa linapokea mazao ya aina yote yanayotoka sehemu mbalimbali katika nchi hii. Mojawapo yakiwa zao la nazi linalotoka kwa asilimia kubwa Mafia, swali langu je, ni lini Shirika la Masoko la Kariakoo litaweza kuweka nafasi nzuri kwa ajili ya zao la nazi ambalo sasa hivi jua likija zinapigwa jua zinakatika na ikiwa mvua zinaharibika. Kwa hivyo au kama itokeapo ni lini itatenga nafasi maalumu kwa ajili ya zao la nazi ili zao lile lipate kunusurika na uharibibu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdulkarim Shah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, inawezekana anayoyaeleza yana ukweli na kwamba ndiyo hali halisi iliyopo pale Kariakoo, lakini hili jambo zaidi la kiutendaji linahusu zaidi *management* ya Kariakoo na mimi nina hakika mkizungumza vizuri na *management* hiyo mnaweza kabisa mkapata ufumbuzi wa tatizo hilo bila matatizo makubwa sana.

Na.38

**Muungano**

**MHE. LUCAS L. SELELII (k.n.y MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulifanyika kwa sura ya mwelekeo wa kuwa na Serikali moja hapo baadaye na kwamba viongozi na waasisi wetu wakati huo waliaminiwa sana na wananchi wa nyakati hizo kwa maamuzi hayo ya

busara; na kwa kuwa Muungano ulifanyika pia kwa misingi ya dharura ambayo ilitarajiwa kuboreshwa kadri ya matakwa ya wananchi na hasa katika kutathmini masuala yote ya Kikatiba na maslahi ya Muungano kwa pande zote mbili:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba yako baadhi ya masuala ya msingi kabisa yaliyomo ndani ya Muungano yanahitaji kutazamwa upya ili yapatiwe ufumbuzi unaostahili badala ya sasa ambapo baadhi ya viongozi na wananchi kutoka pande hizo mbili kuendelea kuhoji mambo fulani fulani juu ya sura ya Muungano?

(b) Kwa kuwa Tume ya Jaji Robert Kisanga ilikabidhi upungufu wa aina mbalimbali ndani ya Muungano na ilitoa mapendekezo kwa Serikali; je, ni kwa namna gani mapendekezo hayo yanatekelezwa na kwamba Serikali haioni kuwa sasa umefika muda muafaka wa kupiga kura ya maoni *referundum* juu ya miaka 40 ya Muungano na hatma yake kutoka kwa wananchi husika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na na Mheshimiwa Mbunge mia kwa mia.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali baada ya kupokea taarifa ya Jaji Robert Kisanga imekuwa ikiyafanyia kazi mapendekezo yanayotekelezeka.

Kuhusu kuitisha kura ya maoni au *referendum* kwa lugha ya kigeni, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina ibara inayoweka msingi wa utaratibu wa utekelezaji wake yaani *referendum.* Hata hivyo, kwa vile maoni ya wananchi ni muhimu Serikali ilifanya hivyo katika Waraka wa Serikali Na.1 wa mwaka 1998 au *White Paper* kama ilivyojulikana wakati huo na kwa lugha ya Kiingereza.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nina maswali ya yongeza mawili.

Kwa kuwa amekiri Mheshimiwa Waziri na kukubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, je, yupo tayari kukubali kwamba Katiba kubwa iwe ni katika ya Jamhuri ya Muungano ili Katiba zingine kwa mfano Katiba ya Zanzibar na katika zingine zikiwa na mgongano zifuate Katiba ambayo ni ya Jamhuri ya Muungano?

Swali la pili, kwa kuwa katika malalamiko yaliyo mengi ya masuala ya Muungano yakiwemo na ya mapato huwa hayapewi nafasi kubwa ya kuzungumzwa na kwa kuwa nchi ya Zanzibar ni ndogo kulinganisha na nchi ya Tanzania haioni imefika wakati ambapo mapato hayo yazungumzwe wazi ili kupunguza pengo ambalo linapelekwa kwenye nchi ya Zanzibar?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Katiba ipi ifuatwe, nina hakika Mheshimiwa Lucas Selelii anakumbuka alipoapa kulinda, kuhifadhi na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo katika Ibara ya 64 (5) inatamka hivi Mheshimiwa Spika na kwa idhini yako naomba ninukuu; "Bila ya kuathiri kutumika kwa Katiba ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba hii kuhusu mambo yote ya Tanzania Zanzibar yasiyo mambo ya Muungano Katiba hii itakuwa na nguvu ya sheria katika Jamhuri nzima ya Muungano na endapo sheria nyingine yoyote itakiuka masharti yaliyomo katika Katiba hii, Katiba ndiyo itakuwa na nguvu na sheria hiyo nyingine kwa kiasi inachokiuka Katiba itakuwa batili."

Mheshimiwa Spika, pili kuhusu suala la kuzungumzia mapato ya Jamhuri ya Muungano ikilinganishwa na yale yanayosemwa kuhusu mapato ya Tanzania Zanzibar, ningependa niseme hivi, suala la kuzungumzia matatizo yenu Kitaifa kwa mujibu wa utaratibu mliojiwekea ni suala la msingi, kimya kinaua. Katika Bunge hili kiko Chama cha Waheshimiwa Wabunge cha kupambana na Ukimwi, kauli mbiu yao ni Tuache Ukimya Tujadili Ukimwi.

**SPIKA:** Naona hili nalo ni nyeti basi tutatumia nafasi zote tatu zilizoruhusiwa na kanuni zetu, nafasi hizo tatu ni Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, wamekwisha na Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, miaka minne iliyopita Serikali ilitamka kwamba itaunda Tume ya kuchunguza na kuhakikisha kwamba kero za Muungano zinaangaliwa na kumalizwa, leo tunaambiwa Waziri anakubali kwamba bado matatizo hayo yapo, je, ni jambo gani hasa linaloifanya nchi yetu katika kipindi cha miaka minne sasa tuwe tunajadili kila siku suala hili bila ya kuzungumza ukweli, kinachofanya suala hili lisimalizwe katika kipindi hiki ni nini hasa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, miaka minne iliyopita lilitoka pendekezo la kuunda Tume ya kushughulikia masuala au matatizo ya Muungano na kwamba matatizo hayo bado yapo na ni nini kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, ningependa niseme kama nilivyosema kwamba matatizo au kero za Muungano hayo yanazungumzika, lakini yawezekana hatujakaa na kama wenzetu wanavyosema hatujakaa kitako kuyazungumza hayo kwa kina. Lakini niseme kwamba hata tutakapojipa nafasi ya kukaa na kuyazungumza kwa kina na tukakubalina kuondoa matatizo ya Muungano bado katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii sidhani kama iko Serikali yoyote hapa duniani inayosema hakuna matatizo katika uendeshaji wa shughuli zake, kitakachofanikiwa pengine ni kuyapunguza kwa wakati tutakao kuwa nao.

Lakini mimi nakumbuka nilipokuwa shule tulikuwa tunasema katika matatizo ya kiuchumi na kijamii unapotatua tatizo moja papo hapo unazalisha tatizo jipya.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais aliahidi hata ndani ya Bunge hili kwamba matatizo ya Muungano yangemalizwa katika kipindi cha miezi sita na sasa imeshachukua muda mrefu sana mambo haya hayajamalizwa na leo Waziri anakiri kwamba matatizo hayo yapo na matatizo bila ya kuzungumzwa hayawezi kuzungumzwa.

Je, Serikali inatuambia ni lini tutakaa kitako na kuyazungumza matatizo ya Muungano ambayo yatatupa nafasi Watanzania kujiunga na jumuiya nyingine kama vile Afrika Mashariki na kadhalika wakati tumetatua matatizo yetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru kutukumbusha yale tuliyoazimia kuyatekeleza katika kutatua matatizo au kero za Muungano. Namshukuru kwa kutukumbusha.

Mheshimiwa Spika, ningependa niseme kwamba hivi sasa katika jitihada hizo za kuandaa mazingira ya kuzungumza matatizo ya Muungano kinaga ubaga, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameteua Tume ya Wataalam ya kufanya maandalizi kutoka Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara waweke mambo bayana ili vikao vya kujadili mambo haya na kufikia maamuzi viweze kufanyika hapo baadaye.

Lakini nikiri kwamba wataalam wetu na niseme hapo wenzetu kutoka upande wa Tanzania Zanzibar wanakuja na msimamo kwa hiyo, hata mazungumzo yanakuwa magumu. *(Kicheko/ Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa si kweli na wala si sawa kwamba Wazanzibar wanakuja na msimamo bali wanakuja kutetea haki. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri anayehusika na mambo ya Muungano, inaelekea hafuatilii hotuba zinazotolewa na mpenzi wetu Hayati Mwalimu Julius Nyerere. Kwa kuwa Mwalimu Julius Nyerere katika hotuba zake zinazotoka *Star TV* na katika redio wanasema walipoungana Mheshimiwa Abeid Amani Karume alimwambia Mheshimiwa Rais wetu wa mwanzo kwamba nchi hii tufanye moja, Rais mpenzi wetu alikataa, akasema sisi hatuna nia hiyo, tuna nia ya kuunganisha Afrika. Leo inakuwaje Mheshimiwa Waziri anakubali suala la mwanzo kwamba tulikuwa na dhamira ya kuungana tuwe na Serikali moja, kwa nini anakubali hivyo wakati sivyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa pale aliposema kuhusu nilichokisema suala la msimamo wa wataalam wetu. Mimi nina hakika yeye hayupo katika kundi la wataalam na kile kinachozungumzwa katika vikao vya wataalam, hata sisi tunaotoa maamuzi tunangoja watuletee lakini kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa sababu tunaratibu tunajua

mazungumzo yanakwenda vipi.  Kwa hiyo, ninachokisema hapa nina hakika zaidi kuliko yeye.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili, nakiri kwamba waasisi wa Muungano hawakudhamiria Jamhuri ya Muungano kuwa nchi moja, nahisi kwa maana ya kuwa na Serikali moja.  Mimi sijui haya ameyasikia wapi, pengine ni vizuri akasome Sheria za Muungano zinazoitwa *Articles of Union,* atapata jibu sahihi la Kisheria.

Na. 39

**Tume ya Pamoja ya Fedha**

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI (k.n.y. MHE. USSI YAHAYA HAJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Tume ya pamoja ya fedha imeundwa kwa muda mrefu sasa na inafuata utaratibu wa gawio la asilimia 4.5 la misaada ya Tanzania inayopaswa kupatiwa Tanzania Zanzibar:-

(a) Je, kiwango hicho kiliwekwa kwa kutumia misingi/vigezo gani?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kiwango hicho cha asilimia 4.5 sasa kimepitwa na wakati na hivyo ipo haja ya kukiangalia upya kiwango hicho?

(c) Je, tangu kuanza kwa Tume hiyo ni kiasi gani cha fedha ambacho Tanzania Zanzibar imefaidika nacho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji, Mbunge wa Chaani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 1994 Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* lilitoa ushauri uliopendekeza kiwango cha asilimia 4.5 kama msingi wa mgawo wa gawio la faida ya Benki Kuu ya Tanzania kwa kuzingatia uchumi wa nchi kwa jumla likiwemo suala la idadi ya watu kwa mujibu wa sensa ya mwaka 1988. Ushauri wa kiwango hicho uliwekwa kukidhi namna ya kushughulikia katika kipindi cha mpito ugawaji wa misaada inayotolewa na wahisani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa  kuzingatia Ibara 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa ni vigumu kusema kiwango cha asilimia 4.5 kimepitwa na wakati mpaka hapo utafiti wa kitaalam utakapokuwa umefanyika na kubainisha hivyo rasmi au vinginevyo. Kwa kuzingatia hayo, Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo imeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha Na. 14 ya Mwaka 1996 ilitangaza kwa njia ya zabuni nia yake ya kuajiri wastadi *(Consultants)* ili wafanye utafiti wa kubainisha vigezo vya kugawana mapato na kuchangia matumizi ya Muungano. Makampuni matatu ya wastadi yamejitokeza kufanya kazi hiyo. Tume itayatumia mapendekezo ya wastadi katika kuzishauri Serikali zote mbili (Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano ya Tanzania) kwa lengo la kukifanyia mapitio kiwango hiki na kuweka kiwango kingine muafaka.

(c) Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha imeanza kazi mwezi Juni mwaka wa fedha 2003/2004. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipata gawio la shilingi milioni 220 kutokana na faida ya Benki Kuu. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 4.5 ya jumla ya gawio toka Benki Kuu. Pia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipata jumla ya shilingi bilioni 45.7 kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kiasi hicho ni sawa na asilimia 5.4 ya jumla ya misaada yote ya Bajeti kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa utata mkubwa ni hoja ya umaskini kutokana na masuala mbalimbali ya kusema mgao, mgao na kwa kuwa kuna mafuta Zanzibar, ni lini tutachimba hayo mafuta ili tuachane na matatizo haya? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwa wazo kwamba pengine ni suala la umaskini ndio linachochea hizi kauli za mgao wa kupata na kufanya nini, lakini ukiisoma Katiba yetu inatoa haki ya mgao na jukumu la kuchangia matumizi ya Muungano.

Vile vile ukiangalia Katiba yetu katika mambo yaliyoorodheshwa kuwa mambo ya Muungano ni pamoja na raslimali ya mafuta na gesi ya asili. Kwa hiyo, ningependa niseme kama tutafika mahali mafuta yakapatikana kwa kiasi kinachotosheleza kuyachimba kibiashara na kwa sababu yanapatikana katika Jamhuri ya Muungano pengine Jamhuri ya Muungano itapata nafasi na fursa ya kupunguza hizi kelele za mgao.

Na. 40

**Sekta ya Mifugo Kanda ya Ziwa**

**MHE. GWASSA A. SEBABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa miaka mingi, Sekta ya Mifugo imesahaulika kuwa ni ya muhimu katika kuondoa umaskini na kukuza Pato la Taifa na kwa kuwa Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa zina ng'ombe wengi wa kisasa kwa kuzalisha maziwa kama vile ng'ombe na maziwa aina ya *Friesan* zaidi ya 650 Wilayani Ngara na *Progressive Farmers* wanaopenda kuanzisha mashamba madogo madogo ya ng'ombe wa nyama na maziwa.

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya kuanzisha kituo cha uhamilishaji katika Kanda ya Ziwa ili wafugaji wapate mbegu za madume bora kutoka karibu kuliko ilivyo hivi sasa ambapo mbegu hupatikana kutoka Kenya, Uganda na *Usa River,* Arusha?

(b) Je, Serikali ina mipango gani ya kufanya Mapinduzi katika Sekta ya Mifugo ili nchi yetu ifaidike na soko zuri na la haraka la nyama na maziwa katika nchi za Burundi, Rwanda na *Congo DRC?*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna umuhimu wa kuanzisha kituo cha kusambaza mbegu za uhamilishaji siyo tu kwa Kanda ya Ziwa pekee bali kwenye Kanda zote hapa nchini pamoja na kuhamasisha matumizi ya Mbegu hizi. Kwa sasa kipo kituo kimoja tu cha uhamilishaji hapa nchini ambacho ni *NAIC-Usa River.* Kituo hiki kina uwezo wa kuzalisha dozi 420,000 za mbegu bora kwa mwaka, lakini matumizi ni kidogo takriban dozi 40,000 kwa mwaka. Hali hii inatokana na kuzorota kwa shughuli za upandishaji *(AI Field Service)* kutokana na sababu mbalimbali ikiwepo Serikali kuachia shughuli hizo kwa Wilaya na Sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka huu wa fedha 2004/2005, imetenga shilingi milioni 10 za kuanzisha vituo viwili vya kanda kwenye Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa ili kusogeza huduma hii kwa wafugaji wengi zaidi wakiwemo wafugaji wa Wilaya ya Ngara. Chini ya mpango huu, Wizara yangu itapeleka vifaa muhimu kwenye kituo cha utafiti wa maradhi ya mifugo *(VIC Mwanza).*

(b) Mheshimiwa Spika, napenda pia kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ufugaji wetu huu wa asili unahitaji kufanyiwa Mapinduzi ili kufuga kibiashara. Aidha, ni kweli kwamba ikiwa wafugaji wa maeneo ya Kanda ya Ziwa watafuga kisasa na kibiashara wataongeza uzalishaji wa mifugo na kufaidika na soko zuri la nyama na maziwa katika nchi za jirani kama vile Burundi, Rwanda na *Congo DRC.*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kuwahamasisha wafugaji ili wabadili mfumo wa ufugaji wa asili na kuingia kwenye mfumo wa ufugaji wa kibiashara kupitia huduma za ugani ikiwa ni pamoja na kutoa vipeperushi, matangazo kwenye redio, vijarida na kadhalika. Aidha, ili kuongeza matumizi ya mbegu bora za mifugo nchini, kituo cha *NAIC Usa River* kinatoa mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam ili kuwasaidia wafugaji kufanya shughuli za uhamilishaji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia mipango mbalimbali na kwa kuzingatia umuhimu huu Serikali inajitahidi kukuza Sekta ya Mifugo kama vile kuongeza soko la mifugo nchini. Aidha, tumejenga miundombinu mbalimbali ikiwemo minada ya awali ya Upili na ile ya mipakani kama vile mnada wa Buhigwe Kigoma na mingineyo. Serikali

imeimarisha utoaji wa habari na kuwawezesha wafugaji na wafanyabiashara kupata bei nzuri ya soko kila wakati.

Aidha, mfumo huo umesaidia katika kudhibiti magonjwa ya mifugo hasa yale ya milipuko. Serikali imejenga machinjio ya kisasa hapa Dodoma na Chuo cha Ukataji Nyama na inahamasisha Halmashauri na Sekta binafsi ziweze kushiriki katika kujenga miundombinu ya kisasa kwenye maeneo ya Mijini. Pia Serikali inahamasisha mawasiliano baina ya wafanyabiashara wa mifugo wa hapa nchini na nchi nyingine kupitia vyama mbalimbali kama *TCCIA* pamoja na kuunda vyama vyao katika kukuza soko la mifugo nchini.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Lakini kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa.

Kwanza Mkoa wa Kagera ulikuwa na mradi wa ng'ombe wa maziwa uliokuwa ukiendeshwa na Waholanzi na mkataba huu ulikwisha mwaka 2000. Kwa bahati mbaya wafugaji ambao wana ng'ombe wengi sana sasa hawana msaada na mradi huu unasua sua. Je, Serikali inasema nini katika kuendeleza mradi huu?

Mheshimiwa Spika, pili, Wilaya ya Ngara ina ng'ombe wa maziwa zaidi ya 1,300 ambao kwa bahati mbaya hawana mhudumu kwa sababu mtaalam aliyekuwepo amehama. Ng'ombe hao wapo katika hali ya kupotea. Je, Wizara ina mpango gani wa kutuma mtaalam mwingine ili kusudi zao hili liendelezwe vizuri na kuondoa umaskini kwa wananchi wa Ngara?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru kwa kutambua kwamba hapo awali Serikali ilijitahidi kupata mfadhili na kawaida ya ufadhili wowote nia sio kuwa na mradi ambao unatakiwa uendelee muda wote ule. Dhana nzima ya mradi wowote huwa una mwanzo na mwisho. Sasa kinachotarajiwa ni kwamba baada ya mradi huo kuisha wafugaji na wadau wote wa maeneo ambayo mradi huo upo walitakiwa kujifunza mbinu na kuuendeleza. Sasa kama haikufanyika hivyo, nasikitika sana kwani ilitakiwa iwe hivyo kwa sababu mradi hauwezi kuwa hauna mwisho.

Mheshimiwa Spika, la pili, nina hakika kwamba sio Wilaya ya Ngara tu ambayo hatuna wataalam wa mifugo, hii inatokana na Halmashauri zetu za Wilaya kutokuona umuhimu wa kuajiri wataalam wa mifugo, lakini kwa kusaidiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tunajitahidi sana kuhamasisha na kuziomba Halmashauri ziweke kwenye Bajeti zao ule umuhimu wa kuajiri wataalam.

Mpaka sasa hivi kuna baadhi ya Wilaya ambazo zimefanya hivyo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge ajaribu kwa sababu wakati huu ni wakati wa Bajeti kuhakikisha kwamba Bajeti ya Wilaya ya Ngara wameweka fungu la mshahara kwa ajili ya kuajiri mtaalam wa mifugo.

Na. 41

**Wakulima Wadogo Wadogo wa Mpunga**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA (k.n.y. MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA)** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu inao wakulima wengi wadogo wadogo wa zao la mpunga na kwa kuwa katika miaka ya 1990 hadi 1995 Serikali ilionyesha nia ya kuwasaidia wakulima hao kupitia Shirika la *IFAD:-*

(a) Je, kwa nini mpango huo haukutekelezwa kwa wakulima wa aina hiyo katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na maeneo mengine nchini?

(b) Je, Serikali itawasaidiaje wakulima hao wadogo wadogo wa mpunga katika Kata za Igagula, Kagunga, Buyagu, Katunguru, Buzilasiga, Sima na Nyamazingo ambao hujitahidi kila mwaka kuzalisha mpunga mwingi bila msaada wa Serikali?

(c) Je, Serikali ina mpango gani hasa juu ya uzalishaji na soko la zao hilo nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka wa 1990/1991 na 1997/1998, Serikali ya Tanzania, kwa kutumia mkopo wa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo wa Umoja wa Mataifa *(IFAD),* ilitekeleza mradi wa umwagiliaji uliojulikana kama *Smallholder Development Project for Marginal Areas (SDPMA).* Mradi huu ulitekelezwa kwenye Mikoa inayopata viwango vidogo vya mvua na ulilenga familia maskini zaidi kwenye Vijiji vya Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Hadi ulipomalizika mwaka wa 1997/1998, mradi ulikuwa umetekeleza skimu 18 zenye eneo la ukubwa wa hekta 4,305 za mpunga.

Kutokana na mafanikio ya mradi huo Serikali iliamua kuchukua mkopo mwingine kutoka *IFAD,* Mpango wa Chakula Duniani *(WFP)* na Serikali ya Ireland. Baada ya kupata mkopo huo Serikali iliamua kuanzisha mpango shirikishi wa umwagiliaji maji mashambani *(Participatory Irrigation Development Programme (PIDP).* Mradi umepanga kuendeleza jumla ya skimu 56 zenye eneo la ukubwa wa 13,676 kwenye Wilaya 12 za Mikoa ya Dodoma, Singida, Mwanza Manyara, Tabora na Shinyanga na tayari skimu 32 zenye eneo la ukubwa wa hekta 8407 zimekamilika.

(b) Serikali inatekeleza programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme (ASDP).* Chini ya programu hii, Wilaya zitaandaa mipango ya maendeleo ya kilimo *(District Agricultural Development Plans (DADPs).* Wataalam kutoka Kituo cha Umwagiliaji Maji Mashambani cha Mwanza watawasaidia

wakulima wa Wilaya ya Sengerema kuandaa maandiko ya miradi ya Umwagiliaji kwa ajili ya kutafutiwa fedha za utekelezaji. Aidha, Wizara itatoa utaalam wa ujenzi na mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji.

(c) Serikali imeendeleza kujenga mfumo wa mawasiliano wa barabara ili kurahisisha usafirishaji wa mazao. Aidha, Serikali imeweka ushuru wa asilimia 75 kwa mchele unaoagizwa kutoka nje ya nchi ili kuwapa wakulima nafasi ya kuuza mchele kwa bei nzuri. Hata hivyo, kiasi cha mchele kinachozalishwa nchini ni kidogo, hivyo kulazimika kuagiza tani 200,000 kwa mwaka ili kufidia pengo la mahitaji.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza; kwa kuwa wakulima wa zao la mpunga katika maeneo yaliyotajwa kwenye swali katika Wilaya ya Sengerema na wale wa Geita, Kahama hususan wale wa Bukwimba, Busolwa, Nyang'hwale, Gwingiro, Shabaka na wengine wamekuwa wakizalisha mpunga kwa wingi na hivyo kulisha Manispaa ya Shinyanga, Jiji la Mwanza, Dar es Salaam na Zanzibar na kwa kuwa pia...

**SPIKA:** Hebu uliza moja kwa moja.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka huu mpunga umelimwa kwa wingi, je, Wizara ya Ushirika na Masoko itakuwa tayari kutafuta taarifa za masoko na bei kwa wakulima wadogo ambao wamekuwa wakipunjwa na wafanyabiashara wa kati ili wapate faida?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa masoko ya mazao yote nchini na ipo Wizara mahususi inayoshughulikia suala hilo. Ninachowashauri wakulima huko walipo wawatumie wataalam wetu wa ugani wa Idara ya Ushirika na hapo litatoka jawabu la kuhusu tatizo la zao hili Kitaifa.

Na. 42

**Athari za Kilimo cha Mbogamboga Kando ya Barabara Mijini**

**MHE. ALI SAID SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa taarifa ya utafiti iliyotolewa na Kituo cha Utafiti wa Madawa ya Mimea *(TPRI)* inaonyesha kwamba kuna athari mbaya za kiafya zinazotokana na kula mbogamboga zinazolimwa kandokando ya barabara za Mijini hasa katika Jiji la Dar es Salaam ambapo moshi wa magari huathiri mimea hiyo na hivyo kuhatarisha maisha ya walaji:-

(a) Je, Serikali inafahamu jambo hilo?

(b) Kama inafahamu hivyo kuna mpango gani wa kukabiliana na athari hizo ili kulinda afya za walaji?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kupiga marufuku kilimo hicho kandokando ya barabara ili kulinda afya za watu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salum, Mbunge wa Ziwani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa karibu miaka 50 sasa madini aina ya risasi yamekuwa yakiongezwa kwenye petroli ili kuongeza nguvu za *engine.* Kwenye miaka ya 1970, ilibainika kuwa madini aina ya risasi yana madhara makubwa kwa mazingira na afya ya binadamu hususan kwa watoto ambapo hudumaza uwezo wa ubongo, kupandisha msukumo wa damu, huathiri figo na kusababisha kushuka kwa uwezo wa kufikiri. Madini hayo hulundikana mwilini kidogo kidogo hadi kufikia viwango vinavyoweza kusababisha madhara.

Mheshimiwa Spika, *Tropical Pesticides Research Institute (TPRI)* hawajawahi kufanya utafiti juu ya athari za kiafya zinazoweza kutokana na kuliwa kwa mbogamboga zilizooteshwa kando kando ya barabara za Mijini. Hata hivyo, Serikali inatambua athari za kiafya zinazoweza kupatikana kutokana na viwango vikubwa vya madini ya risasi katika mwili.

Tafiti mbili zilizofanywa, moja na M. Musabila na O.C. Othman wa *Tanzania Industrial Research and Development Organization (TIRDO)* wakishirikiana na Mkemia F.N. Luilo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na utafiti mwingine uliofanywa na G. B. Luilo na O.C. Othman wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam zilionyesha:-

- Kuwepo kwa uchafuzi wa udongo na mimea kando kando ya baadhi ya barabara za Dar es Salaam uliofanywa na madini na kemikali zilizotokana na moshi wa magari, hususani madini ya risasi *sulphur dioxide* na *nitrogen dioxide.*

- Viwango vya madini na kemikali hizo vilikuwa vikubwa katika umbali wa mita moja hadi tano kutoka kwenye barabara na vilipungua haraka umbali ulivyoongezeka na kutoweka katika umbali wa mita 50.

- Viwango vya uchafuzi wa udongo na majani vilionyesha uhusiano na wingi wa magari yaani magari yaliyoongezeka ndivyo viwango vya uchafuzi vilivyoongezeka pia.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuwalinda wananchi dhidi ya madhara yanayoweza kutokana na taka hizo za sumu, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

- Mwezi Oktoba, 2004, Serikali ilisitisha uagizaji wa mafuta ya petroli yenye madini ya risasi. Aidha, tarehe 31 Desemba, 2005 itakuwa siku ya mwisho kwa matumizi ya mafuta hayo nchini.

- Wizara ya Kilimo na Chakula imekuwa ikiwahimiza wakulima wa mbogamboga kando kando ya barabara walime umbali wa zaidi ya mita 50 kutoka kwenye barabara.

(c) Wizara ya Kilimo na Chakula imeiagiza *TPRI* kufanya utafiti wa kina juu ya viwango vya taka za sumu katika mazao yanayozalishwa kando ya barabara ili kubaini viwango vya taka hizo katika mazao hayo. Matokeo ya utafiti utakaofanywa na *TPRI* yatakuwa msingi wa kuamua juu ya hatua za kuchukuliwa. Iwapo matokeo ya utafiti huo yataonyesha kuwepo kwa ulazima wa kupiga marufuku kilimo cha mbogamboga kando ya barabara, Serikali haitasita kuchukua hatua hiyo. Wananchi wanashauriwa kuosha mboga zote kwa umakini mkubwa kabla ya kuzitumia.

**MHE. ADELASTELA E. MKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa swali kama hili lilijibiwa na niliuliza mimi na tukaahidiwa kwamba Muswada ungekuja ili kukomesha kabisa biashara ya mafuta yenye madini ya risasi, je, Waziri wa Kilimo na Chakula hawezi kushirikiana na Waziri wa Nishati na Madini na Waziri wa Afya ili kukomesha kabisa tatizo hilo na Muswada huo ukaletwa mapema Bungeni tukaupitisha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula amesema tayari Serikali imeweka utaratibu wa kuhakikisha mafuta yenye madini yenye risasi hayaingizwi nchini na nirejee tu kwamba mwisho wa mwaka huu ndio mwisho wa kuagiza mafuta ya aina hiyo na sasa hivi zaidi ya kiwango cha asilimia 90 ya mafuta yanayoingizwa hapa nchini hayana madini hayo. *(Makofi)*

Na. 43

**Tatizo la Miti aina ya Mikaratusi**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1997/1998, Hifadhi ya Taifa ya Misitu ya Magamba katika eneo la Kwembago iliungua na kusababisha madhara makubwa ya kuteketea kwa miti ya asili ambayo ilikuwa mhimili mkubwa wa chanzo kikuu cha maji kwa Mji wa Lushoto na kwa kuwa baada ya moto kuteketeza msitu wa asili sasa kumezuka tatizo kubwa la kuota kwa kasi kubwa miti ya kigeni iitwayo mikaratusi ambayo hunyonya maji ardhini kwa kasi kubwa na athari zake zimeanza kujitokeza katika Mji wa Lushoto kwa kupungua kwa wingi wa maji katika chanzo hicho:-

(a) Je, Serikali itachukua hatua gani kuangamiza miti hiyo ya kigeni ambayo ni tishio kwa chanzo cha maji cha Kwembago ambacho ni mategemeo makubwa kwa wakazi wa Mji wa Lushoto?

(b) Je, ni lini itaanza kupanda miti ya asili katika eneo linalozunguka chanzo hicho cha maji?

(c) Kwa kuwa miti ya mikaratusi ina madhara makubwa ya kunyonya maji ardhini, je, Serikali ina mikakati gani ya Kitaifa katika kushauri kuangamiza aina hii ya miti kwenye maeneo yote ya vyanzo vya maji nchini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Henry Daffa Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, napenda kwanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, miti ya mikaratusi iliingizwa nchini yapata miaka 100 iliyopita. Mikaratusi ina manufaa mengi ikiwa ni pamoja na kutumika kwa ajili ya kuni, mbao, nguzo kwa ajili ya kupitishia nyaya za umeme na simu, ujenzi na kutengeneza karatasi na hadibodi. Miti ya jamii hii hukua haraka na kuanzia miaka saba inaweza kuvunwa ili kukidhi baadhi ya mahitaji haya. Hadi sasa manufaa mengi na makubwa yamepatikana nchini katika uzalishaji wa mazao niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa maji Mjini Lushoto hakusababishwi na mikaratusi bali kunatokana na uharibifu wa msitu wa asili wa Magamba katika maeneo ya Irente na Kwembago ambayo ndiyo vyanzo vya maji kwa ajili ya Mji huu. Uharibifu unaofanyika ni pamoja na kuchoma moto kama ilivyotokea mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Daffa Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali itaruhusu miti ya mikaratusi iliyoota katika eneo la Kwembago ambalo ni chanzo kikuu cha maji kwa Mji wa Lushoto ivunwe kwa ajili ya matumizi mbalimbali na machipukizi ya miti hiyo yataondolewa ili kupunguza kasi ya uotaji wa miti hiyo katika eneo hilo. Aidha, Serikali inawahimiza wananchi wasiharibu misitu kama vile kuchoma moto ili kuhifadhi vyanzo vya maji ambavyo ni muhimu sana kwa maisha yetu.

(b) Kwa kuwa uoto wa asili wenye mchanganyiko wa miti na mimea mengine ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vya maji umeanza kujitokeza katika sehemu kubwa ya eneo la msitu lililoungua, Serikali itaendelea kulinda uoto huo badala ya kupanda miti ya asili na kwa gharama kubwa.

(c) Serikali haina mkakati wa kuiangamiza miti ya mikaratusi nchini kwani ina manufaa makubwa kama nilivyokwishaeleza. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi sana kwa majibu mazuri ya Waziri na pia nampongeza sana kwa vita yake dhidi ya kuharibu miti na hasa uvunaji mbovu wa miti hasa kupigana na magogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza kwa kuwa yeye mwenyewe amekiri kwamba kuna uharibifu wa misitu hii ambao unasababishwa na wananchi. Lakini sababu kubwa ni udhaifu wa ulinzi wa misitu hii ambao unapaswa kufanywa na Wizara na kusababisha wananchi kuingia kwenye misitu hii kuharibu.

Je, Serikali inachukua hatua gani kuimarisha ulinzi na kama vile tulivyokwishaomba kwa nini misitu hii isiingizwe ilindwe na *TANAPA* ambao wana uwezo mkubwa na vifaa vya kulinda misitu kama inavyofanya Udzungwa?

Pili, kwa kuwa yako maeneo mengi ambayo miti imevunwa na haijapandwa na hivyo kusababisha vyanzo vingi vya maji katika Wilaya ya Lushoto kukauka kama vile Mazumbai, Tambwe Serikali inachukua hatua gani kupanda misitu ambayo imekwishavunwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani kwa pongezi alizotoa na ambazo kwa kweli ni za sekta nzima ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Pili, kuhusu uharibifu na ulinzi katika misitu. Sheria ya misitu ya mwaka 2002 ambayo kwa kweli tuliipitisha hapa hapa Bungeni inatoa nafasi kubwa kwa wananchi wenyewe katika ngazi mbalimbali za vijiji kuweza kulinda maeneo haya ya misitu. Ukisema kwamba ni Serikali haitawezekana kabisa kuweza kulinda misitu yote. Ni wananchi wenyewe ambao lazima washirikishwe katika uhifadhi wa misitu hii.

Napenda kutoa pongezi kwa Mikoa ile na Wilaya ambazo kwa kweli wamefanya hivyo. Kuna Mikoa mbalimbali na katika vijiji kama 151 ambapo wamefanya kushirikisha wananchi katika masuala mbalimbali ya uhifadhi. Kwa hiyo, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kweli ndio waliopitisha sheria hii waweze kuhamasisha wananchi wao katika masuala haya ya uhifadhi.

Suala lingine la kupanda miti katika maeneo haya, nimesema kwamba katika maeneo mengine tutaacha uoto wa asili. Ukiacha ardhi kwa muda kwa mfano pale ambapo kumekuwa na uharibifu hata uharibifu wa moto kwa mfano kwa muda hata miaka miwili kunaanza kuchipua na kwa maana hiyo uoto wa asili unatokeza. Kwa hiyo, tukiacha ardhi hii bila hata kupanda mazao ya asili unapotokea uoto wa asili ni kwamba miti ya asili ndiyo ambayo inayokuwa katika maeneo haya. Kwa hiyo, jambo muhimu ni kwamba tuache ukataji ovyo wa miti, tuache uchomaji moto ovyo na tuache uharibifu wa miti katika vyanzo vya maji.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miti hii ya mikaratusi imeleta utata sana katika baadhi ya maeneo hasa katika milima ile ya Usambara na Amani kwamba ipo inayonyonya maji na ipo ambayo hainyonyi maji na wananchi kulalamika miti hii inapopandwa na watu wa misitu. Je, Serikali inaweza kutoa jibu kwamba ni kweli kuna ambayo inanyonya maji na ambayo hainyonyi maji na kama ipo ile ambayo inanyonya maji kwa nini Serikali isiipige marufuku?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, utafiti ambao umefanywa na *TAFORI* umeonyesha kwamba miti yoyote ambayo inakua haraka haraka inafyonza sana maji. Kwa hiyo, mikaratusi ni miti ambayo inakua haraka haraka na nimesema kama muda wa miaka sita au saba unaweza kuvuna na ndiyo maana mara nyingi sana inatumika kwa mfano hata katika kuni, kuezekea na kadhalika. Lakini nimesema hatuwezi kusema kwamba mikaratusi tusiipande kitu ambacho tunaweza kufanya ni kwamba mikaratusi isipandwe katika vyanzo vya maji. Kwa sababu ikipandwa katika vyanzo vya maji itanyonya maji haraka. Hilo la kwanza.

La pili, ni kwamba mikaratusi isichanganywe na mazao mengine yaani isifanywe *agro forest* katika mikaratusi. Ukipanda na mazao mengine mazao yale hayataota kwa sababu jani la mikaratusi likiteremka chini linafanya *germination* na inaharibu mazingira. Kwa hiyo, katika maeneo haya mawili kama hatujapanda vyanzo vya maji na pia tusichanganye na mazao mengine nafikiri kwamba mikaratusi bado tunaweza kupanda na kutumia matumizi yake.

Na. 44

**Vivutio vya Utalii Mkoani Rukwa**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa miaka minne nimekuwa nikiuliza Serikali ni vipi itaweza kutangaza vivutio vya utalii katika Mkoa wa Rukwa, Wilaya ya Sumbawanga ikiwa ni pamoja na Ngome ya Wajerumani ijulikanayo kama *Bismark,* Maporomoko ya Mto Kalambo na Chemichemi za maji ya moto:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa haitilii maanani kuwepo kwa vivutio hivyo kama inavyofanya kwa Mikoa ya Kaskazini?

(b) Je, ni lini Serikali itapandisha daraja Mbuga ya Lwafi kuwa *Game Park* ili kuzuia uwindaji haramu katika *Reserve* hiyo?

(c) Je, ukiondoa *Katavi National Park,* ni kivutio gani ambacho Serikali imekitangaza kwa Mikoa ya Rukwa na Mbeya; na kama jibu ni hapana, je, huo si uthibitisho juu ya ukweli wa sehemu “a” ya swali hili?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatilia maanani vivutio vilivyoko nchi nzima ikiwa ni pamoja na vivutio vilivyoko Mkoani Rukwa. Kufuatia utaratibu tuliojiwekea wa kubaini na kutathmini vivutio vya utalii nchini chini

ya Mpango kabambe wa Uendelezaji Utalii, Mkoa wa Rukwa utafanyiwa ubainishaji na tathmini ya vivutio vya Utalii kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha 2004/2005.

(b) Pori la Akiba la Lwafi liko katika Wilaya ya Nkasi na lina eneo la kilometa za mraba 2,228.26. Pori hili lilipandishwa hadhi na kuandikishwa kama Pori la Akiba kwa Tangazo la Serikali Na. 204 la tarehe 24 Januari, 1993. Hivi sasa pori hili kiutendaji linasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, ili Pori la Akiba liweze kupandishwa hadhi kufikia Hifadhi ya Taifa ni lazima mambo muhimu yazingatiwe ikiwa ni pamoja na:-

- Kuwepo kwa miundombinu, mipaka na barabara za doria;

- Kuimarisha ulinzi; na

- Tathmini ya umuhimu wa eneo lenyewe katika uhifadhi wa bioanuai.

Mheshimiwa Spika, tayari Wizara ya Maliasili na Utalii imeandaa Mpango Huishi *(Management Plan)* unaojumuisha Hifadhi ya Taifa ya Katavi, Pori la Akiba la Rukwa na Pori la Akiba la Lwafi kama eneo moja kiuhifadhi. Ushirikishwaji wa wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori na pia elimu ya uhifadhi wanyamapori itatolewa kwa wananchi. Kwa mkakati huu tunao uhakika kuwa Pori la Lwafi litapata ulinzi wa kutosha hivyo kupunguza ujangili.

(c) Ukiondoa Hifadhi ya Katavi, utangazaji wa maeneo mengine ya utalii katika Mikoa ya Rukwa na Mbeya umekuwa ukifanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta za binafsi. Vivutio kama Ziwa Nyasa, Kimondo cha Mbozi, safu za Milima ya Mbeya, Pori la Usangu, mila na desturi za wenyeji wa Mkoa wa Mbeya na vivutio vilivyoko Wilaya ya Rungwe ni baadhi ya maeneo yanayotangazwa kupitia vitabu vya taarifa za utalii kama *The Lonely Planet, Tourist Guide Book to Southern Highlands. Nelles Guide to Tanzania* na *Tantravel* jarida litolewalo na Bodi ya Utalii Tanzania, kutaja haya ni baadhi tu ya maeneo ambayo utangazaji unafanyika. Aidha, wawekezaji binafsi kwa kupitia mtandao wa *internet* wamekuwa wakitangaza vivutio hivyo.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri aliyotupatia Mheshimiwa Waziri. Lakini katika jibu la msingi ameeleza kwamba sasa ndio wanapanga mipango kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa uweze kubainishwa maeneo ya vivutio. Je, haoni kwamba kutofanya mpango huu mapema kwa kipindi cha miaka 43 toka tupate Uhuru Mkoa huu umekosa vivutio vilivyotangazwa na kutukosesha fedha kama Watanzania katika nchi hii?

Swali la pili, je, Wizara inafahamu kwamba eneo hili la *Bismark* ambalo ni kivutio kikubwa katika Wilaya yetu kinatumika hivi sasa kama kituo cha Jeshi, hivyo wale watalii waliokuwa wanakuja kuangalia kituo hiki hawawezi wakapata nafasi ya kuingia kuangalia kwa sababu tayari kina matumizi mengine ambayo hayakulengwa na Wizara yako?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niseme kwamba katika jambo lolote lile kuna suala zima la kihistoria, mikakati na mtazamo. Kwa hivyo hatuwezi leo hii tukasema kwamba basi kwa nini tusifanye utaratibu huu wa utalii ambao tunafanya sasa mwaka 1961. Kwa sababu mambo yaliyokuwa yanasisitizwa kwa wakati huo yalikuwa tofauti na msisitizo huu wa utalii ndio ambapo hata kiulimwengu hivi sasa umepata mkazo mkubwa zaidi. Kwa hivyo hata tungetangaza kwa mfano mwaka 1961 tusingefanikiwa lolote na ndiyo maana tunasema tunatangaza sasa kwa sababu hata dunia nzima ni masuala mazima ya utalii ambayo yanatiliwa mkazo. Ndiyo maana kwa mfano Tanzania imepitisha hata sera ya utalii mwaka 1998 na hivi sasa tuko mbioni kuweza kuweka sheria ambayo itagusa masuala haya ya utalii.

Lakini ni tosha kwamba tumekuwa tukisisitiza kuanzia hata mwaka juzi. Mara nyingine tunasema *Tourism going South* haya ni mambo ambayo tumekuwa tunasema na tunasisitiza. Mambo mengi ambayo yamefanyika Kilwa kule Kisiwani, hata Katavi yenyewe kuipangia mipango kwa mfano *general management plan* ilikuwa haipo. Lazima ufanye mipango katika jambo lolote, huwezi leo hii ukawa huna mpango kwa sababu watu wanakwenda kuamua labda kujenga hoteli nyingi sana. Kwa hiyo, hayo mambo ni mambo ambayo kwa kweli tunayafanya kutegemea na wakati huu ambao tuliokuwa nalo.

Mheshimiwa Spika, suala la *Bismark* tunalielewa na kwamba kwa pale wapo Wanajeshi na wakati tulipowasiliana ilionekana kwamba eneo hili lichukuliwe kuwa kivutio cha utalii basi labda Wizara ijenge eneo lingine ambapo Wanajeshi hawa wakae. Sasa ni suala ambalo linahusu Wizara mbalimbali. Linahusu Wizara yetu kama masuala ya utalii lakini pia linahusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, lakini pia linahusu Wizara ya TAMISEMI. Tumeamua kwamba watu wangu watafika si muda mrefu kwenda katika eneo hili la *Bismark* kwenda kuangalia halafu baada ya hapo itabidi kwa kweli tuzungumze na Wizara hizi zote tatu zinazohusika. *(Makofi)*

Na. 45

**Ukosefu wa Vifaa vya Kufundishia Chuo cha Ufundi Kisanjuni**

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Mwanga wamejenga Chuo cha Ufundi cha Kisanjuni, Tarafa ya Ugweno; na kwa kuwa elimu ya ufundi inahitajika sana lakini uwezo wa wananchi wa kununua vifaa vya kufundishia ni mdogo:-

(a) Je, Serikali itakubali ombi la wananchi wa Mwanga kutuma wataalamu ili wakabaini mahitaji halisi ya vifaa vinavyohitajika na kutoa msaada wa kuvinunua?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani/upi wa kuvipatia Vyuo vya Ufundi walimu wenye sifa zinazohitajika?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa niwapongeze kwa dhati wananchi wa Tarafa ya Ugweno kwa moyo na bidii zao ambazo zimewawezesha kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Kisanjuni. Wananchi hao wanastahili sifa na ni mfano mzuri wa kuigwa.

(a) Utaratibu wa Serikali kupitia *VETA* wa kutoa misaada ya vifaa vya kufundishia *(tools and equipment)* ni kama ifuatavyo:-

Wamiliki wa chuo husika huchukua fomu ya maombi kuhusu kusudio lao la kuanzisha chuo ili hatimaye kiweze kusajiliwa. Fomu hizo zinapatikana Ofisi za Kanda za *VETA* ambapo kwa wananchi wa Ugweno ofisi hiyo ipo Moshi Mjini. Pamoja na mambo mengine, fomu ya maombi inahitaji wamiliki wa chuo kuainisha aina ya fani za mafunzo pamoja na idadi ya vifaa vya mafunzo *(hand tools)* vinavyohitajika. Aidha, Serikali kwa kupitia *VETA* ina utaratibu wa kutoa vifaa vya kufundishia *(hand tools)* ili kuvisaidia vyuo vya Ufundi Standi vikiwemo vile vinavyoanzishwa kwa juhudi za wananchi wenyewe ili viweze kukidhi mahitaji ya kusajiliwa katika ngazi ya awali.

Kwa hivyo, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuuarifu uongozi wa Chuo cha Ufundi Stadi Kisanjuni, kuwasiliana na Mkurugenzi wa *VETA* Mjini Moshi kwa ushauri na utekelezaji kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na kuwapeleka wataalam kuainisha mahitaji halisi ya vifaa vinavyohitajika kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati wa kutoa misaada kwa Vyuo vya Ufundi Stadi vilivyosajiliwa ili kuwapa walimu wa vyuo hivyo mafunzo zaidi ambayo yanatolewa katika Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi kilichopo mjini Morogoro. Pamoja na misaada hii, jukumu la kukidhi gharama za uendeshaji wa chuo husika ni la wamiliki wa chuo hicho. Msaada unaoweza kutolewa ni kugharamia ada ya mafunzo ya walimu wa ufundi watakaoteuliwa kuchukua mafunzo hayo.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na nitafikisha pongezi hizo kwa wananchi wa Ugweno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mafundi na ufundi ndio msingi wa maendeleo ya viwanda na kwa kuwa vyuo vyetu vya *VETA* vina teknolojia ambayo ni duni na mfumo wake wa kuviendesha unafanya visiwe na walimu ambao wana sifa zinazohitajika, je, Serikali sasa italiona tatizo hili ili kushirikiana na wananchi kujenga vya Vyuo vya *VETA* na kuvipatia walimu nchi nzima kama tunavyofanya kwa Vyuo vya Ualimu na fani zingine?

Pili, kwa kuwa tunao vijana wengi sana ambao hawana kazi ikiwa ni pamoja na wale ambao wamepata Elimu ya Ufundi katika *VETA* kwa sababu hawana uwezo wa kununua vifaa vinavyohitajika ili waweze kujiajiri, je, Serikali itafikiria kuanzisha mfuko ambao utawakopesha vijana hawa waliohitimu katika Vyuo vya Ufundi ili waweze kujiajiri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna tatizo la vifaa vya kufundishia pamoja na walimu wasiokuwa na sifa ya ualimu. Serikali katika kulitatua tatizo hilo tumeanzisha Chuo cha Ualimu wa Walimu Ufundi Stadi pale Morogoro ambao vile vile hufundishwa namna ya kutengeneza vifaa vya kufundishia kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuhakikisha kwamba fundi seremala ili aweze kutoa useremala wake vizuri lazima awe na elimu ile ya ualimu wa kutoa elimu aliyonayo yeye kumpa mwanafunzi wake. Kwa hiyo, tunalifanyia na chuo kile sasa hivi muda wote kinajaa na mimi ningeomba Vyuo vya Ufundi Stadi vya watu binafsi visione taabu kupeleka walimu wao pale ili wakapate elimu hii tuweze kuifikisha elimu inayokusudiwa kwa vijana kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala si kushirikiana na wananchi katika kujenga Vyuo vya Ufundi. Hatuanzi katika hatua ya awali, lakini wakishamaliza tunahakikisha kwamba tunawapatia vifaa *(hand tools)* za kufundishia na sio mashine.

Pili, vifaa kwa wanafunzi wanaomaliza mafunzo yao vyuoni. Hivi sasa kwa kuanzia Chuo cha Mwanza biashara yote wanayoifanya wanafunzi kutokana na kazi zao za mikono kunatenganishwa asilimia maalum kwa ajili ya kusaidia vifaa kwa vikundi badala ya kumpa mtu mmoja mmoja. Lakini tunajitahidi programu hii iendelee katika vyuo vyote na karibu tutawashauri wazazi nao wachangie wakati chuo kinachangia na wazazi wanachangia ili wanapotoka pale wanafunzi wasiende tu kukaa mabarazani waendelee na kazi moja kwa moja. *(Makofi)*

Na. 46

**Kuwasaidia Vijana Waliojiajiri katika Vikundi Mbalimbali**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia vijana waliojiajiri katika vikundi mbalimbali vya ushonaji, ufundi uashi, ulinzi na vikundi vya uzalishaji mali katika nchi hii mijini na vijijini vikiwemo vijiji vya Mkambalani, Pangawe, Kizinga, Mkono wa Mara, Maseyu, Ngerengere, Tununguo, Kiwege, Lung'ala, Changa, Amini, Luholole, Mwarazi, Kibuko, Kidugalo, Mikese, Kikundi, Kivuma, Bamba, Kiziwa, Mkuyuni, Chanyumbu, Matuli, Kwaba na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mipango kadhaa ya kusaidia vijana waliojiajiri katika vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali mijini na vijijini vikiwemo vijiji mbalimbali ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja.

Mheshimiwa Spika, upo Mfuko wa Kukopesha vijana uliopo chini ya Wizara yangu ambao ulianzishwa mwaka 1993. Fedha hizi hupelekwa katika Halmalshauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji kwa ajili ya kukopeshwa vikundi vya uzalishaji mali ambavyo vimeomba mkopo huo. Ikiwa vikundi alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge havijawahi kuomba mkopo kutoka mfuko huo kupitia Halmashauri husika, basi Mheshimiwa Mbunge awaelimishe, ili hatimaye waweze kunufaika na mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, mpango mwingine uliopo ni wa kutoa elimu ya ujasiriamali, mafunzo yanayojumuisha uongozi, utafutaji wa masoko, utunzaji wa vitabu vya mahesabu, utunzaji stoo na kadhalika. Serikali pia hushirikiana na Mashirika yasiokuwa ya Kiserikali na Mashirika ya Dini katika kuviendeleza vikundi vya vijana vya uzalishaji mali.

Na. 47

**Uhaba wa Askari Polisi Zanzibar**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna uhaba wa Askari Polisi na wale wa doria katika Manispaa ya Mji wa Zanzibar na sehemu za vijiji hasa ukanda wa Pwani ya Zanzibar:-

(a) Je, isingekuwa vyema Askari Polisi wetu kushirikiana na vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kufanya doria kisheria?

(b) Je, ni hatua gani za makusudi zimechukuliwa za kulinda fukwe zetu kwa ushirikiano wa vikosi hivyo maalum?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir , Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa Zanzibar sio sahihi sana kuzungumzia upungufu wa askari Polisi kwani ina uwiano mzuri wa askari kwa raia. Kwa mujibu wa uwiano huo, kila Askari Polisi mmoja analinda watu 222 tu ukilinganisha na uwiano wa Tanzania nzima wa Askari Polisi mmoja kulinda watu 1,260. Uwiano wa Zanzibar ni mzuri zaidi kuliko uwiano unaokubalika Kimataifa yaani wa Askari Polisi mmoja kulinda watu kati ya 500 na 700.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inashirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika ulinzi wa raia Tanzania Zanzibar. Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar vinavyoshirikiana na Polisi ni JKU, VALANTIA na KMKM. Napenda kuchukua nafasi hii kuvishukuru Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano mkubwa vinaoutoa kwa kufanya doria na Polisi katika kulinda maisha ya watu na mali zao, Unguja na Pemba.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na fukwe zetu kuwa na vitega uchumi vingi vinavyohitaji kulindwa, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vikosi maalum vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imechukua hatua zifuatazo kuhakikisha kuwa kuna ulinzi madhubuti.

(i) Viongozi wa Polisi na wa Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hukutana na Kamisheni ya Utalii Zanzibar kila mwezi kutathmini matatizo ya usalama yanayowakera watalii na kupanga mikakati ya kuyatatua.

(ii) Jeshi la Polisi likishirikiana na vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hufanya doria za mara kwa mara katika eneo la mahoteli ya kitalii yaliyoko ufukweni. Kamisheni ya Utalii Zanzibar hushiriki katika doria hizi kwa kutoa magari.

(iii) Manispaa ya Zanzibar inaandaa mpango wa kuanzisha askari Wasaidizi *(Auxiliary Police)* ambao watapatiwa mafunzo maalum ya Kipolisi na kuwezesha kudhibiti makosa madogo madogo mitaani. Vile vile Manispaa tayari imeshafanya utaratibu wa kuwa na Mahakama ili kesi zinazohusiana na Manispaa zishughulikiwa haraka kwa mujibu wa Sheria. Jeshi la Polisi linasaidia katika maandalizi ya mpango huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba upo ushirikiano mkubwa baina ya Jeshi la Polisi na Vikosi Maalum vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika ulinzi wa raia Visiwani Zanzibar. Jitihada hizi za pamoja zimefanya Mikoa ya Zanzibar kuwa na matukio machache sana ya uhalifu ikilinganishwa na Mikoa ya Tanzania Bara.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema kuwa uwiano unaonyesha ni mzuri kwa Zanzibar. Lakini hata hivyo inaonyesha mgao wa askari hao katika sehemu ni mbaya sana haikidhi haja. Je, suala hili wameliangalia katika fukwe zetu ambazo ujambazi kila siku unafanyika kwa watalii?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, mgao wa askari hutegemea na hali ya ulinzi na usalama kwa wakati huo. Kama kuna eneo ambalo kwa wakati fulani lina matatizo ya kiusalama basi askari wengi wanaelekezwa huko. Kwa mfano, juzi juzi tulipokuwa tunaandikisha daftari la wapigakura kule Pemba kulitokea rabsha rabsha kule, ilibidi kuchukua baadhi ya askari kutoka maeneo mengine ya Zanzibar kwenda kushughulikia tatizo lile. Tatizo lilipokwisha wanarejea. Kwa hiyo, kwa kweli mgao unategemea na hali ya mazingira, tishio la uhalifu mahali lilipo na kwa upande wa Zanzibar bado sisi tunafikiri kwamba askari waliopo sasa hivi wanatosheleza kukabili matatizo ya Zanzibar.

Na. 48

**Ajali za Barabarani**

**MHE. BERNARD K. MEMBE** aliuliza:-

(a) Je, ni ajali ngapi za barabarani zimetokea tangu mwezi Januari hadi Desemba, 2004?

(b) Je, ni vifo vingapi vilitokea na mali kiasi gani ziliharibika?

(c) Je, ni nini sababu za ongezeko la ajali barabarani na hatua gani zimechukuliwa kukabili hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge wa Mtama, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya Januari hadi Desemba, 2004 zimetokea ajali za barabarani 17,039, ambazo zilisababisha vifo vya wananchi 2,366 na wengine 17,241 walijeruhiwa. Aidha, Wizara yangu haina takwimu za mali zilizoharibiwa kutokana na ajali hizo. Tathmini ya mali zinazoharibiwa kutokana na ajali na maafa mbalimbali hufanywa na Taasisi mbalimbali pamoja na Mashirika ya Bima.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba takwimu hizi zinaonyesha ongezeko la ajali 375 au 2.3% zikilinganishwa na ajali mwaka jana ambazo zilikuwa 16,664. Zipo sababu mbalimbali za ongezeko hili la ajali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Uendeshaji magari kwa uzembe wa kutozingatia sheria za barabarani ambao ulichangia ajali 9,360 sawa na 55% ya ajali zote zilizotokea mwaka 2004.

(ii) Ubovu wa magari ilichangia ajali 2,403, sawa na 14.1%.

(iii) Uendeshaji wa mwendo kasi sababu hii iliosababisha ajali 607, sawa na 1.5% ya ajali zote.

(iv) Ulevi wa madereva hawa walisababisha ajali 171 sawa na asilimia 1.5 ya ajali zote.

(v) Uzembe wa watembea kwa Miguu, wapanda pikipiki/baiskeli nao pia huchangia kutokea kwa ajali za barabarani.

Katika kukabiliana na tatizo la ajali za barabarani, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(a) Kufanya marekebisho mara kwa mara ya Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30/1973 ili kuhuisha viwango vya adhabu za makosa ya barabarani.

(b) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa magari ya abiria yaendayo mikoani kabla na baada ya kuanza safari na kuhakikisha usalama wa magari hayo kuhusu uimara wa matajiri, ulevi wa madereva, ujazaji abiria na kuwepo kwa vidhibiti mwendo.

(c) Kufanya doria za mara kwa mara katika barabara kuu na kuwachukulia hatua madereva wanaokiuka sheria na kanuni za Usalama Barabarani.

(d) Kukagua leseni za madereva wa mabasi na kuwachukulia hatua wale wanaokiuka sheria

(e) Kuendelea kutoa mafunzo ya kisasa kwa askari wa usalama Barabarani ili waweze kuzifahamu vyema zaidi sheria na kusimamia kwa ufanisi zaidi. Mafunzo hayo hutolewa kwa kushirikiana na Taasisi zingine kama Chuo cha Taifa cha Usafirishaji.

(f) Kuelimisha umma kupitia vyombo vya habari kuhusu sheria na kanuni za matumizi ya barabara. Aidha, ili vijana wapate uelewa wa masuala ya usalama barabarani, somo la usalama barabarani limeanza kufundishwa katika baadhi ya shule za msingi kwa majaribio katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Pwani. Lengo ni kufundisha somo hili nchi nzima.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinatisha, maana yake ni kwamba watu sita wanakufa kila siku kutokana na ajali za barabarani

kutokana na takwimu alizoleta Waziri. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba sababu ya sita na ya saba ambazo hakuzisema zinazosababisha ajali hizi kuwa nyingi ni ukosefu wa fidia kwa familia zilizofiwa pamoja na ukosefu wa kuwajibika katika ngazi za Serikali hasa uzembe unapotokea. Mheshimiwa Waziri atakubaliana na hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tatizo la ajali za barabarani ni kweli linatisha na linatutisha sote na hatuwezi tukalaumu tu upande mmoja ni tatizo letu wote nchi nzima kwa sababu kila anayetumia barabara naye ana mchango katika kupunguza ajali ama kuongeza ajali, ni tatizo letu wote. Lawama kwamba pengine kwa sababu fidia hazitolewi, fidia sheria iko wazi kila mwenye gari lazima awe na bima. Wenye mabasi lazima wawe na bima kubwa *(comprehensive)* ili anapopata ajali ile bima yake iweze kutoa fidia kwa waathirika. Tatizo raia wetu wengi hawajui kwamba wanayo haki ya kudai fidia kwa wenye mabasi wanapopata ajali.

Kwa hiyo, kupitia Bunge lako Tukufu, natoa wito kwa wananchi kwamba wanayo haki ya kudai fidia kwenye mabasi wakipata ajali waende kwa *police traffic* watawajazia zile fomu za kudai madai ili kila mwenye gari aliyefanya ajali kama mahakama ikithibitisha kwamba ajali hiyo amesababisha yeye aweze kulipa kupitia hiyo bima yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali ni rahisi sana kuilaumu Serikali na vyombo vya Serikali, ni kweli siwezi kukataa kwamba baadhi ya askari wetu kule barabarani wanafanya uzembe. Tulishatoa wito kwa raia kama mkikutana na askari kama hao mtupe taarifa Waziri yuko Dar es Salaam, sasa askari mzembe yuko Mwanza na kadhalika huko hawezi kujua naomba wananchi pale mnapoona askari wa barabarani anazembea, basi limejaza kupita kiasi, analisimamisha, wanazunguka kwenye kichaka halafu basi linaondoka likiwa limejaa watupe taarifa ili tuweze kuwachukulia hatua kali askari kama hao. Lakini kubwa zaidi natoa wito jambo hili ni kubwa vyombo vya dola peke yake haviliwezi, wananchi mtusaidie, Waheshimiwa Wabunge, mtusaidie kutoa elimu juu ya jambo hilo. Tukipunguza uzembe barabarani ajali zitapungua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa saa 1.30 wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, lazima tuendelee na shughuli nyingine sasa.

Kwanza ni matangazo ya vikao vya Kamati. Kuna Kamati tatu zimepangiwa kukutana leo. Ya kwanza ni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* Mwenyekiti, wake Mheshimiwa Mgana Msindai, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa tano asubuhi chumba namba 231 ghorofa ya pili. Kamati ya pili ni Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wake anaomba wajumbe wakutane saa tano asubuhi hii katika chumba namba 133 ghorofa ya kwanza.

Kamati ya mwisho ni Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba wajumbe wake wakutane saa tano asubuhi hii kwenye chumba namba 219 ghorofa ya pili. Hivyo ndiyo vikao vya kamati.

Sasa baada ya Kamati, Semina. Tulikwishapanga kwamba kesho Jumamosi kutakuwa na semina, lakini waliodhamini semina hiyo wametuletea barua ya kwamba hawajawa tayari. Kwa hiyo, semina haitakuwepo kwa kesho. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaa!

**SPIKA:** Lakini Jumapili, tulishawapangia semina inayodhaminiwa na Idara ya Utumishi, Ofisi ya Rais, hiyo itaendelea kuwepo kuanzia saa tano asubuhi. Semina ya Jumapili inahusu uzinduzi wa programu kuhusu Maadili ya Uongozi inasimamiwa na Idara Kuu ya Utumishi hiyo ni Jumapili.

Sasa kwa leo Waheshimiwa Wabunge, wamegawiwa ratiba ya shughuli za Benki ya *CRDB,* wameniambia kwamba shughuli hizi zimewalenga Wabunge, hasa ndiyo wawe wageni Waheshimiwa katika maeneo yote mawili uzinduzi wa tawi lao na hafla ya jioni *Dodoma Hotel.* Kwa hiyo, Katibu wa Bunge ameniambia kwamba magari yanayowachukua wajumbe kawaida yatawachukua kwa nyakati zinazohitajika kuwapeleka kwenye hiyo sherehe ya *CRDB.*

Mwisho niseme tu kwamba orodha mtakayoiona kwenye ubao wa matangazo ndiyo ya mwisho ya wachangiaji katika hoja ya mabadiliko ya Katiba. Orodha imekuwa wazi kila siku wamekuwa wakiongezeka wengine ambao walichelewa mpaka asubuhi hii hakuna aliyeongezeka wa ziada. Kwa hiyo, nachukulia kwamba wote waliotaka kuchangia sasa wamewasilisha majina yao na ndiyo orodha ya mwisho. Yako majina 20 tu kwa hiyo, nina hakika mjadala utakwisha leo.

Kwa hiyo, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, kwamba mtoa hoja atahimisha hoja yake siku ya Jumatatu. Muhimu ni kwamba tutapiga kura siku hiyo hiyo ya Jumatatu kabla ya saa saba. Kwa hiyo, nimekuwa nikisita kutoa ruhusa kwa walioomba kwa siku ya Jumatatu.

Napenda kuwakumbusha wale waliokwishapata ruhusa inayoishia Jumapili, tafadhali wawepo siku ya Jumatatu kwa sababu ni kura ya kuita majina. Si jambo zuri wapiga kura wako wasikie kwamba hukuwepo Bungeni siku ile wakati wa kupiga kura ya Katiba, ndiyo tunawakumbusha kwamba siku ya Jumatatu ndiyo siku muhimu ya kuhitimisha mjadala huu wa mabadiliko ya Katiba. Mwisho wa matangazo, Katibu tuendelee na *Order Paper.*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Nne katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Mwaka 2004

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Wa kwanza kwenye orodha ni Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. Ngoja kidogo wanaokwenda kunywa chai, atafuatiwa Mheshimiwa Dr.

Milton Mahanga, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na Mheshimiwa Henry Shekiffu, ndiyo wa mwanzo kwa asubuhi. Mheshimiwa Profesa Maghembe, unaweza kuanza sasa na muda wako wa kusema unahesabiwa kuanzia sasa.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu wa marekebisho ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia napenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watalaam wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa ushirikiano mkubwa ambao tulikuwa nao kwenye Kamati katika kuujadili Muswada huu. Kwa kusema haya niseme wazi kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba katika mapendekezo ambayo tumepewa, pendekezo la nne limesemewa sana na watu wengi na mimi nisingependa kurudia rudia yale ambayo yamekwishasemwa. Ila niseme tu kwamba wasiwasi wa wale ambao waliongea na hasa wale waliongea kutoka Zanzibar ilikuwa ni uhusiano wa sehemu ya 19 (2) ya Katiba kuhusiana na uendeshaji wa Mahakama ya Kadhi, kule Unguja na mjadala ambao unaendelea sasa katika Kamati yetu kwa ajili ya mahakama hizo katika sehemu ya Muungano ya Tanzania Bara. Suala hili likizingatiwa basi mimi sioni kama kuna mgogoro wowote ambao unaweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi natokea kwenye Jimbo la Uchaguzi la Mwanga ambapo kumekuwa na msuguano kidogo hasa katika Kanisa la KKKT. Ningependa sana nishauri katika ile sehemu ile ya tatu. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kulielewa suala hili na kubadilisha neno pale mstari wa nne, neno la kwanza pale, neno njia liwe kiwango, ili kuchukua msingi wa hali ilivyo katika jimbo langu lile la uchaguzi. Hayo ni mambo madogo ambayo nilikuwa nataka niyaseme kama utangulizi kabla sijasema yale ya muhimu ambayo ningependa leo niyaongelee kuhusu mabadiliko haya.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya mapendekezo ya 14 ya kubadilisha Katiba hii, ni jambo la kufurahisha sana kwamba sasa tunaondoka katika hatua ya uwakilishi ya akinamama Bungeni kutoka asilimia 20 kufikia asilimia 30. Hili ni suala la msingi kwa sababu wote tunaelewa na sensa ya mwaka 2002 imetuonyesha kwamba asilimia 52 ya watu wote wa Tanzania ni akinamama. Kwa hiyo, utaratibu wa kuongeza uwakilishi wa akinamama kuanzia asilimia 20 mpaka 30 liwe ni njia ya kuelekea idadi yao halisi ya asilimia 52 kwa 100 ya wawakilishi wote katika Bunge na katika vyombo vingine vya uwakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika mapendekezo haya, uwakilishi huu kweli uwe wa akinamama, si tu kwamba akina mama wamekuja kwenye Bunge, hapana, kwamba akinamama hawa wanachaguliwa wachaguliwe na akinamama kweli. Wawakilishe akina mama wale walioko vijijini, akina mama wale wa hali za chini, akinamama maskini wale ndiyo waweze kuwachagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wasiwe wawikilishi wa wenyeviti vya vyama na wasiwe wawakilishi wa *special interest* katika vyama vya siasa. Waingie kwenye Bunge kwa kuchaguliwa na akinamama. Hivyo marekebisho haya yangehusu pia utaratibu wa kuwachagua akinamama hawa. Asilimia 30 ya Wabunge ni wengi sana. Kwa hiyo, lazima kuwe na utaratibu wa kuchagua hawa akinamama na utaratibu huu uwe wa kidemokrasia. Unaowapa akinamama uwezo wa kuwachagua hawa wawakilishi wao, ili kweli waweze kuwawakilisha akinamama Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Chama cha Mapinduzi, mtu angeweza kusema kwamba akinamama hawa wapite kwenye kila Wilaya wachaguliwe na Mikutano Mikuu ya akinamama. Wasichaguliwe na wale akinamama wakubwa wakubwa tu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, kila chama kingetakiwa kiwe na utaratibu wa kuchagua hawa akinamama ambao unakubalika na Tume ya Uchaguzi ya Taifa. Hili lingekuwa msingi mzuri wa kuwateua na kuwachagua hawa akinamama.

Pia akinamama hawa wasiweze kufukuzwa tu na Mwenyekiti wa Chama, akienda nyumbani kwake akilala, amepiga maji yake, akitoka anasema nimemfukuza huyu Mbunge nataka kuweka mwingine. Hapana. Lazima kuwe na ulinzi katika uchaguzi huu ili hawa akinamama kweli wawe na miaka mitano kwenye Bunge na wawakilishe akinamama, wasiwawakilishe Wenyeviti wa Vyama au Kamati zao za siasa au Kamati zingine za aina yoyote. Baada ya wao kuteuliwa basi ni Wabunge na waweze kuwakilisha wananchi kikamilifu. Wakiwa na hiyo *peace of mind* nadhani wanaweza kuwa wawakilishi wazuri sana wa akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Bunge na kama jamii tuanze kufikiria kwa kipindi cha muda mrefu kwamba wa wanawake ni asilimia 52 ya watu wote wa Tanzania. Tukubali ukweli kwamba katika uwakilishi, uwakilishi unakuwa *proportional* sijui nisemeje kwa Kiswahili.

**WABUNGE FULANI:** Uwiano.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, unakuwa na uwiano na namba ya watu na tukubali huko tunakokwenda kwamba hivi tunavyokwenda lazima akina mama waende wafikie uwiano huo wa uwakilishi wa asilimia 52. Kama hivyo ndivyo basi utaratibu huu wa kuwachagua ufikiriwe upya na asilimia 50 ya Bunge haiwezi kuchaguliwa tu na watu ambao wanajikusanya kwenye vyumba, lazima wa akina mama wenyewe waweze kuwachagua moja kwa moja kwa mtu mmoja na kura moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia niongelee juu ya marekebisho ya Ibara ya 110 (1). Napendekeza kwamba Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania wawe na muda wa kufanya kazi na wakati wa kustaafu uwe sawa na Majaji wa Mahakama ya Rufaa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa maana hiyo, kwamba Jaji katika kifungu cha

(1) kwamba Jaji wa Mahakama Kuu, atalazimika kuacha kazi akiwa na umri wa miaka 65 kama mwenzake wa Mahakama ya Rufaa, badala ya ilivyo sasa kwamba alazimike kustaafu kwa miaka 60.

Mimi nadhani hakuna tofauti kubwa hata ukiangalia kwenye sifa, ziko tofauti lakini siyo kubwa ambazo zinastahili kwamba Jaji wa Mahakama Kuu, astaafu akiwa na umri wa miaka 60 na yule wa Mahakama ya Rufaa astaafu akiwa na miaka 65. Ukiangalia Majaji wetu waliopo sasa utaona kwamba baada ya miaka miwili, mitatu karibu wote wataondoka kwenye mabenchi yao na hili haliwezi kuleta *continuity* katika *bench. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo sehemu ile ya pili inayopendekeza kwamba Jaji, anaweza kuomba kustaafu kwa hiari katika umri wa miaka 55, basi lirekebishwe liwe sawa na lile la Majaji wa Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa niongelee kidogo sehemu ambayo haikupendekezwa na mabadiliko haya ili iwe ama ni benki ya mapendekezo yaliyotolewa au tuanze kuyafikiria. Nilikuwa nataka niongee juu ya sehemu hii ya Mhimili wa Bunge. Mhimili huu haukupendekezwa katika mabadiliko haya lakini baada ya kukaa kwenye Bunge hili kwa kipindi nilichokaa ningependa kutoa mapendekezo kidogo. Mapendekezo haya ningeomba Serikali iyaweke kwenye kumbukumbu zake na ningependa Wabunge pia tuanze kujadiliana kuhusu suala hili.

Kwanza kwamba muda wa Bunge hasa Bunge la Bajeti ni mfupi sana. Kutoa hoja katika Bunge muda hautoshi. Waziri anatoa hoja pale anasoma kama kasuku na hawezi kusoma mpaka akamaliza hoja zake kama alivyopanga. Mimi nadhani hiyo siyo nzuri. Mjadala katika Wizara nyingi wa siku moja tu halafu siku hiyo hiyo, Waziri hata kabla hajaongea na watalaam wake atoe majumuisho, ajibu hoja za Wabunge, halafu waanze kusema kwamba hoja zilizotolewa ni nyingi sana sitaweza kuzijibu zote, haiwezekani muda hautoshi. Hiki siyo kisingizio kinachokubalika. Haiwezekani Waziri asijibu hoja zote za Wabunge. Haiwezekani, lazima muda upatikane, ajibu hoja zote. Kwa nini asijibu? Sababu inayotolewa kuwa hakuna muda wa kutosha hakikubaliki.

Sasa Bunge litasimamiaje Serikali kama Serikali kisingizio chake ni hakuna muda kwa wewe kunisimamia? Hili halikubaliki. Kwa hiyo, Bunge lifikirie kuongeza muda wake wa kufanya kazi. Kamati za Bunge wakati tunakaa hapa kama Kamati ya Bunge Zima kujadili na kupitia kifungu kimoja kimoja tunakimbizwa hapa kama tuko kwenye *relay. (Makofi)*

**SPIKA:** Nafikiri unamuonea Waziri hili siyo suala la Katiba.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, suala hili liko kwenye Kanuni za Bunge ambazo ziko ndani, ziko *provided* kwenye Katiba hii.

Mheshimiwa Spika, najua tatizo hili, lakini ningependa nitumie uhuru wangu kidogo kwamba muda wa Maswali hapa Bungeni ni mdogo na tungependa tuwe na muda

ambao tunaweza kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, atueleze Serikali inakwendaje. Kwa hiyo, ningependa Katiba hii itambue kwamba Bunge ili liliweze kusimamia Serikali sawa sawa liongezwe muda na mimi ningependekeza Bunge kama Mabunge ya nchi zingine nyingi likutane wakati wote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naomba tena niseme kwamba naunga mkono hoja iliyotolewa kwa ajili ya marekebisho ya 14 ya Katiba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, amekwenda Mtera, anayefuata ni Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, naye kaenda zake Mtera, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, naye, Ooh! Jamani. Mheshimiwa Henry Shekiffu, yupo Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, tafadhali jiandaeni.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Muswada huu ambao ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kutoa rambirambi zangu za dhati kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lushoto na mimi mwenyewe binafsi kwa msiba wa ndugu yetu, Mbunge mwenzetu Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati, Mbunge wa kutoka Kasulu Mashariki. Mimi nimefanya naye kazi nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, mchango wake ulikuwa mkubwa sana na tunaamini tutamkosa kwa kipindi kirefu na tutaendelea kumkumbuka. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nitoe pia shukrani na pongezi nyingi kwa uwakilishi mzuri wa Muswada huu. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amesaidia kufafanua na uwasilishaji wa Waziri umekuwa ni wa ufasaha. Pia niipongeze Serikali kwa utayari wake wa kukubali ushauri wa Wabunge mara kwa mara katika mijadala ya Miswada. Hii ni sifa na kwa kweli ni kitu ambacho kinasaidia sana kuondoa migogoro kati ya Serikali na Wabunge. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri sitarudia yale ambayo wenzangu wameyazungumza. Lakini ni vizuri niyataje yale ambayo nayaunga mkono kwa nguvu ili iwe *recorded* kwamba hata dhamira yangu inanielekeza hivyo. La kwanza, napenda kuunga mkono sana kukubali kwa Serikali kuondoa suala la Baraza la Ushauri kwa Rais, napongeza sana wala sihitaji kuongeza kwa sababu wajumbe wengi wamezungumza. *(Makofi)*

Pili, naipongeza Serikali na Wizara kwa kuleta mapendekezo ya kuongeza asilimia ya uwakilishi wa akinamama kufikia asilimia 30. Wala hii haina mjadala maana ni malengo ya kuwapa nafasi akinamama katika utekelezaji wa demokrasia na tatu, naomba niunge mkono Serikali kwa kukubali na kuleta mabadiliko ya kuunda Tume ya Utumishi wa Mahakama. Ni eneo ambalo ni muhimu na baadaye nitachangia zaidi katika eneo hilo. Lakini vile vile naishukuru Serikali kwa kuongeza katika Muswada huu

kuimarisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Huko nyuma yalikuwepo mapungufu na naamini mpaka sasa yako mapungufu mengi ambayo yalikuwa yanatokea kuja kwa Miswada, kuchelewa kuleta Miswada naamini kwa kuimarisha ofisi hii mapungufu haya yatapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika mambo ambayo moja kwa moja kwa kweli mimi siafikiani nayo na wengi wameyazungumza, mimi naamini kabisa muda wa kujadili Miswada hii hasa inayohusu Katiba ni muhimu uwe mrefu. Si kujadili tu katika eneo la Bunge, lakini pia hata zile *consultations* kwa wananchi. Miswada hii imekuja kidogo imechelewa, wengine tumepewa Dar es Salaam, hatukupata nafasi ya kuiwasilisha hata kwa wananchi kupata mawazo yao kwa kina. Kwa hiyo, mengi pengine tunayozungumza ni yale ambayo ukikutana na mmoja basi unamuuliza anakupa maelezo kwa hiyo, anatupa uwezo wa kuchangia. Lakini yanatunyima haki ya kwenda ndani kujua watu wengi wanasema nini. *(Makofi)*

Lingine ni kifungu kile kinachohusu kumpa Rais mamlaka ya kuteua Wabunge 10. Mimi nafikiri si busara kuweka masharti kwa Rais ateue watu wa namna gani. Naomba kifungu hicho kirekebishwe, Rais apate uhuru wake amteue mtu kufuatana na anavyoona atamsaidia. Pia napenda niseme eneo moja ambalo niliomba liongezwe msisitizo, kuongezwa makundi maalum katika vile viti vya upendeleo. Kwa sasa hivi tumeona umuhimu wa akinamama lakini tumesahau viti vya makundi maalum, kwa mfano vijana, ni vizuri wafikiriwe hawa kuwa na uwakilishi wa kutosha katika Bunge, walemavu ni muhimu wafikiriwe kuwa na uwakilishi wa kutosha katika Bunge. Kwa hiyo, naamini mapungufu haya katika mabadiliko yajayo ni vizuri sana nimeambiwa na wasioona lakini wasioona ni walemavu. Kwa hiyo, naomba sana makundi haya yafikiriwe na yapewe nafasi yake kwa sababu siyo kwa wao kwa njia hizi za kawaida kuingia Bungeni matatizo ni makubwa sana.

Sasa nije kuchangia eneo ambalo mimi nimeona ni muhimu sana na wengi hawakulizungumzia sana japo lipo katika mabadiliko haya. Ni suala ambalo limetamkwa na yale mabadiliko yaliyoletwa katika jedwali la mabadiliko yaliyoletwa. Hili linahusu ibara ya 18 inayohusu mabadiliko kwenye ibara ndogo ya kwanza ya Ibara ya 107 (a) ambayo inatamka imebadilishwa sasa itatamka mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji wa haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama. Mimi nakubaliana sana na tafsiri hiyo. Lakini nina mgogoro kidogo katika utekelezaji wa haki hizo. Ziko sababu nyingi zinazosababisha kukiukwa kwa haki. Pasipokuwa na haki amani haiwezi kuwepo. Kwa sasa hivi ni kipindi kigumu sana katika nchi yetu. Sisi tunaokaa na wananchi tunaona jinsi haki zinavyokiukwa. Sasa ni sababu zipi zinazosababisha kuzidi kukiukwa kwa haki?

Kwanza tukija katika mahakama zenyewe ambazo ndizo zinasimamia haki kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu. Kuna upungufu mkubwa wa Majaji. Waziri alikwishatamka mara nyingi na alikwishasema kwamba kwa kweli na ni kweli huko vijijini Mahakama nyingi hazina Mahakimu. Wananchi inabidi watembee masafa marefu kwenda kupokea haki, eti wanakwenda kuhukumiwa, anatembea akahukumiwe kilometa 10, 15 ili aende akahukumiwe. Kwa kweli huu ni upotovu kabisa wa haki za binadamu.

Sasa najua Serikali inachukua hatua na itatujibu hivyo lakini mimi naamini hatua zinazochukuliwa na Serikali hazitoshi kwa mfano katika suala la upungufu wa Mahakimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Lushoto, kimejengwa kwa madhumuni ya kuelimisha Mahakimu ili kupunguza tatizo la Mahakimu.

Lakini hatua zinazochukuliwa hazionyeshi kweli kwamba hata katika miaka 10 inayokuja tunaweza kuliondoa tatizo hili, ni kwa sababu ya fedha zinazotengwa kwa kukipanua Chuo hiki. Hivi sasa uwezo wa Chuo ni kuchukua Mahakimu 50 ambao wana *Diploma* na Makarani 51 ambao wangeweza kusimamia shughuli za Mahakama.

Kwa uhaba tulio nao wa Mahakimu 600 na kwa sasa ni zaidi ya 600, hata ukigawanya idadi hiyo utakuta ni zaidi ya miaka 10 na wengine watakufa na wengine wastaafu. Ni zaidi ya miaka 10 tunaambiwa tutapata Mahakimu wa kutosha katika nchi hii. Kitu kinachotokea ni kwamba hakuna juhudi za dhati zinazoonekana. Sheria inasema, haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa. Yaani imekataliwa. Sasa tutawezaje kutenda haki wakati tunasema mhimili huyu hasimamii haki? Kama misingi ya kwanza ya kuongeza wale atakaowasimamia na kutoa haki hawapo na namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba kwa sasa hivi wanafunzi wanaosoma katika Chuo cha Mahakama Lushoto, pamoja na uchache wao wanapotoka inabidi tena waombe kazi katika Mahakama.

Mimi nashangaa, wanapelekwa na Serikali hii, wanaelimishwa kwa gharama ya Serikali hii, wanatoka tena waombe kazi kwenye Serikali hii. Tuliwachagua wa nini kuwapeleka huko? Naamini mtu akishafaulu kama vile Mwalimu, anapokwenda kwenye Chuo cha Ualimu, akishafaulu na akaonekana amefikia viwango vya kuwa Mwalimu, apewe haki ya kuajiriwa. Mwaka huu tumetangaza nafasi 55, wale waliofaulu pale wangechukuliwa wote kwa sababu madhumuni ya kukiunda Chuo kile cha Mahakama ni kuwafunza wafanyakazi wa Mahakama na Mahakimu wawe na tabia za *ethics* za kiuhakimu na zilindwe, kama unavyomchukua mtu kutoka nje ,zile ethics hakuzisoma, itabidi umpeleke akajifunze. Kwa hiyo, mimi naamini Chuo kile kimeundwa kwa madhumuni ya kuweka kada ya Mahakimu wanaoeleweka kweli kwamba ni Mahakimu na walioelimika vizuri. Kwa hiyo, Chuo kitumike kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, hilo nimechangia kwa uchungu sana kwa sababu mimi ninatoka katika eneo la Chuo kile na tunajitahidi sana kuhakikisha kwamba kinaboreshwa na ninaiomba Serikali tuunge mkono. Imejitahidi lakini nafikiri umefika wakati kwa sababu tumetamka katika Katiba kwamba mhimili huyu apewe haki ya kutenda haki, basi tumpe zana za kutendea haki. Bila ya kumpa zana tunajidanganya na tunaibadilisha Katiba kwa madhumuni ambayo hayatasaidia.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo pia katika kutenda haki ya rasilimali inayoitwa watu, *human resource*. Haya yanatokana na upungufu wa kibinadamu. Jana niliangalia katika *television,* Jaji Mkwawa alikuwa anafungua kazi za Mahakama. Alielezwa upungufu uliopo katika Mahakama, moja iliyotajwa ni kucheleshwa kwa kesi pamoja na

rushwa na lingine ambalo limetamkwa ambalo ni zito sana ni askari kubambikiza wananchi kesi. *(Makofi)*

Mimi nafikiri Muswada unawahusu *Police Ordinance*, sijui unaitwa *Police Ordinance* sijui uletwe tuuangalie! Hivi inawezekanaje mtu abambikizwe kesi? Malalamiko haya ni makubwa! Tutatendaje haki bila kuangalia chombo hiki kinachosimamia hilo? Mimi nina ushahidi ambao pengine isingekuwa vizuri nizungumze leo hapa, lakini napenda niseme kwamba siku mbili zilizopita nimeona jinsi haki ilivyokiukwa. Polisi kwa jicho langu na wananchi wanalalamika kweli na mimi nimeona mwenyewe. Mtu anapigwa na Polisi katika Kituo cha Polisi, hana kosa! Hii haki inatoka wapi?

Ni kipindi gani askari anaruhusiwa kumpiga raia? Raia maskini wa Mungu hana silaha, hajatamka kitu chochote, tena mtoto mdogo chini ya miaka 17, hajatukana, hajafanya lolote; hata kama angetukana, kikubwa zichukuliwe pingu kama anafanya fujo. Lakini kumpiga, tena unampiga kwenye kichwa! Kwa sababu hili sijalipeleka kwenye vyombo vinavyostahili ngoja nisiviweke kwenye *public*.

Lakini hili ninaamini na Bunge lililopita ninamshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika Bunge hili nilitamka jinsi wananchi kule Shinyanga walivyoonewa, kuwekwa ndani na kubambikizwa kesi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kweli aliahidi litatatuliwa katika muda wa siku 7 na limetatuliwa. Namsifu sana. *(Makofi)*

Sasa ni wangapi walio na uwezo na huyu Mwanasheria wa Serikali atakwenda katika maeneo mangapi na ni wangapi ambao wanaweza kusema kiwazi wazi kwamba hawa wanaonewa ni wachache. Sasa tuweke misingi ambayo kwa kweli itasaidia kuondoa dhuluma. *(Makofi)*

Ninachoomba na ninachosisitiza katika hili ni kuisisitizia Serikali kwamba tuwape zana hawa wenzetu ili tuwalaumu kwa haki. Kitu kimoja kilichosemwa hapo Polisi mimi nilipofika waliniuliza, sasa wewe Mbunge umekuja kuwatetea hapa. Sasa hebu mwambieni kwamba pia hatuna gari la kutembelea. Haya nimeambiwa na hao wanaohusika. Sasa akusaidie gari na kweli walikuwa wanakwenda kupambana na majambazi.

**SPIKA:** Kengele ya pili. Kwa hiyo unga mkono.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda na mimi kwanza kabisa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutoa pole za dhati kwa niaba ya Jimbo langu la Mtama kwa kifo cha ghafla cha ajali ya gari kilichomsibu mwenzetu Mheshimiwa Frank Mussati wa Kasulu Kigoma. Tunatoa pole zetu nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye Ibara ya 37 ambayo ningependa niizungumzie kwa maana ya kutoa changamoto na kuwaomba Wanasheria wanisaidie kujibu maswali ambayo yananisumbua. Ibara hii ni hiyo inayosema kwamba Rais anapokuwa hayupo, Makamu wa Rais atachukua nafasi hiyo na kama hayupo Waziri Mkuu ndiye atakayekuwa anakaimu.

Mimi kwa kweli wala sina matatizo sana na ibara hiyo, wala sikusudii kuipinga. Lakini nilitaka kuipanua zaidi kwa njia ya kujiuliza maswali ili tuone kama kweli uamuzi wetu wa kufuta au kuwafuta Mheshimiwa Spika na Jaji Mkuu ku-*act* au kukaimu bado ina uzito zaidi au pengine tutakuwa na fikra nyingine. Changamoto yenyewe ni kama ifuatavyo:-

Nilikuwa najiuliza kwa mfano; Je, inapotokea kama ilivyotokea Burundi mwaka 1993 ambapo Rais aliyechaguliwa kidemokrasia aliuawa na baada ya kuawa tu *Cabinet* yake na Mawaziri wake wote wakasambaa, baadaye Bunge baada ya kama wiki mbili, ndiyo Bunge likakutana kumteua mtu anaitwa Cyprian Mtayamirwa na mara baada ya kutoka na yeye kuja Tanzania kwenye Mkutano, akafa: Swali langu katika mazingira ya aina ile ambapo Rais na Makamu wake au *Cabinet* yake hawapo, anayekaimu ni nani?

Au tujiulize kilichotokea Madagascar Desemba mwaka 2003 kwenye fujo za Uchaguzi ambazo Rais Didia Rasraca baada ya kwenda kwenye Uchaguzi na Lazaro Manana, siku tatu baada ya Uchaguzi akatangaza kwamba uchaguzi huu haukufanyika kihaki na kwa kweli hakuna mshindi na urudiwe tena. Wananchi wakaenda mitini wakaanza fujo. Toka Desemba walipofanya uchaguzi ule mpaka mwezi *March* Madagascar ilikuwa kwenye matatizo. *Cabinet* pamoja na Makamu wake wakajiondoa na hawakuwa na uwezo hata wa kukaimu kutokana na wingi wa fujo zilizotokea. Wengine walikimbilia Ufaransa.

Najiuliza peke yangu, katika mazingira ya fujo za uchaguzi yaliyotokea kama Madagascar, Kisiwa tu cha hapa jirani ambapo Rais yanampata na wenzake wanakimbia, yakitukuta siku moja, nani anakaimu? Au twende Ukraine, Ukraine ambako ulipofika uchaguzi wa Victor Kuchma pamoja na huku Victor Sychenko ukaonekana ni batili na wananchi wakaandamana na wakapinga na Waziri Mkuu, Victor Kuchma akaungana na *opposition,* Waziri Mkuu wake yule na angetakiwa a-*act* akaungana na *opposition* na kwa kweli katika uchunguzi alikuwa amesaidia sana kumwondoa Victor Kuchman Schenko *Opposition*.

Najiuliza, katika mazingira ya aina hii, ambapo Rais na Waziri Mkuu wake hawaelewani na baadaye Rais anaondoka na Waziri Mkuu naye akajiunga na kundi lingine, labda hii kesi ni ya kimalaika mno, mbele ya safari, kitu hiki hakiwezi kutokea na tumwombe Mwenyezi Mungu kisitokee. Kikitokea, nani anakaimu? Lakini katika nchi hii yametukuta mwaka 1983 Zanzibar. Hali ya hewa ilipochafuka Zanzibar mwezi Oktoba, Rais Aboud Jumbe Mwinyi, alipolazimika kuondoka, hakuondoka peke yake. Akaondoka na *Chief Minister* wake, Mheshimiwa Ramadhan Haji Faki. Najiuliza mimi inapotokea kwamba kunakuwa *crisis* au tatizo katika nchi linalomwondoa Rais na

mtendaji wake na mara nyingi makosa haya yana mlolongo wake wa kufuatana, yanapotokea mazingira ya aina hii nani anakaimu?

Mheshimiwa Spika, twende *DRC. DRC* Rais wa kwanza, Laurent Kabila alipouawa na kwa sababu Katiba ilikuwa kimya, haisemi unapokufa nani anachukua nafasi, ilibidi Bunge baada ya siku nane Bunge lilikakaa kujadili nani akaimu. Ikamchukua mwanaye wa miaka sijui 29, Joseph Kabila, akakaimu. *Why?* Kwa sababu *Constitution* ilikuwa kimya. Hayo yakawakuta.

Lakini twende Rwanda. Marehemu Habyaremana alipokufa ghafla kwa ajali ya ndege, alikuwa na *Prime Minister* pale nyumbani kwake, mama mmoja. Lakini usiku ule ule akauawa na *Cabinet* ikasambaratika. Yanapotokea mazingira ya aina ile Mungu pitishia mbali, nani anakaimu? Busara za Kimataifa ziliposema Spika au Jaji Mkuu wanaweza kukaimu ni katika mazingira ya aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo mazingira yaliyo-*lead* katika *Conventional Wisdom* ya kusema kwamba kama *Executive Branch* na hawaangalii *individual President* wanaangalia chombo *Presidency* na *Presidency* ni Rais, Makamu wake wa Rais, Waziri Mkuu na kuteremka, wanaweza kuharibikiwa siku moja. Wakati nguzo hiyo inapotetereka lazima tutafika mahala kama hatukubali sasa siku moja vizazi vyetu vitakuja kukubali. Nguzo nyingine ya pili ni lazima ikaimu ili nguzo ile inayoongoza ijiweke sawa ya kushika nchi. *(Makofi)*

Katiba ambayo hatutaki kuibadilishabadilisha kila siku hili, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Wanasheria nchi yetu ni nchi ya amani sana. Hakuna mashaka! Lakini amani hii inaweza kutoweka siku moja. Tutawaacha wahuni waje kuishika nchi kwa muda. Yanaweza kutukuta kwa sababu haikuandikwa kwamba nchi hii milele iwe nchi ya amani na utulivu. Kwa nini hatulioni hilo kwa mbele. Tukaweka *provision* siyo kufuta haya tunayoyasema sasa, lakini tukaweka *provision* kwenye *constitution* kwamba *constitution* yetu *in circumstances*, mazingira ya kutatanisha na ya hatari *impeachment* ya uchaguzi ya vifo, inavyoweza kutokea na yakakumba *executive branch* hatuna ujanja. Tuweke *provision* itakayosema, Spika au Jaji Mkuu wanaweza kukaimu. *(Makofi)*

Hicho ni kipengele changu cha kwanza. Naendelea kumimina. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Katiba lazima iangalie mbele. Katiba haiangalii hapa hapa. Wenzetu wa Zanzibar wamesema kwamba jamani katika upande wa *protocol* kipengele chenyewe kina matatizo. Hili ni tatizo, wala tusilifumbie macho. Ni tatizo kabisa kwa sababu katika *presidency,* Rais, Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar, *Prime Minister, Chief Minister* na wengine waingie hapo, halafu wanakwenda kule. Hilo nalo liangaliwe. Lakini narudi pale pale, Mheshimiwa Philip Marmo ametukumbusha tena na tena kwamba tunapofanya marekebisho ya Katiba lazima tuangalie tunadhani kuna tatizo gani sasa au mbele ya safari ambalo tungependa liangaliwe katika Katiba. Mimi nasema tena, si vibaya Mawaziri mkakaa mkasema katika Ibara ya 37 lazima tuongeze kifungu kinachotoa hali ya dharura ya aina hii ambayo kwa vyovyote vile hatuwezi kuikwepa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, baada ya kusema yote hayo ninaunga mkono hoja, lakini natoa ombi hilo kwamba kifungu cha nyongeza kiwekwe kwa sababu mbele ya safari lolote linaweza kutukuta na si vyema tukasema *the constitution is silent,* tutapata matatizo. Ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuweza kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Mabadiliko ya 14 katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Awali ya yote, kwa niaba yangu na Wapigakura wa Jimbo la Musoma Mjini, naomba nitoe salamu zangu za rambi rambi kwa familia ya Marehemu ndugu yetu Frank Mussati pamoja na Wapigakura wa Kasulu Mashariki. Namwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza kwenye maeneo machache maana nadhani mambo mengi yamezungumzwa na wazungumzaji waliotangulia. Ningependa nichangie kwenye ibara hii inayoongezwa, ibara ya 59(b) tunapomwingiza Mkurugenzi wa Mashitaka kwenye Katiba ya nchi na kumpa madaraka ambayo hayadhibitiki. Katika nyongeza hiyo ambayo inataka kufanywa ukisoma kifungu cha 59(b)(a), (b) na pale chini 3, 4, nashindwa kuelewa kwamba ni sababu zipi ambazo zinapelekea tuweze kuingiza nafasi ya Mkurugenzi wa Mashitaka katika Katiba wakati tayari kazi hizi ambazo tunataka kuziingiza katika Katiba wamekuwa wakifanya kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kusoma pale kwenye kifungu cha (b) kuhusu shughuli ambazo Mheshimiwa Mkurugenzi huyu wa Mashitaka atakuwa akizifanya. Anasema, kuingilia kazi na kuendesha mashitaka yote ya jinai ambayo hayakufunguliwa kwa mamlaka yake; (c) inasema kusitisha mashtaka yoyote ya jinai yaliyoanzishwa na mtu yoyote au chombo chochote; mimi sikubaliani na kifungu hiki cha kusema kwamba tunampa mamlaka ya kusitisha mashitaka yoyote ya jinai yaliyoanzishwa na mtu yoyote au chombo chochote, kwa sababu endapo tutapata jambazi pale, anaweza kutumia haya mamlaka vibaya. Pale chini wanasema kwamba Mkurugenzi wa Mashirika atakuwa huru katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa ibara ndogo ya pili na hataingiliwa na mtu yoyote au mamlaka yoyote isipokuwa atapaswa kuzingatia maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, ukimkuta huyu ni fisadi, hivi atazingatia vipi maslahi ya umma? Nasema hivyo kwa sababu katika eneo ambalo limekithiri kwa rushwa ni katika hili eneo la Idara ya Mashitaka kwa sababu kuna watu ambao wamefanya madhambi makubwa, wamejificha na wameua watu. Lakini *DPP* anafuta mashitaka kwa sababu watu wale wana fedha na wanahonga kwenye Idara yake hiyo. Kwa hiyo, hiki kifungu nakiona kama ni kifungu ambacho kinampa mamlaka makubwa sana *DPP.* Lakini pia kwa nini *DPP* ikitungwa Sheria ambayo itamwezesha kutekeleza majukumu yake haya na isiwe kwamba ni lazima kazi za *DPP* zitamkwe kwenye Katiba ya nchi. *(Makofi)*

Mimi sioni sababu ya msingi ya kumwingiza *DPP* kwenye Katiba ya nchi na kuainisha shughuli ambazo anatakiwa kuzifanya. Lakini ukikiachia hiki kipengele Na.4 ambacho kinasema huyu *DPP* haingiliwi na mamlaka yoyote hapa mimi nachelea kuelewa kwamba hivi tunaweza kutoa mamlaka kubwa kiasi gani kwa mtu mmoja kwamba yeye atakuwa hawezi kuingiliwa na chochote. Ndiyo tunasema tunaweza kutunga sheria ambayo inampa mtu mamlaka makubwa ambayo yanaweza kuathiri maslahi ya watu wengine katika jamii.

Mimi nina mfano wa kesi kama mbili ambazo sitaki kuzitaja, lakini nina hakika kuna watu wameua watu, lakini ofisi ya *DPP* ikafuta mashtaka hayo kwa sababu ya uwezo huu ambao tunataka tena kumpa Katiba ambao unatamkwa ndani kwamba watu, ushahidi upo. Lakini kwa kupitia kwa *DPP* na wale Wasaidizi wake wengine ni hao Maofisa Upelelezi katika Mikoa, inafika mahali kwamba kesi za mauaji za watu wenye fedha zinafutwa na wanaoendelea kubaki kwenye mahabusu ni watu wasio na fedha.

Mheshimiwa Spika, nadhani hii Sheria ya mamlaka haya nadhani kipengele kisingekuwepo. Lakini hata hivyo nilidhani kulikuwa hakuna sababu ya msingi kuiweka hii sheria kwenye Katiba. Maana kama sababu za msingi ambazo zinatufanya yafanywe mabadilikko ya Katiba ni tatizo ambalo limejitokeza katika jamii. Ni sababu ipi ya msingi ambayo tunadhani inasababisha iwe inapelekea kwamba sisi tufanye mabadiliko ya kumwingiza Mwendesha Mashtaka, Mkurugenzi wa Mashitaka katika Katiba ya nchi, na sijui ni nchi ngapi ambazo zimeweza kufanya hivyo, maana tusije kufanya vitu ambavyo kwa kweli vinatuumiza.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo napenda nichangie ni ile ya mabadiliko ya Ibara ya 78. Katika mabadiliko ambayo tunataka kuyafanya tumesema kwamba kwa madhumuni ya uchaguzi wa Wabunge Wanawake wanaotajwa katika ibara 66(1)(b) Vyama vya Siasa vilivyoshiriki uchaguzi kwa kufuata utaratibu uliowekwa na kupata asilimia tano ya kura zote halali za Ubunge au Rais kwa kadri itakavyokuwa vitapendekeza kwa Tume ya Uchaguzi majina ya wanawake kwa kuzingatia masharti ya uwiano wa kura na masharti yaliyoainishwa katika ibara ya 82.

Mheshimiwa Spika, kama tunataka kupanua wigo wa demokrasia na kupata ushiriki wa Vyama vingi vya Siasa mimi nimejaribu kutazama kumbukumbu za Uchaguzi wa mwaka 2000, Vyama vya Siasa vilivyopata juu ya asilimia tano vilikuwa Vyama vitatu. CCM ilipata asilimia 65, *CUF* ilipata asilimia 12.5 na *TLP* ilipata asilimia tisa. Kwa hiyo, utaona kwamba Vyama vilivyobaki, kwa *UDP* walipata asilimia 4.4, CHADEMA asilimia 4.2 na *NCCR-MAGEUZI* asilimia 3.6.

Hivi Vyama vyote kama sheria hii tungeanza kuitumia haviku-*qualify* kuwa na Wabunge kwa sheria hii tunayotaka kuibadilisha ya asilimia tano. Pendekezo langu ni kwamba kama tunataka kupanua wigo nilidhani kwamba hii asilimia iko juu sana kwamba angalau basi ingekuwa asilimia tatu au nne kwa sababu ukichukulia hii ya mwaka 2000 inaonyesha kwamba kuna Waheshimiwa Wabunge hapa wasingekuwa Wabunge kama hii Sheria tungekuwa tumeipitisha kwenye Viti Maalum.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba ingekuwa vyema tukaweka asilimia ambayo angalau inaweza kufikiwa na Vyama vingi kidogo kuliko hii asilimia tano. Kwa hito huu ndio wasiwasi wangu kwamba tuiangalie kama itawezekana, basi badala ya asilimia tano tuseme asilimia nne ambayo kama tukiweka asilimia na tukachukulia takwimu za mwaka 2000 Vyama sita vingekuwa na sifa ya kuwa na Wabunge wawakilishi katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, suala la Wagombea binafsi limezungumzwa. Nilikuwa najaribu kusoma Katiba ibara ya tano ambayo inasema, kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kama raia anakuwa na haki ya kupiga kura akifikisha umri wa miaka 18, ni vyema raia huyo pia akapewa haki yake ya kupigiwa kura akishafikisha umri wa miaka 18. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba kama raia anapiga kura akiwa na miaka 18, basi tushike masharti ambayo yanamzuia raia yule wa miaka 18 kupigiwa kura katika nafasi yoyote ya uongozi.

Lakini lingine la msingi ni kwamba bado hatujawa na sheria ya kuwaruhusu wagombea binafsi. Lakini nadhani kama walivyosema wenzangu, kuzuia wagombea binafsi katika mfumo wa Siasa tulionao, tunawanyima haki ya msingi raia wa nchi hii ambao sio wanachama wa Vyama vya Siasa. Kwa hiyo, mimi nakubaliana kwamba wakati wa kufanya mabadiliko ya kuruhusu mgombea binafsi umefika na nina hakika tukiweza kufanya mabadiliko haya ya kuruhusu wagombea binafsi tutaviimarisha Vyama vyetu viwe ni Vyama ambavyo vinaweka maslahi ya nchi ile badala ya maslahi binafsi katika Vyama vya Siasa.

Kwa hiyo, mimi nadhani wagombea binafsi sasa wakati umefika na tusione aibu na nina hakika kwamba Vyama ambavyo vinasimamia maslahi ya wananchi havitapata tatizo la kuwa na wasiwasi kuhusu mgombea binafsi. Tuwe tayari sasa kwa mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, niangependa tu nichangie hivyo kwamba suala hili la wagombea binafsi sasa ni suala ambalo lingetazamwa na limekuwa kwamba mapendekezo yametolewa toka wakati wa Tume ya Nyalali, Tume nyingi zimeundwa kwamba hatuna sababu ya kuwa na wasiwasi wa kuruhusu wagombea binafsi. Nina hakika tukiruhusu wagombea binafsi tutaviimarisha sana Vyama vyetu vya Siasa. Maana Vyama vingine kwa kweli vimekuwa ni kama Vyama vinaendeshwa tu na familia fulani, kundi la watu wachache na hivyo kuwatendea isivyo haki baadhi ya wanachama ambao hawana nafasi ya uongozi katika Vyama hivyo vya Siasa. Kwa hiyo, nadhani tukiruhusu wagombea binafsi Vyama vitajiimarisha vyenyewe kwa sababu bila kufanya hivyo watu watakuwa na sababu ya kupitia kwenye Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nakushukuru na mimi naunga mkono hoja iliyo mbele yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ngoja niwataje walio ndani ya Ukumbi, sasa hivi nawaona. Pengine wengine wako kwenye Kamati. Lakini nitawapa nafasi ambao wapo ndani ya Ukumbi. Mheshimiwa Hamad Rashid, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Profesa Mwaga, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail na Mheshimiwa James Msekela, wajiandae hao. Sasa namwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Michael Laizer jiandae.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kukushukuru na naomba vile vile niungane na wenzangu kutoa mkono wa pole kwa Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati, pamoja na familia yake Mwenyezi Mungu amrehemu huko aliko.

Mheshimiwa Spika, kazi iliyoko mbele yetu ni kubwa na ningeomba sana Serikali kwamba suala la kubadilisha Katiba siyo jambo dogo sana ni jambo kubwa na ni tofauti sana na lile la kupitisha sheria tu. Uzoefu umeonyesha hapa ndani ya Bunge kwamba tunapokuwa na sheria nzito watu tunafanyiwa angalau semina kwanza kuelimishwa juu ya yale mambo yatakayobadilika. Lakini inashangaza tunafanya mabadiliko ya Katiba hata semina hatukupata nafasi ya kuwa nayo angalau tunakaelezwa msingi madhubuti wa mabadiliko haya yanayoletwa. Hilo ni sikitiko langu la kwanza.

Lakini la pili, naomba ufafanuzi, kwa utaratibu nafahamu kwamba Kanuni huwa haishindi Sheria na Sheria haishindi Katiba na Katiba haishindi yale maamuzi yanayosababisha kutengenezwa kwa Katiba. Kwa hiyo, nikitaka labda Waziri anifafanulie ni utaratibu upi unatumika wa yale mambo ya msingi yanayosababisha kutengenezwa kwa Katiba ambayo unatumika kubadilisha hayo mambo ya msingi. Kwa mfano, tulikuwa na mambo fulani yalikubaliana katika Muungano, Marais wetu wawili Marehemu Mzee Amani Abeid Karume na Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, walikubaliana na wakaweka msingi na hatimaye tukatengeneza Katiba ya muda na baadaye Katiba ya kudumu ya Tanzania. Nakumbuka Mheshimiwa Pius Msekwa pia alikuwa Mjumbe wa Kamati hiyo. Sasa tukitaka yale mambo ya msingi yanabadilishwa kwa utaratibu gani. Katiba tunaifahamu, lakini haya mambo ya msingi kama haya yakitaka kubadilishwa, yanabadilishwa kwa utaratibu gani? Ningependa kupata ufafanuzi wa hilo.

La tatu, nilitaka nieleze vile vile Jaji Mkuu wa Tanzania ndiye Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufaa. Jaji Mkuu wa Zanzibar ana nafasi gani katika Mahakama Kuu ya Rufaa? Nalo pia nataka ufafanuzi. La nne, nakumbuka Serikali imefanya juhudi kubwa sana katika kuanzisha Mahakama ya Kadhi na muda mrefu sasa imepata na mawazo mbalimbali yamekusanywa tulitaka tupata *position* ya Serikali juu kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi. Nasema hilo kwa sababu Serikali yenyewe tayari imeshalifanyia kazi, wamekwenda kwenye Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Lakini mpaka sasa hatujapata matokeo yoyote, kwa hiyo, tungependa vile vile kupata ufafanuzi wa hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi wa jumla ningependa tena kusema kwamba katika kipindi cha kumi na mbili cha mfumo wa vyama vingi, tumejenga uzoefu mkubwa sana. Sisi tulielewa mapema Serikali ilipokuwa na wasiwasi wa kuwa na

Mkutano wa Katiba wakati ule kwa sababu bado nchi yetu ilikuwa inatoka mfumo wa chama kimoja, hakijajenga uzoefu katika mfumo wa vyama vingi. Kwa hiyo, Serikali ikawa na wasiwasi kwamba pengine tungeweza kufanya mambo yale bila ya kupata uzoefu. Sasa baada ya uzoefu huu wa miaka kumi na mbili Serikali inatuambia nini sasa kutokana na taarifa za Jaji Francis Nyalali, Jaji Robert Kisanga, inatueleza nini juu ya mapendekezo yale yaliyotolewa na hao Majaji wetu wawili? Hili nalo nadhani lingetusaidia tukajua tunakokwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, la tano, ni kwamba nchi yetu imebadilika, sasa tunaingia katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, tunategemea keshokutwa tutakuwa na *Federation* ya Afrika Mashariki tutaingia kwenye *SADC* na kadhalika. Kwa hiyo, hatuwezi sasa hivi ndani ya nchi yetu sisi wenyewe tukawa na Katiba ambayo haituelekezi mbele tunakoelekea. Kwa hiyo, nafikiri kuna msingi mkubwa wa kukaa hasa *serious* tukaitazama Katiba yetu kama kweli inatupeleka mbele tunakokwenda. Kwa sababu tunakumbuka Rais wetu amekuwa Mwenyekiti Mwenza katika mambo ya *globalisation,* ni moja kwamba tutaingia katika mfumo wa utaratibu huu. Kwa hiyo, lazima tuwe na Katiba itakayotusaidia kutupeleka huko. Sasa Katiba yetu bado huko ndani yenyewe tuna matatizo, bado hatujayatatua. Moja ambalo tumelishuhudia asubuhi hapa ni tatizo letu la mambo Muungano kwamba bado hilo hatujalitatua.

Kwa hiyo, bado chombo ambacho kitasimamia nchi kitatuongoza na wananchi wakawa na matumaini bado kina kasoro nyingi ndani ya nchi yenyewe licha ya pale ambako tutaweza kuingia ushiriki na watu wengine. Nafikiri nalo hilo tungeweza kuliangalia lingeweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ya jumla, ningeomba kusema tu kwamba Wabunge hapa nilikuwa nawasikia wanasema tusichukue mifano ya nchi za nje lakini nafikiri ndio tunayoichukua. Maana hata ukiangalia Katiba yetu, tukiangalia *Westminster*, Marekani kidogo na hata Bunge letu sasa hivi tumebadilisha kidogo tume-*copy* ya India, ndio ustaarabu. Kile kizuri cha wenzetu wanachokifanya hatuna budi kuwa na utaratibu wa kukiiga. Mimi nafikiri tusichukue tu kwamba lazima tuige Afrika hata kama jambo ni baya, tuige yale mazuri popote pale yalipo. Sasa kwa sababu hiyo, suala la kuwa na Tume ya Uchaguzi ambayo itawajumuisha na viongozi wa vyama vya siasa, mimi nafikiri ni jambo la msingi.

Tulipokuwa na kikao cha Makatibu Wakuu wa Vyama vya Siasa vya *CUF* na CCM, mpaka tukafikia muafaka jambo hili tumeliona na likakubalika na likapitishiwa Sheria na tumeona matunda yake. Tumekuwa na uchaguzi *very smoothly,* uchaguzi mdogo uliyofanyika Pemba kwa sababu ule wasiwasi ambao humu miongoni mwetu ulikuwa umepungua kwa sababu kila mmoja alikuwa na taarifa ya kinachoendelea. Tusisahau ni miaka kumi na mbili imepita nchi yetu ilikuwa haruhusiwi mtu mwingine yeyote kuwa na chama chochote kingine zaidi ya chama kimoja CCM.

Kwa hiyo, hata Majaji, Mwanajeshi huwezi kwenda Chuo Kikuu kama siyo mwanachama, tusisahau hayo na bado mawazo hayo yapo. Kwa hiyo, si rahisi kuamini kwamba huyu mtumishi wa Serikali hayupo kwenye chama cha siasa ni taabu sana

kuamini hivyo. Kwa hiyo, angalau sasa tuanze huu uzoefu wa kuanza kutoka katika mfumo tuliokuwa nao tunaingia katika mfumo mpya, mimi nafikiri lazima kujenga uaminifu.

Mimi nafikiri tuendelea kabisa kukubaliana na pendekezo hili la kuwaruhusu viongozi wa kisiasa kuingia katika Tume ya Uchaguzi ili tuondoe zile shaka ambazo zipo ambazo hatimaye zinaweza zikatujengea uhasama usiokuwa na sababu. Kwa hiyo, hili pendekezo naunga mkono na naomba Waheshimiwa Wabunge kwa mtazamo huo walikubali.

Mheshimiwa Spika, suala la wanawake nakubaliana kabisa na pendekezo hili na naomba kusema tu katika mila zetu za Watanzania bado mwanamke kupewa nafasi ya kuchaguliwa katika jamii siyo rahisi sana. Kwa hiyo, lazima tutafute utaratibu ambao tunawezesha angalau na wao wakajijengea uwezo wa kuwa na *confidence* na hatimaye nao wakaweza kwenda kugombea. Kwa hiyo, utaratibu huu ni mzuri lakini naomba vile vile wanawake waitumie nafasi hii sasa kuweza kujijengea uhalali wa kuchaguliwa kwa wananchi. Wamepatiwa nafasi ya kuingia kwenye nafasi hizi kwa njia hii, kwa hiyo, watumie nafasi ile ile ya kupata kura kwa wananchi ili waweze kuchaguliwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala la uteuzi wa nafasi kumi za Rais, kuna pendekezo kwamba Rais awekewe mipaka kidogo katika kuchagua watu hawa. Mimi nafikiri siyo wazo baya na nitatoa uzoefu.

Katiba yetu Kifungu cha (67) hakizuii Rais kumchagua mtu yeyote kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano ilimradi ana akili timamu, anatimiza masharti ya kuwa Mbunge. Lakini uzoefu umetuonyesha kwamba hakuna hata wakati mmoja Rais amemchagua mtu au amemteua mtu nje ya chama chake isipokuwa baada ya muafaka huu uliotokea hivi karibuni ambapo mimi nimepata nafasi hiyo na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar amemchagua Mjumbe mmoja kuingia katika Baraza la Wawakilishi. Sasa inaonyesha wazi kama hukumwekea mipaka Rais ataelemea tu upande anaotaka yeye. Sasa hiyo siyo nzuri sana kwa sababu Katiba inamwambia anayo haki ya kuchagua Mtanzania yeyote anayetimiza masharti ya kuwa Mbunge aweze kumteua kuwa Mbunge.

Lakini nasema uzoefu wa vipindi vyote tangu tulipoanza na awamu ya kwanza, ya pili haijapata kutokea hata siku moja akatokea Rais akamchagua mtu ambaye hayupo katika chama cha siasa kile ambacho yeye anakiongoza. Sasa mimi nafikiri kumwekea mipaka ni jambo zuri na uzoefu vile vile umeonyesha hapo Wabunge tunaruhusiwa kuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma. Lakini hakuna Mbunge hata mmoja wa Kambi ya Upinzani kwenye Mashirika ya Umma na Mawaziri haiwafungi kabisa kuwateua Wabunge hao kuwa Wajumbe wa Bodi. Sasa huo ndio uzoefu unavyoonyesha. Kwa hiyo, ni vizuri tukaweka mipaka hii ikasaidia ili kuondoa ule wasiwasi kwamba huyu mtu anaweza kuyatumia haya madaraka yake vibaya.

Mheshimiwa Spika, suala la mgombea binafsi limezunguzwa na naomba tena niseme kwamba nchi yetu tumeingia katika huu mfumo wa vyama vingi. Lakini Rais

tumemsikia akisema hapa kwamba bado kuna udhaifu katika vyama na kwa sababu tulitoka katika mfumo wa chama kimoja kwa muda mrefu wananchi bado pia hawajajenga *confidence* na baadhi ya Vyama vya Siasa. Sasa njia peke yake ya huyu mtu ni kumpa haki yake kikamilifu, ni kumruhusu akaweza kugombea nafasi anayoitaka kwa kupitia utaratibu ambao utawekwa na Sheria na Katiba. Kwa hiyo, mimi nafikiri hatuwezi kutoa haki upande mmoja na upande mwingine tunauvuta. Ningeomba kabisa tukubaliane na maamuzi yale ya Mahakama ambayo yalikuja kubadilishwa baadaye kwamba mgombea binafsi aruhusiwe katika nchi yetu katika ngazi zote. Itatusaidia sana kujenga amani na umoja katika nchi kwa sababu hii mifarakano inayotokea ndani ya vyama ni ule ukiritimba uliomo ndani ya vyama ambavyo umewekwa kwenye Sheria na Katiba. Hili ni jambo baya sana, siyo zuri hata kidogo, tusiwanyime watu nafasi yao ya kugombea nafasi za uongozi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba tu kusema kwamba suala la *simple majority* katika kushinda Uchaguzi wa Rais. Mimi ningeomba sasa tufike mahali tuseme huyu Rais lazima akapate asilimia angalau 51 ya kura za wananchi wa Tanzania ndio achaguliwe kuwa Rais. Nasema hivyo kwa sababu kutakuwa na Rais ambaye wakati mwingine kwa sababu ya vyama vingi tulivyonavyo amepata asilimia 35 tu lakini anaonekana ni mshindi. Inawezekana kabisa kwa sababu kuna vyama vingi huyu kapata kura 15 mwingine 20, kila mmoja kachukua chukua tu. Sasa hiyo siyo nzuri sana, haileti utaratibu mzuri sana kwa hiyo, nafikiri nalo lingeangaliwa

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho ni suala la Zanzibar kama Mheshimiwa Bernard Membe, alivyosema. Mimi nakubaliana naye kabisa. Kuna haja kabisa ya kukaa na kuyatafutia uvumbuzi matatizo yetu ya Muungano. Yapo malalamiko ya msingi kama watendaji wanafikiria wanaonekana ni wakorofi, wanasiasa tunaweza kabisa kuyatatua matatizo haya. Wakae Wabunge na Wawakilishi pamoja tuyazungumze matatizo haya, tuchukue taarifa za Jaji Robert Kisanga na Jaji Francis Nyalali zinatosha kabisa kuyatatua matatizo haya ya msingi. Hatuwezi kuendelea na mambo haya kila siku yanarudisha nyuma maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, leo tunakataa kuchimba mafuta. Dunia ya leo mafuta yanachimbwa kila kona ya Afrika. Tutakapokuja kuamua sisi nani atakuja tena ku-*invest?* Watasema haya mafuta yako tele nani ana hamu tena ya ku-*invest*. Kwa hiyo, haya ni mambo ya msingi kabisa ya kuangalia kabisa tusipoteze muda hapa kwa kulumbana bila ya sababu, tueleze kuna tatizo la kukaa kitako tukayatatua matatizo ya Muungano ili tuwe na Katiba itakayojitahidi kwa kiwango kikubwa kutatua matatizo haya na tusirudi hapa Bungeni kurudia tena maneno hayo kila siku. Ni aibu sana, Tanzania imejijengea uwezo wa kuweza kutatua matatizo yetu.

Mimi sikubali kabisa kama hili ni tatizo kubwa, ni tatizo dogo mno, lakini hatutaki kuwa wazi tukayazungumza matatizo, wananchi na viongozi wakayafahamu ili kuyatatua. Lazima tukubali, mimi nashangaa kabisa maana sasa hivi Serikali zinazotawala zote ni za Chama cha Mapinduzi. Mnapokuja hapa mnasema kuna matatizo sasa matatizo hayo yanatokea wapi. Maana hakuna Serikali ya Upinzani ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi zote mbili halafu mnatuambia bado kuna matatizo hayawezi

kutatuka, atayeyatatua ni nani sasa. Sasa tushirikishwe wote tuyatatue matatizo haya. Lakini nasema ni aibu kubwa sana kukaa hapa tukasema kwa muda wa miaka 40 tuna matatizo, hatuwezi kuyazungumza.

Mheshimiwa Spika, mficha uchi hazai, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kuhusu marekebisho ya Katiba. Ningependa kumpongeza sana Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba pamoja na Kamati iliyokaa na kuchambua marekebisho haya na kutuletea, nasema wamefanya kazi kubwa sana kwa hiyo, ningependa kuwapongeza.

Mimi ningependa kusema machache kuhusu marekebisho haya. Nianze na haki ya mtu, Katiba yetu imefafanua kabisa na kulinda haki ya mtu na kimaandishi kwa kweli kila mtu anaona kwamba ni sawa na sahihi. Lakini hii haki wakati mwingine baadhi ya watu wanakosa hii haki. Kuna mambo mengi yaliyozungumzwa na Wabunge wenzangu hasa suala la Majaji kuwa wachache katika nchi yetu. Kuna watu wengi wanasota rumande kwa ajili ya kukosa Majaji wa kusikiliza hizo kesi. Halafu najiuliza hivi sasa ni kosa la nani, ni kosa la mtuhumiwa au la nani au siyo ukiukwaji wa haki ya mtu hapa na hatujaitupia Serikali kwamba ndio wamevunja haki ya mtu kumweka rumande inawezekana huyo mtu hakuwa na kosa. Amekaa miaka miwili baadaye anaachiwa hana kosa sasa hiyo fidia nani anaweza akafidia miaka miwili aliyosota rumande.

Kwa hiyo, naona hiyo irekebishwe kwa gharama yoyote na Majaji wapatikane wa kutosha wa kuendesha kesi za wananchi. Haki nyingine tunayokosa na Wabunge wenzangu wamezungumzia sana, mtu wa hali ya chini ambaye hawezi kujitetea kwa njia nyingine. Hii rushwa inawanyima wanyonge haki. Matajiri wanawanyanyasa kabisa watu ambao hawana uwezo kwa ajili ya rushwa. Pesa ndio inatawala siku hizi, siyo haki, usipokuwa na pesa basi wewe huna haki. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba na hiyo haki iliyoandikwa kwenye Katiba inayomlinda mtu inapotezwa na rushwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni hizi nafasi kumi za Wabunge wanaoteuliwa na Rais. Kwanza naipongeza sana Serikali kufuta au kuahirisha ile Tume ya Ushauri, ningependa wangepeleka pamoja na hii. Hizi nafasi kumi apewe Rais mwenyewe siyo kubanwa tena kwamba wachukue watu hawa na hawa. Hivi Rais anapoteua Baraza la Mawaziri, nani anayemwambia kwamba awaweke wanaume kadhaa na wanawake kadhaa, anatumia busara tu anawachagua anavyoona yeye mwenyewe. Anavyowateua Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na *DCs*. Kwa hiyo, hili liende sambamba na nafasi hizo, ateue anavyotaka mwenyewe. Ningeomba na hili Mheshimiwa Waziri baadaye ukitoa majumuhisho upitishe kwamba na hili limefutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kulizungumzia hili suala la Muungano. Mwenzangu aliyechangia sasa hivi alichukua sehemu kubwa ya mchango wangu. Lakini ningependa kusema kama una jipu ukawa unalipapasa tu unasema kwamba silipasui kwa

sababu linauma hilo jipu litajengeka kama lilikuwa ni dogo linakuwa kubwa zaidi na baadaye litakwenda kupasuka lenyewe hata kama hutaki. Kwa sababu ule usaha hauwezi ukawa nyama ni usaha tu na ukikosa kwa kupita utajipenyenza. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba hili jipu tusiogope kulipasua wala hatujui kama lina nini. Hayo matatizo ya Muungano viongozi wote wanapata shida hakuna mtu anayeweza akamjibu mwananchi yeyote atakayekuuliza suala la Muungano. Hakuna mtu mwenye jibu kamili anasema kuhusu Muungano, wewe acha tu yaani kila awamu inapita inasema kwamba acha awamu hii ipite, acha uchaguzi huu upite. Hivi tutaacha mpaka lini?

Hapa hapa tunaanza kurushiana wenyewe sisi Wabunge kelele tu. Kwa hiyo, mimi nilitegemea kabisa kwamba katika marekebisho ya 14 ya Katiba na hili suala la Muungano lingewekwa kabisa, lingekuwa ndio *point* ya kwanza ya kuzungumzia. Tunapoacha suala hili bila ya kuzungumzia, kwa kweli mimi naona litaleta matatizo baadaye. Leo asubuhi wenzetu waliuliza mgao wa 4% imepitwa na wakati na mimi nasema hivi kipengele cha kumpa 4% ni nini, ni ukubwa wa nchi au watu? Kwa sababu kama ni watu, nadhani Mwanza ina watu wengi kuliko Zanzibar. Kwa hiyo, nikasema siyo watu kwa sababu ingekuwa ni watu wasingepata hii 4%. Hayo ni mambo mengi tu ambayo yanaleta wasiwasi na mashaka na tusingependa kuwa nayo kila wakati. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni mgombea binafsi, mimi naungana na Wabunge wenzangu waliosema kwamba waruhusiwe wagombea binafsi wasinyimwe. Kwa sababu nikizungumzia chama siyo Chama kimoja (CCM) vyama vyote. Vyama ni watu na Viongozi waliopo ni watu, kuna tofauti tu nikianza kugombea yaani viongozi walioko katika Chama hawataki kabisa nigombee natoa tu mfano wangu. Kwa hiyo, nanyimwa tu kugombea kwa ajili ya viongozi, lakini watu wananitaka. Sasa nakosa nafasi ya kugombea kwa ajili ya fulani na fulani lakini wananchi wananitaka. Nitoe mfano wa Mheshimiwa Danhi Makanga. Mheshimiwa Danhi Makanga, alifukuzwa na viongozi wa Chama lakini wananchi wakasema kwamba Mheshimiwa Danhi Makanga, sisi tunamhitaji ni wale watu wake wa *UDP* ndio walimpigia Mheshimiwa Danhi Makanga, kura wakamrudisha hapa hata bila ya *UDP* kutaka. Lakini alirudishwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba kupitia kwako ningeishauri Serikali kwamba hili jambo la mgombea binafsi liruhusiwe kabisa na iwekwe katika Katiba ili wakati mwingine hata viongozi hata chama. Hiyo itaimarisha chama kwa sababu itajenga ile heshima. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja na baada ya hayo sina mengi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nichangie Muswada huu wa Sheria ya mabadiliko ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa mwaka huu 2004. Mimi naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu na kwa kweli umewasilishwa vizuri na Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie mapendekezo yanayoletwa kwenye Ibara ya 20 ya Katiba. Kwanza inapendekezwa kuifuta Ibara ndogo ya kwanza na kuiandika

upya. Ukilinganisha Ibara hiyo ndogo ya zamani na hii inayoandikwa upya, hakuna tofauti yoyote ya msingi inayofanya kufutwa kwa Ibara hiyo ya kwanza au ibadilishwe. Sura ambayo inajitokeza katika marekebisho haya ni kwamba sasa uhuru hautadhibitiwa na sheria yoyote ya nchi. Sentensi inayosema kwamba sheria za nchi ndizo zitakazodhibiti uhuru wa mtu imeondolewa. Maana yake sasa uhuru utakuwa ni uhuru huria. Sina uhakika sana kama tumekwishafika na hali ya kuwa na uhuru huria. Tuna amani ni sawa lakini sidhani kama kuna nchi yoyote duniani ina uhuru ambao hauna mipaka. Kwa hiyo, mimi nashauri hapa marekebisho haya yasingechukua sura hiyo.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa vile vile Ibara ndogo ya pili ifutwe iandikwe upya. Mabadiliko yaliyokusudiwa kufanywa katika Ibara hii ndogo mimi sina matatizo nayo nayaunga mkono mia kwa mia. Lakini siungi mkono sehemu ya Ibara ndogo ya nne iliyofutwa na kuandikwa upya hadi hapo nitakapopata maelezo ya kutosheleza. Ibara hii ndogo ya nne ina sehemu mbili, sehemu ya kwanza inasema hivi; “Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimishwa kujiunga na Chama chochote au shirika lolote.” Sehemu hii ya Ibara ndogo inayopendekezwa naikubali sina matatizo nayo. Naikubali kwa sababu mtu hawezi kulazimishwa kujiunga na Chama chochote na ukifanya hivyo utakuwa umemwondolea uhuru wake wa Kikatiba ambao unalindwa na Ibara hiyo hiyo ya 20(1).

Kwa hiyo, madhumuni ya kurejea uhuru huu katika Ibara ndogo ya nne ni kutoa mkazo tu na umuhimu wa pekee. Sehemu hii ya kwanza ya Ibara hii naiunga mkono mia kwa mia. Sehemu ambayo siungi mkono kabisa ni ile ambayo inasema: “Itakuwa ni marufuku kwa chama chochote cha Siasa kukataliwa kusajiliwa kwa sababu tu ya Itikadi au falsafa ya Chama chake.” Sehemu hii ya Kifungu hiki kidogo cha nne nashauri iondolewe.

Kwanza inapingana na Ibara ndogo ya pili niliyoitaja juu. Ukisoma ile Ibara ndogo ya pili na mtiririko wake, halafu ukasoma kipengele hiki ninachokizungumzia utaona jinsi inavyopinga moja kwa moja. Kwa sababu inapinga na Ibara Ndogo ya pili, inaanzisha mgogoro ndani ya Katiba. Mgogoro ambao siyo wa lazima.

Pili, Katiba siku zote kazi yake ni kuweka misingi ambayo sheria nyingine zitatungwa juu yake. Kwa hiyo, kuweka kipengele ambacho sheria zitakazotungwa juu yake zitaleta mgogoro ni jambo la hatari. Pengine niseme kidogo nini maana ya Itikadi na falsafa. Kwa mujibu wa John Nellis katika kitabu chake kinachoitwa *A theory of ideology of the Tanzanian, example* ukurasa wa 19. Itikadi maana yake; *a set of values and ideas that justify and irrationalise the programmes a system carries forward* yaani Itikadi ni mkusanyiko wa mawazo ambayo yamejengeka na kutumika kutoa na kuhalalisha mwelekeo fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu ninukuu: “Falsafa ni elimu asili maana na sababu za mambo na vitu mwenendo wa maisha ya binadamu” Kwa hiyo kila chama cha siasa duniani, lazima kiwe na Itikadi na Falsafa yake. Kwa kweli mambo haya mawili ndio yanayofanya kuwe na mkusanyiko wa watu na wajiunge katika Chama. Kwa sababu wanakubaliana katika Itikadi na sera lazima kiwe na itikadi na Falsafa yake na kweli mambo haya mawili ndio yanayofanya kuwe na

mkusanyiko wa watu na wajiunge katika Chama. Kwa sababu wamekubaliana katika Itikadi, Falsafa na Sera za Chama cha Siasa, zinatokana na itikadi na falisafa ya msingi ya chama hicho na utekelezeji wake unatafsiriwa katika Katiba na sera za Chama.

Kwa hiyo, najenga hoja kwamba Katiba na Sera za Chama chochote cha Siasa haziwezi zikatenganishwa na Itikadi na Falisafa za chama hicho. Kwa msingi huo najenga hoja ya pili kwamba ubaguzi wa aina mbalimbali unaweza ukawa ni Itikadi na Falsafa ya Chama cha Siasa na ukawekwa katika Katiba na Sera za Chama hicho. Katika historia ya dunia kumekuwepo na Vyama vya namna hiyo, Afrika Kusini kulikuwa na Chama cha Ubaguzi kilikuwa na Itikadi na Falsafa za kibaguzi na kilisajiliwa na kiliandikishwa.

Mheshimiwa Spika, mapambano kwa kutumia nguvu kufikia malengo ya kisiasa yanaweza kabisa yakawa ndio itikadi na falisafa ya Chama Cha Siasa na sera za Chama hicho zikaonyesha namna ya kutumia nguvu katika kufikia malengo ya kisiasa. Katika historia ya dunia kumekuwepo na Vyama vya namna hiyo vyenye itikadi na falsafa ya mapambano ya kitabaka katika nchi za Ulaya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, zipo falsafa na itikadi za kiimla duniani ambazo hazitaki kusikia kitu demokrasia na hivyo kujiwekea sera na Katiba zinazoondoa demokrasia katika Vyama vya Siasa. Kwa nchi zinazoendelea hili ni jambo la kawaida kabisa. Unakuta Chama kinakuwa ni mali ya mtu mmoja. Hakuna uchaguzi na hata ukiwepo hakuna demokrasia na vipo Vyama vya namna hiyo. Sasa marekebisho yanayoletwa sehemu ya pili ya Ibara ndogo ya (4) yanataka Chama chochote kisikataliwe kusajiliwa hata kama itikadi na falsafa yake ni ya kibaguzi, ya kiimla, haitaki demokrasia na haitaki amani. Hivi kweli ndivyo tunavyotaka nchi hii iende? Chama kisikataliwe kusajiliwa hata kama itikadi yake na falsafa yake ni ya udini, ya ukabila, ujimbo, rangi na jinsia, hivi kweli hivyo ndivyo tunavyotaka kwenda?

Kuyaondoa masharti ya Ibara ndogo ya (2) na kufungua milango kwa Chama chochote chenye itikadi na falsafa yoyote. Je, huko ndiko kujenga? Je, Wasukuma wakitaka waanzishe Chama chao cha Siasa kwa ajili ya maslahi ya kabila lao la Wasukuma, mabadiliko yanayoletwa katika Katiba hii leo yanasema ruksa kuanzisha Chama hicho cha Kisukuma? Mimi naogopa kukubali mabadiliko haya kwa sababu yatatufikisha pabaya. Hivi walokole wakitaka kuanzisha Chama chao cha Siasa na kuweka itikadi ya kulia na kuweka sera mtu akiwa mgonjwa asipelekwe hospitalini ila aombewe; kwa mujibu wa marekebisho haya tunayoletewa leo, Chama hicho ni ruksa kuandikishwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hivi ndio sawa! Hivi kukitokea watu wakitaka kuanzisha Chama chenye kudai malengo ya kisiasa kwa mapambano ya silaha na kuwa na sera za jino kwa jino, hawa nao ruksa? Kwa mujibu wa marekebisho haya ni ruksa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nategemea Serikali imenielewa kwamba sehemu hii ya pili ya mabadiliko Ibara ya nne inayotaka Chama chochote kisisajiliwe bila masharti yoyote, sio tu kuna hatari ya watu wengine kukosa uhuru na haki yao za kiraia lakini kinyume kabisa

cha dhamira na misingi ya Katiba yetu, kifungu hiki kiondolewe, basi kikiondolewa kifungu hicho mimi nitaunga mkono mabadiliko haya na kisipoondolewa mimi sintaunga mkono. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES ALEX MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi nichangie hoja ambayo ilitolewa na ikaungwa mkono na kwamba ijadiliwe. Napenda na mimi kuichangia kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kitu kimoja ambacho nimegundua ni kwamba ukitaka kuandika Katiba ambayo utapata mwongozo wa kila kitu unajisumbua, kwa sababu hutafanikiwa. Lakini vile vile nimegundua kwamba ukitaka kuandika Katiba ambayo hata ile *wisdom* yako haitatakiwa kufanya kazi, vilevile unajisumbua, kwa sababu kuna mahali lazima utahitaji kutoa tafsiri ambayo pia inaendana na *wisdom*, inaweza kuwa ya viwango mbalimbali lakini bado busara itatakiwa. Kwa hiyo, nataka niseme kwa maneno mengine kwamba, inabidi ifike mahali ndani ya Katiba tukubaliane yale ambayo tunafikiria yanatawala kama thamani ya jumuiya kwa wakati huo na yatambulike kwa mtazamo huo na basi ufafanuzi unatolewa kwenye sheria nyingine. Lakini nafikiri hiyo itatusaidia kuepuka kurudi kila kwenye Katiba, kwa sababu baadaye tutakuta tunabadilisha Katiba mara nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna haya ambayo yamekuja. Mimi nilikuwa nafikiria mengine yako kwenye viwango ambavyo yangeweza kupelekwa kwenye sheria ambazo zinaisapoti Katiba. Kwenye Katiba labda kungekuwa na misimamo. Maana yangu ni kwamba, ili kule kwenye zile sheria tuweze kuwa *adoptive* zaidi kulinga na hali hizi *dynamics* za maisha. Wakati mwingine zinatupeleka kwenye ukingo ambao hatukuutazamia kabisa. Kwa maana pamoja na kuwa yamekuja haya ndio yatafanyiwa uamuzi, lakini nilikuwa nafikiria kwamba kuna mengine yangeachwa au mengine yangepunguzwa. Lakini hata hivyo nichangie *directly* kwenye machache ambayo nafikiri muda unaweza kuniruhusu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni wazo ambalo napenda niliseme kwa sauti ni namna ya kuamua ambayo yameelezwa kwenye Ibara ya (98). Unapofanya maamuzi juu ya mabadiliko ya Katiba, imeelezwa kwenye kifungu cha 98 ndani ya Katiba hii tunayoitumia nchini hivi sasa. Sasa pale wanasema unatumia theluthi mbili isipokuwa kuna baadhi ya mambo ambayo yameainishwa pia kule ndani. Sasa mimi niseme kwamba unapojadili Muswada kama huu ambao tunaujadili leo, kuna mapendekezo mengi sana ambayo wengine utakuta unayakubali mengine unayakataa. Lakini inatakiwa iamuliwe kama Muswada, sasa mkibishana watoa hoja na wachangiaji kwa maana ya Wabunge kwenye hatua fulani, lazima hata hivyo kuwe na kitu ambacho tunakubali kama ni kitu ambacho kinaweza kupita hata kama baadhi ya mambo huko ndani wengine hawayapendi.

Kwa hiyo, kwa sababu ya hii theluthi mbili mimi nilikuwa nadhani labda inahitaji kutazamwa vizuri hapo kwamba labda kuna baadhi ya vifungu ambavyo ni muhimu sana ambavyo vingependa venyewe vifanyiwe maamuzi ya hiyo theluthi mbili na wala si kwenye Kamati ya Bunge Zima. Iende kwenye rekodi kwamba hayo ndio yalikuwa

maamuzi rasmi kwa theluthi mbili kwa maana ya kwamba nguvu ya wengi iheshimike. Lakini hilo ni wazo ambalo nilikuwa nafikiria linaweza likapata kuangaliwa katika siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, niseme katika suala la kuongeza hii asilimia ya Wabunge wanawake na nilikuwa najitahidi sana kuangalia sijapata mahali ambapo vimeandikwa Viti Maalum. Kwa kweli nimejitahidi lakini mtaniwia radhi kama labda kuna mahali pako, lakini sijapaona. Lakini niseme kwamba hili wazo ni jema, nafikiri ni hatua nzuri na ninataka niamini maadamu tumeandika na mimi moja kati ya maeneo ambayo najua tutarudi si baada ya muda mrefu ni eneo hili. Kwa maana nyingine ni kwamba, naweza nika-*guarantee in the next ten, five years* tutarudi kwenye Katiba kuangalia hili kwa sababu hii ni asilimia ndogo, kwani wanawake hapa Tanzania ni asilimia 52 na duniani, wanawake ni zaidi kuliko wanaume. Sasa hii ni *affirmative action* na sisi tumejikita kwenye hiki kiwango cha asilimia 30. Ingawa inasema si chini asilimia 30 lakini bado tunajua maamuzi ni asilimia 30. Kwa hiyo ina maana kwamba siku nyingine tutarudi na si mbaya na ndio maana nilikuwa nasema ni kifungu kizuri kwa wakati wa sasa, lakini nacho kinatuambia kabisa tutarudi kwenye Katiba.

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa nataka niseme kwamba kama ningeulizwa wewe unataka asilimia ngapi ningesema kwa mujibu wa *census* hivyo hivyo asilimia 52. Lakini tatizo langu hapa ni namna ile *formula* ya kuwapata hawa Wabunge. Jinsi ilivyoelezwa inaonekana inatembea tembea haijatulia, mara wanajikita kwenye Urais, mara wanajikita kwenye Wabunge, haijatulia na hii nafikiri inawapatia kazi kubwa sana wale ambao watabidi wapitishe hayo majina ya hao Wabunge wa Viti Maalum nitumie neno hilo. Mimi nilikuwa nadhani maadamu sasa tunafahamu idadi ya juu ya Wabunge ambao wanatakiwa na nafikiri ulitaja ni 322, basi kwa nini tusi-*assign percentage?* Kwa kila fungu. Wanalo fungu la viti kumi vya Rais, wawakilishi watano, Majimbo 231 una-*assign percentages*. Lakini la pili kwa sababu moja kati ya masharti ambayo tuna-*operate* nayo sasa hivi ni kwamba Wabunge wawe ni wale ambao wamedhaminiwa na Vyama. Kwa maana nyingine ni kwamba tunatambua umuhimu wa *origin* ya huyu Mbunge na mimi nadhani hapa ndio mahali penyewe pa kuanza ku-*zero in* katika namna ya kuwapata wale Wabunge wa Viti Maalum, mimi kwangu ingekuwa ni *simple* na *straight.* Kuna Wabunge X ambao wanaweza wakapatikana moja kwa moja kwenye kura, basi *assign percentage* yako. Kwa mfano, Wabunge 231wanapatikana kwa Majimbo, *you assign that percentage out of three hundred twenty two.* Sasa unakwenda na mahesabu hayo.

Niseme hapa tunachofanya ni maamuzi ya kisiasa, lakini katika kuwapata hao watapiga hesabu, hawatakwepa hilo. Ndio maana nilikuwa nafikiria kwamba hapa ni suala la hesabu, hapa ni *arithmetic* gani itatumika? Mimi nilikuwa nafikiri ku-*assign percentage*, lakini sasa lazima u-*define* vizuri una-*assign percentage* kwa Wabunge wa Chama kupitia kwenye Majimbo. Sasa utakuja utapata *percentage* ya wanawake wa chama hicho kutokana na *percent* ya Wabunge waliopita kwenye majimbo. *Similarly* utakuja kwa Rais, *we don't have to even tell him* kwamba wasipungue asilimia hamsini, sheria imeshambana tayari ukitaka kufuata *logic.* Mimi ndio ninavyoona. Ipo tayari hapa, tumeshasema isiwe chini ya asilimia 30, ataharibu uwiano. Kwa sababu kama akichagua wanaume tu inamaana anaharibu uwiano, lazima na yeye a-*maintain* hilo hilo. Ndio

maana nasema hilo la kumwambia walau asilimia 50 tuliondoe ni kurudia rudia nafikiri liondoke tu kwa sababu tayari hapa tumeshamwambia *30 percent* anatakiwa ku-*observe* hiyo.

Sasa na yeye hivyo hivyo akianza kuchagua na yeye a-*observe* hiyo kwa sababu tunakuja humu ndani kupitia kwenye vyama, kama atakuwa anateua kwa busara yake na mimi nasema ni sawa kabisa kwamba hapa Wabunge wa CCM, kwenye 10 mimi nitaweka watano, kwenye chama fulani ninachokipenda watakuja wawili. Sasa afate *proportion* hiyo hiyo ili asiharibu uhusiano au uwiano, nafikiri hilo linajimaliza moja kwa moja.

Sasa suala ni kwamba kwa sababu hii *attempt* ya kuweka hizi hesabu ipo humu ingawa haijajionyesha, ni busara kuiweka hapa *the arithmetics* ya jinsi ya kuwapata ipo tayari nafikiri inatakiwa tu kuelezwa sawa sawa hapa na nasema kwa aina zote za Wabunge na baadaye utapata kila *percent* ina-*fetch* Wabunge wangapi kuingiza kupitia Viti Maalum.

Lingine ni hili la dini, katika Muswada huu tulioletewa Ibara ya 4, wanapendekeza kufanya mabadiliko kwenye Ibara ya 19 ya Katiba kwenye kifungu cha pili. Mimi nilikuwa najiuliza nikawa napata taabu sana. Nafikiri dhamira hapa ni kutamka. Kuna maneno nimegundua pia kumbe si rahisi sana kuyaandika kwenye Katiba lakini unaweza ukayatamka kwa urahisi tu. Kwa mfano unaweza ukasema nchi hii haina dini na watu watakuelewa, lakini ukitaka kuelewa kimsingi kabisa utaanza kujiuliza kwa nini na namna gani.

Mheshimiwa Spika, hapa asubuhi unapofungua Bunge lako Tukufu unaanza kwa sala na hiyo sala inamtamka bayana Mwenyenzi Mungu na mimi nafikiri hiyo *appeal* yetu sisi kwenda kwa Mwenyenzi Mungu tayari *by itself* ni *acknowledgement* ya chombo hiki ambacho pia ni sehemu ya muundo wa nchi yetu. Sasa mimi nilikuwa nafikiria hapa suala kumbe ni kukiri tu kwamba Serikali ama inatambua kuwepo kwa Mungu ama haitambui kuwepo kwa Mungu basi. Mimi nafikiri tukiri hapa kwamba *in God we trust,* tunaamini kwamba Mungu yupo ndio tunavyosali hata kwenye Bunge hapa. Hilo la kwanza.

Lakini la pili ukisema dini wakati mwingine unapata matatizo sana, labda useme dhehebu kwa mfano unasema mamlaka ya nchi haitakuwa na dini yoyote lakini hapa dhamira ilikuwa ni ile ya kusema kwamba sisi hatutakuwa na dini rasmi.

Sasa nilikuwa nataka niseme ama kifungu kile kile kilichoko ndani ya Katiba kilivyo sasa kibaki hivyo hivyo kwa sababu mimi nimekiangalia kwa kukisoma kwa dhamira ile ile inaonekana bayana kabisa kwamba Serikali kama chombo cha usimamiaji na utoaji wa *service* na haki hakitakuwa na mwelekeo wowote unaotawaliwa na *any of these ideologies* za kidini nafikiri hilo lipo. Sasa kama hapo walikuwa wanafikiria ni muhimu kuliweka basi napendekeza. Basi kama hii *version* iliyopendekezwa hivi sasa wanaitaka ni bora wakaongezea neno rasmi baada ya ile yoyote waseme mamlaka ya

nchi haitakuwa na dini yoyote rasmi, waseme hivyo na kwa kusema hivyo mimi najua kwa *implication* tayari tushasema Mungu yupo.

Mheshimiwa Spika, labda nitumie muda wangu uliobakia mchache kwa kusema hili moja. Nashangazwa na kelele ambazo nimezisikia huko mitaani kwamba kuna watu sijui walitaka kuandamana kuhusu haya mambo nani atakaimu nafasi ya urais.

Mimi nataka kusema kwa kweli Mheshimiwa Bernard Membe, amelieleza vizuri sana na mimi naungana naye asilimia mia moja. Lakini pia nataka niseme moja ambalo nafikiri watu hawalioni hapa. Tunazungumzia hapa mtu atakaye kaimu nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, huyo mtu lazima awe na sura hiyo hiyo. Anatoka kwenye chombo cha namna hiyo kinachosimamia shughuli za Muungano, *he can't be less. (Makofi)*

Mniwie radhi kwa kusema hivyo, lakini huu ndio ukweli kwa sababu huwezi kwenda kukaimu kwenye nyumba ya mwenzako wakati mtoto mkubwa tu yuko pale, utatokaje wewe jirani ukakaimu kwenye nyumba ya mwenzako? Haipo hiyo. Kama baba anataka kuondoka na anafikiri ni muhimu kuna mambo ya kusimamiwa, atamchagua mtoto mkubwa kama na mama pia hayupo. Hawezi kwenda kumchukua jirani wakati bado kuna watu pale, haipo, *it doesn't make sense,* isipokuwa anaweza kumwambia, ukitaka ushauri, yule mzee fulani namwamini. *(Makofi)*

Sasa mimi niseme tusiwe tunaingiza jazba kwenye mambo bila ya kuwa tumeelewa kina chake. Mimi nadhani hili linaeleweka kabisa lilivyo na mimi niseme tu kwamba kumwongeza Waziri Mkuu ilikuwa ni *logical* lakini ile ya ku-*provide for Speaker* na Jaji ina *sense.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwa wakati huu na la pili nitoe pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati, kwa kifo kilichotokea kwa ajali ya basi, mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, sasa nichukue nafasi tena kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wao kwa jinsi walivyoandaa Muswada huu na kutuletea hapa Bungeni ukiwa wazi na unaoeleweka, nawashukuru sana kwa hilo.

Mimi niende moja kwa moja kwenye mchango wangu kwenye masuala ya Viti Maalum vya Wabunge. Nimeangalia katika Ibara ya 66 inayohusu Viti Maalum. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyoweza kuridhia umuhimu wa Viti Maalum kuongezewa asilimia ambayo inaanzia 30 na nina uhakika kwa jinsi alivyo Mheshimiwa Rais wetu na maombi anayoyasikia hapa kutoka kwa Wabunge wanawake na Wabunge wanaume anaweza akaongeza asilimia hii kwa kipindi hiki ikafika walau 40. Tunatanguliza hizo shukrani zetu kabla hajatoa idhini nyingine inayofuatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu gani tunasema hivyo, kihistoria nchi hii imekubali wanawake tulikuwa nyuma katika vitengo mbalimbali vya uongozi na sababu zinajulikana kwamba wanaume waliwahi kuelimika kabla ya sisi wanawake, tulikuwa nyuma katika masuala ya elimu, tulikuwa nyuma katika masuala mengi hata ya kugombea, zamani tulikuwa hatujitokezi.

Sasa kwa misingi hiyo kama hatutazingatia katika eneo hili kupewa nafasi ya kutosha tukaachiwa tu kwamba na sisi twende tukapambane kwenye majimbo hakika tunaweza kwa sababu tuna wenzetu hapa Wabunge wanawake, Waheshimiwa ambao wamepambana na wanaume kwenye majimbo na wamepita kwa kura nzuri tu lakini tuangalie na hali halisi. Tukiangalia hapa tuliopo wanawake na Wabunge wanaume na majimbo yao ile ukipita tu ziara ya kawaida tu basi ukirudi atafanya udadisi alisema nini huyu! Amesema anataka kugombea huko sasa zile hofu haziwezi kuisha kama hamtatuunga mkono ya kuongeza asilimia hii ambayo Mheshimiwa Rais amekwisha iridhia. Kwa misingi hiyo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, mtuunge mkono asilimia hii na nyingine ifikie angalau 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo mimi nimesoma katika mabadiliko haya, mimi nasema labda limesahaulika huenda Mwanasheria Mkuu au Mheshimiwa Waziri amesahau kuliona au Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naye amelisahau. Tuna Viti Maalum pia katika eneo la Madiwani halijatajwa mahali popote.

Mimi nilikuwa naomba sana kama limesahaulika basi Mawaziri wanaohusika walishughulikie hili mapema ili na wao waweze kuongezewa asilimia ifike 40 katika Viti Maalum vya Udiwani na sisi lazima tuangalie kwamba hawa Madiwani ndio wanaotusaidia kufagilia majimbo yetu.

Mheshimiwa Spika, tunapowasahau kuwasemea ndani ya Bunge hili na wao wanasononeka. Nasema hivyo kwa sababu tunasikia, tunazungumza nao, Waheshimiwa Madiwani wanasema wenzetu mnatusahau, hamtusemei Bungeni, hamtusemei haki zetu, basi yale ambayo tumeyasema hapa kila mmoja wetu anakumbuka tuliomba Waheshimiwa Madiwani wazungumziwe masuala ya mikopo. Lakini hilo halikuwezekana, basi tunarudia tena walau hili la kuongezea *percent* kwa vile lipo kwenye utaratibu wa chaguzi zetu, tunaomba sana Waheshimiwa Viti Maalum vya Udiwani navyo tupate nafasi ya asilimia 40 na ikiwezekana kwenye uchaguzi huu wa mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimeomba utaratibu ulioelezwa kwamba baada ya taratibu zetu za uchaguzi kupitia kwenye vyama vyetu katika asilimia hii inapelekwa kwenye Tume ya Uchaguzi. Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi ataangalia sifa za yule mgombea anastahili ndipo aweze kutangazwa.

Mheshimiwa Spika, lakini sikuona mahali palipoandikwa hilo kwa Viti Maalum na ninahofia kwamba ikiwa hili halitawekwa wazi na vizuri tunaweza yakatokea malalamiko kwa sisi wanawake tunaogombea nafasi hizi na viongozi wetu kwa misingi

tu kwamba mtu amepita vizuri amekwenda kule baadaye anatangazwa mwenzake aliyekuwa na kura ndogo anakwenda mbele na wewe ambaye umepata kura nyingi unakuwa haupo katika uteuzi ule au kutangazwa kuwa Mbunge. Lingeandikwa hapa litatusaidia na wataalam mara nyingi wanaangalia Katiba imesema nini au Kanuni imeeleza nini hatutapata nafasi ya kwenda Tume ya Uchaguzi tukaja tukajieleza mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, naomba sana hili lirekebishwe au liwekwe wazi. Kwa sababu nimesoma Kifungu Ibara ya 5 nayo sikuona maelezo ya kutosheleza kwa upande wa Viti Maalum. Kwa misingi hiyo, tulikuwa tunaomba sana marekebisho hayo yawe wazi ili wataalam watakapofikia wakati wa uteuzi tusiwe na matatizo ya aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la uhuru wa kuabudu, mimi Kisheria si mtaalam sana wa masuala ya Sheria, nimesoma Ibara hizi zinazohusika lakini nimeona fursa zingine zitatupa matatizo kwa sababu hivi sasa baadhi ya madhehebu au watu wanaopewa majukumu katika madhehebu mbalimbali wanatumia nafasi hizo vibaya.

Mheshimiwa Spika, badala ya kwenda kuelezea au kueneza neno la Mungu katika maeneo ya Misikiti au maeneo ya Makanisa wanakwenda maeneo ya hospitali, kwa mfano, pale Muhimbili utawakuta pale mtu anatoka jasho kulielezea neno la Mungu wakati mgonjwa pale anajisikia vibaya, yeye anatoa maelezo yale hayamuingii wala hayamsaidii kwa kipindi kile kwa sababu mgonjwa yuko hoi, yuko kwenye foleni. Lakini kama ingekuwa wanakwenda katika maeneo mazuri mtu anaweza akawa msikivu, akasikia na akashawishika kujiunga na dhehebu hilo.

Mheshimiwa Spika, wengine kwenye vyombo vya usafiri, wanahutubia mambo ya dini kwenye vyombo vya usafiri kama daladala na wengine pia mimi nimeshuhudia kwenye treni wanatandika mikeka, wanaswali pale na wewe unahitaji kupita uende ukapate chakula, huwezi kumkatisha mbele wakati anaswali, unahofu, unasononeka mpaka amalize ile swala ndio uweze kupita. Sasa hizo ni kero ndogo ndogo ambazo kama hazikuwekwa vizuri katika sheria hii ya uhuru wa kuabudu itatuletea kero.

Mheshimiwa Spika, hili nalo tuweze kulifanyia kazi vizuri na lisituletee matatizo. Naomba kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi. Naomba niipongeze Serikali kwa kuendelea kufuata ushauri wa katika hotuba Mheshimiwa Jaji Robert Kisanga katika ripoti yake. Lakini pamoja na kusema hayo, naomba niseme kwamba huenda ikawa tunatibu dalili badala ya kutibu ugonjwa wenyewe kwamba marekebisho yanayokuja siyo yale yanayohitajika haraka kama mengine ambayo hayaji kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, kwa hiyo, yale ambayo Mwenyekiti wangu ameyasema hapa naungana naye mkono siyo kwamba napinga Kamati. Hata hivyo, kuna mambo ambayo

ni ya kibinafsi ambayo nimeona lazima nilieleze Bunge, pamoja na kwamba tulijadili kwenye Kamati na hayo yako mambo kama matano hivi.

Mheshimiwa Spika, naanza na lile la kutenganisha madaraka ya ile mihimili mitatu ya dola. Kweli hatua zimechukuliwa; Mheshimiwa Spika hataweza kuwa tena Kaimu Rais wa nchi hii kama tutapitisha haya mabadiliko. Mheshimiwa Jaji Mkuu hataweza pia kuwa Kaimu Rais, na mimi naona hiyo ni sahihi kabisa. Maana hawezi kuwa mtawala na mtunzi wa Sheria au hawezi kuwa mtawala na mwelekezaji wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mahali pamoja ambapo Katiba inaruhusu muingiliano wa madaraka ya dola kwa kiasi kikubwa sana na hii naamini yanaingilia utendaji wa kazi wa watu na hili ni jambo la Mawaziri kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri kuwa Mbunge anakuwa na kofia mbili, anakuwa mwakilishi wa watu na wakati huo huo anakuwa mtawala. Katika kiti chake cha mwakilishi wa watu anafungwa na ule wajibu wa *collective ministerial responsibility.* Katika utawala lazima aamue na watawala wenzake. Lakini wakati huo huo lazima atetee maslahi ya wapiga kura wake.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiria wakati umefika kwamba tufikirie *seriously* Mawaziri wasiwe Wabunge na hata kama itabidi basi wakae Bungeni basi Mawaziri wasiwe Wabunge wa kuchaguliwa, watumie muda mkubwa zaidi kwenye Majimbo yao kuliko kutumia muda wao mkubwa katika Ofisi za Uwaziri.

Hili tatizo linaonekana hata sasa wakati ambapo kuna hii homa ya uchaguzi, watu wameshaanza kuulizwa mlikuwa wapi na hii ni sababu lazima amtii Rais wake, afanye kazi yake ya Uwaziri lakini wakati huo huo lazima aende kwenye Jimbo lake. Hawezi kutetea barabara ya Jimbo lake hapa kwa sababu anakaa na *Cabinet* anajua siri za *cabinet*, anajua matatizo *cabinet* waliyonayo. Mimi nafikiria hata kama itabidi wakae Bungeni wasiwe Wabunge wa kuchaguliwa.

Mheshimiwa Spika, la pili ni juu ya uhuru wa kuabudu, naomba nianze kwa kutangaza kwamba mimi ni mkristu wa *Roman Catholic*. Kwa haya ninayosema huenda ikawa yatahusisha imani yangu.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana katika Kamati kwamba yale mapendekezo yaliyokuwa yameletwa na Serikali yalikuwa sawa na hii ilikuwa baada ya Kamati yetu kwenda sehemu tofauti za nchi hii na kusikiliza mawazo ya wadau. Wale waliokuwa na mashaka tuliwakumbusha kwamba tunayo Ibara ya 30 ya hii Katiba ambayo Ibara ya 30 inasema hizi haki hazibadilishi Sheria iliyoko na wala hazizuii Bunge kutunga Sheria nyingine. Lakini pendekezo ambalo limekuja katika *schedule of amendment* limefanya hata ile Ibara ya 19 iliyokuweko inaonekana ilikuwa ni nzuri zaidi. Mimi sielewi kwa nini wanaibadilisha hiyo Ibara.

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu walivyosema huenda ikawa tunaficha jipu baadaye litatupasukia tutanuka tu.

Mheshimiwa Spika, pale Kunduchi kwangu kuna Walokole ambao wanaanza kuhubiri saa tano ya usiku na ma-*loud speaker* makubwa sana. Watoto wamelala, wazazi wamelala wanangojea kuwahi kazini kesho asubuhi, usiku kucha wanaimba na sio lazima wanawaimbia Walokole wenzao. Samahani kuna baadhi ya Misikiti pia wanaanza kuhubiri saa tano ya usiku na wanahubiri usiku kucha na mbaya zaidi sio kwamba wanahubiri dini yao. Huwezi kuihubiri dini yako kwa kutukana dini nyingine. Nikitaka kuhubiri injili nitahubiri injili, sitahubiri *quran,* kuonyesha jinsi *quran* ilivyo na kasoro.

Lakini hii inatokea. Masuala ya imani ni masuala yanayofadhaisha sana. Siyo elimu, sio utu uzima, mtu analipuka kwa sababu ya imani, vita vimetokea kwa sababu ya imani. Sasa ikiwa tutachelea jambo hili tuta-*polarize society* yetu kiasi kwamba itafika wakati tutapigana hadharani kwa sababu ya mihadhara inayotokea ya Kikristu na Kiislam. Sasa mimi nilikuwa nafikiri ile Ibara ilivyopendekezwa katika Ibara ya 4 ya ule Muswada itakuwa ni marufuku kwa shughuli za imani kueneza dini na jumuiya za kidini kutumiwa na mtu au na kundi na madhehebu ya shirika lolote na kadhalika ambayo itahatarisha usalama, mshikamano katika jamii, umoja wa Kitaifa au kuvuruga amani ndani ya jamii au katika nchi. Hiyo marufuku iwekwe rasmi ndani ya Katiba. *(Makofi)*

Sisemi hivyo kwa sababu ya dini moja. Sisemi hivyo kwa sababu ya dhehebu moja, wapo Wakristo wanaosumbua, wako Waislam wanaosumbua, wako wapagani wanaosumbua. Hii yote ni kwa sababu ya amani yetu wote. Watu wataamka usiku na bastola waende wakapige watu wanaohubiri. Mimi nafikiri huu Muswada ulivyokuwa umeletwa ni muhimu ubaki ulivyo.

Mheshimiwa Spika, la tatu nililokuwa nataka kusema ni juu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika Kamati tulikubaliana kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *Deputy Attorney-General* (Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali) na Mkurugenzi wa Mashtaka *(Director of Public Procecution)* tusiwalinganishe na Majaji. Tuseme *qualification* zao zile ambazo ni za kazi zao. Tulikubaliana hivyo na nafikiri Serikali katika Kamati ilikubali.

Lakini kilichonishtua katika *schedule of amendment* ambayo tumeletewa ukurasa wa 3, pamoja na *qualification* za Mwanasheria Mkuu kutajwa kwenye Ibara ndogo ya pili kumekuwa na Ibara ndogo ya tatu inayosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa na hadhi iliyo sawa na mtu anayeshika kiti cha Jaji wa Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, Katiba ni Sheria mama ya nchi, kuna vitu vinavyotakiwa viwekwe ndani ya Katiba na ambavyo havitakiwi viwekwe ndani ya Katiba. Kwa nini tutaje *qualification* za Jaji Mkuu kuhusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali? Serikali ni nafasi ya utendaji, kwa nini tuitaje kwenye Katiba? Mimi nafikiri kama ni mambo ya mishahara na marupurupu ni waraka wa Serikali huo. Tusitunge Sheria kwa ajili ya sasa, tutunge Katiba ambayo wajukuu wetu watasema wale wazee walifanya kazi nzuri.

Nne *DPP,* Madaraka ya *DPP* yalikuwa kwenye Sheria ya utaratibu wa kuendesha mashtaka ya jinai. Sasa tunaweka mamlaka ya *DPP* kwenye Katiba ambayo tukitaka

kumnyang'anya hayo mamlaka lazima tuje tukae theluthi mbili ya Bunge. Ni kwa nini? Kwa nini tuiondoe kwenye *Criminal Procedure Act?* Kwa nini tunatunga Sheria tunasema kuwe na Mahakama Kuu ambayo mamlaka yake itakuwa kama inavyoainishwa kwenye Sheria nyingine. Mahakama ya Rufaa hivyo hivyo. Halafu *DPP* tumwekee mamlaka yake kwenye Katiba. Mimi sijaiona kwenye Katiba yoyote popote katika dunia hii. *(Makofi)*

Pia wakati umefika hata kama tungeweka hayo mamlaka kwenye hii Katiba, hivi kwa nini tumruhusu *DPP* nikianza mashtaka yangu binafsi yeye ayaingilie na ayafute? Kwa nini tumpe hayo madaraka?

Mheshimiwa Spika, mwisho juu ya Tume ya Uchaguzi. Mengi yamesemwa hapa lakini Tume ya Uchaguzi inakuwa huru pale ambapo haifungamani na upande wowote. *(Makofi)*

Tunajidanganya kusema kwamba Tume ya Zanzibar ni huru. Ushahidi umeonekana Pemba, wakati wa uchaguzi mdogo wa Pemba. Wale waliokuwa wanaelekea CCM walisema wale waliokuwa wanagombea kwa tiketi ya *CUF* hawakuwa na sifa za ugombea. Wale waliokuwa na mwelekeo wa *CUF* kwenye ile Tume walisimama upande mwingine wakasema hawa wa *CUF* wana sifa za kugombea. Tume ya Uchaguzi inatakiwa iendeshwe kwa muafaka kwa *consensus. (Makofi)*

Mimi nilikuwa nafikiria kama tunataka hii Tume iwe huru kabisa kazi ya uchaguzi ni kazi ya Bunge. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba Tume ya Uchaguzi inakuwa chini ya Bunge kupitia kwa Katibu wa Bunge au kupitia kwa *Commission* ya Bunge. Lakini kuweka vyama ndani ya ile Tume ni kuleta malumbanao makubwa sana ambayo hayafai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, naomba nirudie tena nisieleweke kwamba napingana na Mwenyekiti wa Kamati yangu, lakini hayo niliyoyasema kwa sababu nilikuwa nayafikiria sana na naomba nitoe ilani kwamba kama Serikali haitasikia, nafikiria kutoa *schedule of amendment* niombe *backbenchers* wanisaidie. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya mwisho kwa asubuhi ya leo kuchangia katika Muswada huu wa marekebisho ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Awali ya yote niipongeze Serikali kwa kupitia Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa kuuleta Muswada huu. Kama ambavyo inavyojulikana Katiba ya nchi hurekebishwa kadri hali ya kisiasa, ya kijamii na ya kiuchumi inavyoendelea katika nchi na ndio maana sasa tuko katika marekebisho ya 14, nina hakika tunaweza tukaona mabadiliko ya 15 kwa sababu huu ni mchakato endelevu.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na kwa kweli tutakuwa tunarudia baadhi ya mambo kusisitiza zaidi.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ninalotaka nizungumzie ni kushukuru sana Serikali kwa kuona umuhimu na kuwasikiliza wadau na kisha wakaondoa lile suala la Baraza la Ushauri la Taifa. Kwa kweli limezungumzwa na wadau nje na ndani ya Bunge hili na nadhani hii inaonyesha kwamba Serikali yetu inasikiliza wadau wanasema nini.

Lakini nataka nisema kwamba katika kusikiliza wadau hao kama nilisikiliza vizuri ni kwamba Serikali imeahirisha iende kupata maoni zaidi ya wadau. Mimi nadhani hapo ndio napingana kidogo na hilo, kwa sababu wadau wameshatoa maoni yao kwamba hili Baraza liondolewe moja kwa moja. Sasa hili la kuahirishwa ili wadau wasikilizwe zaidi mimi sijui ni wadau gani kwa sababu wadau kwa kweli walishazungumzia sana na hili nadhani limefungwa sio kuahirishwa, limeondolewa, mimi nadhani lingesomeka hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kushukuru kwa kuliondoa hilo labda nizungumzie mambo mengine mawili, matatu kama msisitizo na haya kwa kweli yameshazungumzwa na Wabunge wengine na mimi nianzie na hili la uteuzi wa Mheshimiwa Rais la Wabunge kumi. Nisisitize kabisa kwamba kama walivyosema wenzangu kwa kweli hizi nafasi tumwachie Rais kwa utashi wake ateue Wabunge kumi au wachache kwa kadri anavyoona bila kuingiliwa kwa kuambiwa kwamba lazima wanawake wasipungue watano.

Nasema hivyo kwa sababu mimi nadhani kabisa kwamba nafasi hizi anazopewa Mheshimiwa Rais nafasi kumi sio kwa ajili ya *gender balance* hata kidogo. Nafasi hizi anapewa ili atumie mamlaka aliyonayo pamoja na vigezo alivyonavyo na upungufu anaouona maeneo fulani ndani ya Bunge na ndani ya Serikali yatakayoweza kumsaidia yeye kama Rais au kama nchi itakavyoweza kusaidia kama nchi. Sasa vigezo vile mimi nadhani tumwachie kama akiona kwamba vile vigezo ni lazima ateuwe wanawake wanane ndio wanatosheleza vigezo vyake basi tumwachie afanye hivyo. Kama ni wanaume saba tumwachie vile vile atumie vigezo vyake aweze kuteuwa kwa busara atakayokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, mimi nina hakika tunamchagua Rais ambaye tunajua ana busara na anaelewa kabisa ni watu wa aina gani wanaweza wakamsaidia na hizo nafasi kumi ni vigezo gani atavitumia.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia vile vile kwamba katika Katiba au Muswada huu wanasema kwamba atateua Wabunge wasiozidi kumi. Kwamba sio lazima ateue kumi anaweza akateuwa watatu, sasa kwa mfano ameteua watatu na ameona kwamba kwa vigezo vyake hana sababu ya kuteua wengine saba. Ameshapata aliokuwa anawataka au pungufu waliokuwa nao maeneo fulani na akawateuwa wanaume watatu kwa mfano. Sasa tunamfuata kusema kwamba wale wanawake watano wako wapi? Na sisi tulimwambia kwamba ateue wasiozidi kumi si lazima wafike kumi. Sasa wasipovuka watano kwa sababu umeweka kwamba wanawake wasipungue watano tunamlazimisha, lazima avuke watano. Sasa sisi tunajua ni vigezo gani ambavyo atavitumia.

Kwa hiyo, mimi nadhani suala hili ni jema kuliweka lakini lisiwe la *gender balance*. *Gender balance* tunayo maeneo na tumeyazungumzia na mimi nitakuja kuzungumzia kwenye 30% na hilo tunaweza tukalizungumza kama tunaongeza au kama alivyosema Mheshimiwa Dr. James Msekela, hata kama tukisema 50% lakani pale ndio tunajenga *balance* lakini sio katika hao Wabunge kumi tu ambao tume-*reserve* kwa ajili ya Mheshimiwa Rais. La sivyo tuseme basi kifungu hiki hakina maana tufute kabisa lakini kama tutakiacha kwa kweli tusimwingilie Rais.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni hilo la akinamama ambalo nimelitaja na mimi niseme kwamba naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu na kwa kweli sisi ndio tunapitisha ni vizuri dada yangu Mheshimiwa Esha Stima, amemshukuru Rais. Lakini jukumu la kupitisha ni sisi Wabunge, sisi ndio tunaweza tukasema 50 wala tusiseme kwamba Rais tunaomba uongeze kesho, hapana sisi hapa tukisema ni 40 hata leo tunasema ni 40 au 50.

Kwa hiyo, pamoja na kwamba tunajua Rais ameshiriki katika Baraza lake kuleta mapendekezo haya lakini mwisho wa siku ni sisi tunaamua ni asilimia ngapi leo. Kwa hiyo, tuamue tu wenyewe kwamba tunafikisha wangapi lakini mimi kwa hatua hiyo tuliofikia nashukuru sana. Kwa sababu sio hatua ndogo kwa 30% na tukizingatia kwamba bado tunawapa changamoto wakinamama waweze kugombea kwenye Majimbo.

Mimi niliwaambia pale Dar es Salaam akimama wa chama changu walikuja kwenye mkutano mkubwa sana wanawake wote wa Mkoa wa Dar es Salaam wa UWT wakasema usiogope Mbunge, maana yake Mbunge mwanaume nilikuwa peke yangu kwenye kikao kile cha akinamama na waliponiambia Bwana usiogope na mimi nikasema hapana mimi nawapa changamoto kwamba ifika Oktoba, 2005 haya Majimbo saba yaliyoko Mkoa wa Dar es Salaam akinamama mchukue sita, Ukonga tu ndio awepo mwanaume mimi. Itakuwa furaha kubwa sana mimi nikisindikizana na akinamama sita wengine kutoka Majimbo mengine sita ya Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, mimi nawapa changamoto wagombee na wataongeza badala ya asilimia 30 itafika zaidi. Lakini niseme kwamba katika nchi za *SADC* ambazo na sisi kwa kweli ndio tumewekeana Mkataba huo kwamba jamani tufikishe 30%. Kwa kweli kitu ambacho wakuu wetu hawakuangalia ni mtindo gani wa uchaguzi upo katika nchi gani na nadhani ingetakiwa wauangalie. Kwa sababu kama unatumia mtindo wa uwiano kama unavyotumia nchi kama 4 hivi za *SADC,* za Afrika Kusini, Msumbiji, Namibia na Angola ni rahisi sana kufikisha 30% na kwa kweli wamefikisha wale.

Lakini kama unatumia mtindo wa Majimbo, *first past the post* kama tunavyotumia sisi, Botswana, Zimbabwe, Zambia na Malawi ni vigumu kufika asilimia 30% mwaka huu na hawa hawatafikisha wengine Malawi, Zambia, Zimbabwe, Botswana hawatafika mwaka huu. Tanzania tusingefika kama tusingebuni huu mtindo mzuri wa Viti Maalum na ndio maana tunajipongeza, ingawa hao wengine ukiwauliza wanasema huu mtindo wenu sisi hatutaki bwana. Sisi tutafikisha kwa kwenda Majimboni, akinamama wote waende Majimboni wapate 30% lakini ni ngumu sana kutegemea mazingira yaliyopo.

Kwa hiyo, nasema tumefanya vizuri kutafuta mbinu ambayo itatuwezesha kufikisha asilimia hiyo pamoja kuwa na mtindo wa Majimbo.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kusifu hatua hii mimi nadhani kuna haja tuangalie sasa baadaye tunawapataje akinamama na hili limezungumzwa vizuri kutoka kwenye vyama kwamba kuwepo na uwazi zaidi katika hatua ya vyama kuteua hawa akinamama. Mimi niseme kwamba hawa akinamama Wabunge ni wa vyama, sio wa viongozi, wala sio wa umoja wa akinamama wa vyama hivyo. Ni Wabunge wa vyama hivyo, Wabunge wa Tanzania kupitia vyama hivyo na vyama maana yake nini? Ni wanachama wote kwa hiyo, wanachama wote wahusishwe katika kuwapata hawa akinamama. *(Makofi)*

Tunavyo vyama, tunajua ambavyo viongozi tu wanakaa wanateuwa akinamama fulani ambao kwa sababu moja au nyingine wanakuwa na vigezo vyao, wanakuja Bungeni na kuna vyama vingine wanatumia umoja wa akinamama zaidi toka eneo la chini. Chama chetu Tawala ni mojawapo kwamba tunatumia zaidi umoja ule wa akinamama kuanza kuwapata hawa Wabunge akinamama, sasa mimi nasema kutoka hatua za chini kama ni mkutano wa Wilaya au Mkoa basi uwe ni mkutano wa wanachama wote wanaume na wanawake wawachague hao Wabunge akinamama. Lakini hilo nina hakika litawekewa utaratibu.

Mheshimiwa Spika, katika hilo nilitaka niongezee kwamba mtindo ambao umewekwa kuwapata, huu wa uwiano naupongeza sana badala ya kutumia ule mtindo wa idadi ya Wabunge. Kwa sababu sasa unaangalia ni kura ngapi Wabunge wa Majimbo wamepata badala ya Wabunge wangapi wamepatikana na hii itasaidia. Kwa kweli katika lile suala ambalo liliondolewa la kuleta uwiano wa Wabunge limekuja kuzingatiwa kwenye upatikanaji wa Wabunge akinamama kwamba kura za Wabunge kwenye Majimbo zinachukuliwa na hii itawapa changamoto vyama karibu vyote kama inawezekana wasimamishe Wabunge kwenye Majimbo. Kwa sababu kura zozote utakazookoteza zitakuwezesha au zitahesabiwa katika kwenda kumpata Mbunge akinamama. Kwa hiyo, ni changamoto kwamba vyama vyote visimamishe Wabunge kwenye Majimbo angalau waokoteze kura zitakazoweza kuhesabiwa baadaye kuweza kupata angalau mwanamama mmoja hata kama chama ni kidogo kuja hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, lakini ninachotaka kukazia ni 5%. Asilimia 5 kwa maana ya Demokrasia tunayozungumza kwa maana ya kusaidia Demokrasia ikue na vyama vidogo vidogo na vyenyewe viweze kuja Bungeni 5% ni kubwa. Mimi nasema tungepunguza iwe kama 2% au asilimia 3% chama kilichookoteza kikapata kura 2% au 3% kiweze kuleta angalau akinamwama mmoja Bungeni hapa. Nasema hivyo kwa sababu gani 3%? Mimi mwaka huu kwa mfano nadhani watu kama milioni kumi watapiga kura. Sasa 3% ni watu 300,000 hao 2% ni watu 200,000. Kwa hiyo, chama ambacho kimeokoteza kura 200,000 katika nchi au 3 mpe nafasi moja angalau ya akinamama aje Bungeni. Nasema hivyo kwa sababu vile vile hao Wabunge 75 akinamama ukiwagawia kura 10,000,000 kila mmoja atakuja Bungeni kwa kura 133,000 kwa 75 watakaokuja kwa mtindo huu. Sasa kama hawa kwa ujumla wao kila mmoja 75 wanakuja kwa kura 133,333 kama kura 10,000,000 ndio zimepigwa. Kwa nini chama kilichopata 200,000 ambayo ni 2% au

300,000 ambayo ni 3% asipate angalau mmoja. Kwa nini tuanze na 500,000 nadhani kiwango ni kikubwa. Nasisitiza kwamba hilo liangaliwe la asilimia katika kujenga Demokrasia na ili tuwe na vyama vingi ndani ya Bunge badala ya vyama vitano tu kila siku na kumbe tumeandikisha vyama 16, 17.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, ndio tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Katika orodha wamebaki Waheshimiwa Wabunge nane pamoja na wale niliowaita hawakuwepo, lakini watapewa nafasi kipindi cha mchana. Labda niwataje tu Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba na Mheshimiwa Monica Mbega.

Lakini kama miongoni mwao kuna ambao hawataonekana kipindi cha mchana basi hao watakaokuwepo wakimalizika Mheshimiwa Naibu Spika ataahirisha Bunge tu mpaka Jumatatu hawatapata nafasi tena, kwa sababu kanuni zetu zinampa Spika kuweka utaratibu wa uendeshaji bora wa shughuli za Bunge. Kwa hiyo, taratibu nilizoweka ni kwamba tukija Jumatatu kipindi cha maswali kitachukua saa moja tu mpaka saa nne ili kusudi kutoa nafasi ya kuhitimisha shughuli hii vizuri.

Kwa hiyo, kuanzia saa 4 asubuhi watoa hoja wataanza kuhitimisha hoja yao tutakwenda kwenye Kamati ya Bunge Zima na kuna taarifa imeshatolewa kwamba kuna Mbunge mmoja anataka kuleta mabadiliko sasa tunataka kutoa muda wa kutosha ili Bunge liutendee haki Muswada huu muhimu wa Marekebisho ya Katiba. Basi baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 jioni.

*(Saa 06.59 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii mchana huu kuwa wa kwanza ili nami niweze kutoa maoni yangu kuhusu Muswada huu ulio mbele yetu.

Kwanza kabisa, nawatakia kila la kheri ya mwaka mpya wenzangu wote mliopo na wale ambao hawapo ili mwaka huu wa mapambano uwe mzuri kwenu nyote na hatimaye mwisho wa mwaka tukutane tena katika ukumbi huu huu.

**WABUNGE FULANI:** Amen.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka pia kutoa pole hasa kwa mwenzetu Mheshimiwa Frank Mussati ambaye alitutoka na nawapa salamu za rambirambi wenzake pamoja na wananchi wa Kasulu Magharibi kwa kupoteza shujaa mkubwa ambaye alikuwa anawatetea sana katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo, nataka nitoe salamu zangu za pole kwa wote waliopatwa na misiba kwa kufiwa na wazazi, wenzi wao, ndugu na jamaa zao. Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba kwa hatua hii tuliyofikia sasa, mengi yamezungumzwa humu ndani ya Bunge yaliyobaki sisi wengine ni katika kukazia kama kwa msumari ambao haujaingia sawasawa ili kuushindilia kwa nyundo *heavy* ili mambo yawe sawasawa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono Muswada huu hasa lile suala la kuongeza idadi ya akina mama katika Bunge letu na kufikia asilimia 30. Jambo hili ni kubwa na la kihistoria. Mimi mwenyewe binafsi na sisi kwa tabia zetu katika ukoo wetu, katika makabila yetu huko Kusini, tunampa heshima kubwa sana mama na hata katika koo zetu mara kwa mara tunachukua koo zetu kutoka kwa mama. Hii inaonyesha jinsi gani tunavyoamini kwamba hawa wana uwezo wa kutuletea duniani na wana uwezo pia wa kutufanyia mambo mengi. Kwa hiyo, hili ni mojawapo ambalo mimi kwa niaba ya wenzangu wa Kusini tunaliunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ila ningeomba tu kwamba wakati tunaanza mfumo huu na mimi pia kwa bahati nzuri niko katika Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala, hili tulilizungumza kwa nguvu kabisa kwamba hapa sasa tuhakikishe kwamba demokrasia inakwenda mpaka chini.

Mheshimiwa Spika, tuhakikishe katika *regulations* zetu tunaweka utaratibu ambapo hakutakuwa na upendeleo, kutakuwa na haki katika chaguzi hizi. Tukasema kwamba haifai tukaziachia tu Kamati za Vyama zifanye uchaguzi huo. Pale inapowezekana kama ilivyo upande wa UWT katika CCM tuanze na utaratibu ambao utahakikisha wajumbe wanaowachagua hawa akina mama wawe wengi zaidi. Maana yangu ni kwamba isiwe tu Wajumbe wa Halmashauri Kuu ndio wanaowachagua lakini kama inawezekana iwe wajumbe au wanachama wote akina mama waliopo katika Wilaya ile. Wakifanya hivyo itakuwa mtu anachaguliwa kwa uhakika na walio wengi. Sasa demokrasia hii ndiyo itakayotusaidia kupata wagombea akinamama kidemokrasia.

Si kwamba hatuna imani nao, lakini tunaomba wigo ule waweze kuupanua ili hata kijijini kabisa mtu wa mwisho kama ni mwanachama wa Chama fulani naye ahusike katika kumchagua yule mama atakayekuja kumwakilisha hapa Bungeni. Hiyo ikifanyika, kwa kweli itatupa raha kubwa sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hii ni mara ya kwanza tunaanza suala la kura za uwiano. Jambo hili bado halijaeliweka kwa Wabunge wengi hivyo halijaeleweka kwa wananchi wengi. Ni mara ya kwanza tunataka kujaribu kura za uwiano. Kwa hiyo,

naomba Wizara husika na Serikali ifanye kila jitihada ili kuwafahamisha wananchi na hasa wale wahusika maana ya kura za uwiano, mgombea anapatikanaje, haki na wajibu wake unakuwaje na mambo mengine kadhaa wa kadhaa na pia humu Bungeni mambo yatakuwaje kwa sababu mara nyingi tunavyojua Wabunge wanakuja Bungeni baada ya hapo wanarudi katika Majimbo yao.

Sasa wakati ule wanaporudi hawa wa kura za uwiano watahusika namna gani, wanaenda wapi, watafanya nini? Hili ni jambo ambalo linatakiwa lifanyiwe kazi na wananchi waelezwe zaidi ili waweze kuwatumia vizuri hawa wenzetu watakaopata hizo kura za uwiano. Inawezekana kwa baadaye jambo hili litaeleweka na litakuwa jepesi lakini kwa sasa hivi naomba sana Serikali ijaribu sana kuwafundisha watu mbalimbali na katika rika mbalimbali juu ya maana ya kura za uwiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi, Mheshimiwa Bernard Membe jirani yangu hapa alileta mapendekezo kuhusu nyongeza ambayo ingewekwa sehemu fulani, Wanasheria wanaweza kujua namna ya kuweka lakini nia yenyewe ilikuwa kuhakikisha kwamba hapawi na *vacuum* inapotokea kwamba Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu hawapo. Kulikuwa na pendekezo kwamba ni lazima tuwe na ka-*clause* kamoja katakachoonyesha kwamba Jaji Mkuu na Mheshimiwa Spika nao wanaweza pia kufanya kazi hizo za Rais. Nataka rasmi kuunga mkono jambo hili ili liwepo katika Muswada, tuweke mahali kabisa patakapoonyesha endapo watu wote hawa wanne hawatakuwepo basi ni nani atakayekaimu nafasi hiyo ya Rais. Naomba sana hili lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kuzungumzia, hapo mwanzo nimesema kwamba mimi kwa bahati nzuri nilikuwa katika Kamati hii ya Kudumu ya Sheria, Katiba na Utawala. Mimi toka niwe katika Kamati hii sijawahi kuona jitihada kubwa iliyofanywa ili kufikisha suala hili kwa wananchi. Jitihada kubwa sana sana imefanyika. Kamati hii ilipangiwa kwenda sehemu mbalimbali kwa mfano imekwenda Arusha, Mwanza, Tabora, Zanzibar, Mbeya pamoja na Dar es Salaam kutafuta maoni ya wananchi ili kuboresha Muswada huu. Kusema kweli tumepata bahati ya kuwa na utajiri wa maoni mengi sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi karibuni nimeona baadhi ya viongozi wa upinzani katika vyombo vya habari wakibeza kwamba mpaka hivi sasa suala hili halifahamiki sawasawa kwa wananchi na kwamba watafanya maandamano ili wananchi waonyeshe kutoridhishwa kwao na mabadiliko haya ya Kumi na Nne. Nataka kusema kwamba huu ni upotoshaji mkubwa wa mambo kwa sababu Kamati hii katika kuzunguka sehemu hizi zote imekutana na watu wa kila aina na katika Kamati yenyewe wapo wajumbe Wabunge wa vyama hivyo mbalimbali wa CHADEMA, *CUF, TLP* sasa kama wangekuwa na maoni yoyote si wangetoa katika Kamati na mikutano hii? Leo kwa nini watu hawa wanakuja kuitisha vyombo vya habari na hata kudiriki kutoa maneno ya kashfa na matusi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kweli nilichukia sana wakati kiongozi fulani anamwita Rais wetu kwamba mtu huyu nisiyemfahamu, anayeitwa kwa jina fulani fulani,

kama vile ni ndugu yake au mtoto mwenzake. Jambo hili ni lazima Watanzania tulipinge kabisa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Wasanii wamekuwa na maendeleo makubwa katika fani yao. Kuna msanii mmoja sijui jina lake sawa lakini anaitwa Kingwendu na huyo Kingwendu ana msemo mmoja ambao unaitikia 'mapepe'. Hata kwenye mpira siku hizi likifungwa goli watu wanashangilia 'ooh mapepe, mapepe, mapepe'.

Sasa mimi nasema hayo maandamano hayana maana na ni ya kufurahisha tu kama mapepe. Kwa hiyo, maandamano hayo yakiwepo, wayaone kuwa ni mapepe.! Kwa hiyo, mimi naona kwamba kuandamana huku ni furaha tu ya watu, ni mapepe tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba Watanzania tunapopata nafasi ya kuleta hoja zetu tuzilete kupitia Wabunge wetu, kupitia kwenye mikutano yetu hii inayohusu Katiba hii halafu baada ya hapo ndio tuje na mpango maalum ambao Watanzania wote tunaweza kuupitisha. Huu ni utekelezaji awamu kwa awamu wa mapendekezo ya Tume ya Jaji Kisanga.

Kwa hiyo hata masuala mengine haya ya mgombea binafsi na nini yatakuja kwa wakati wake unaofaa lakini kwa sasa hivi kulazimisha kila kitu kiwe sasa hivi, aah, aah hayo ni mapepe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo tuyangoje hayo mapepe, wananchi waelewe kwamba ni mapepe na mimi nataka kusema kwamba naunga hoja hii mkono mia kwa mia na naamini kabisa tukiitekeleza vizuri basi itakuwa moja kwa moja ni njia mojawapo ya kuhakikisha kwamba vipengele mbalimbali katika Katiba yetu vinarekebishwa na tunaondoa matatizo ya wananchi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nitoe rambirambi zangu kwa jamii ya Mheshimiwa Mussati na wapiga kura wa Jimbo la Kasulu Mashariki kwa kuondokewa na kiongozi wao, kiongozi wetu na kiongozi wa Taifa kwa muda ambao ulikuwa hautegemewi. Naomba roho ya marehemu iwekwe mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba moja kwa moja niunge mkono hoja hii na nasema kabisa imeandaliwa vizuri lakini kama ilivyo kawaida kwamba Bunge ni mshauri wa utungaji wa sheria na bado ikawa ni chombo cha kutunga sheria, sina budi na mimi nigusie sehemu mbalimbali katika kuboresha maeneo mbalimbali ili kuufanya Muswada huu au kuifanya Katiba yetu iweze kuwatumikia wananchi wa Tanzania vema zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na kusema kwamba kwa ufahamu wako na ufahamu wa nyumba kumekuwa na malalamiko mengi sana na kwa muda mrefu

sana kuhusu mambo mengi ambayo hayaendi vizuri katika Muungano wa Jamhuri ya Tanzania. Wenzetu kutoka Visiwani mara kwa mara wanalalamika na hata majibu yaliyokuwa yanatoka hapa asubuhi ya leo kutoka kwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kweli hayakuwa yanapendeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, muungano huu ni sawasawa na ndoa kati ya mke na mume. Ndoa ya namna hiyo ni kwamba ni mkataba unaopaswa kuheshimika na ili uheshimike wakati wote kunapaswa kuwa na meza ya kukaa chini na kuzungumzia mambo yanayohusu ndoa hiyo leo Muungano huo. Haiwezekani kwa miaka yote hii tukakubali kukaa na manung'uniko ya mara kwa mara, mara kwa mara tukafanya mabadiliko katika Katiba ya nchi lakini tukashindwa kufikia mwisho au angalau kuyapunguza manung'uniko haya kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ilione hili ili kupunguza kutoa mwanya kwa maadui wa ndani na nje kuendelea kutusuta, kutushtumu na kuendelea kuleta chokochoko kati ya nchi hizi mbili. Wapinzani katika nyumba na nje ya nyumba hii mara kwa mara wanatumia mwanya huu kwa kusema kwamba Serikali ya Muungano ni dhaifu, haijali, haisikii, maneno kama haya hayapendezi mwananchi baada ya kuwa na uzoefu wa miaka karibu 44 ya uhuru wetu. Naomba kabisa suala hili lishughulikiwe na lionekane lina umuhimu wake wa pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo ambalo linaendelea kukua siku kwa siku kuhusu ulinzi na usalama wa Taifa la Tanzania. Huu ni ujambazi ambao mkazi wa Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya anauona na anaishi kwa mashaka ya maisha yake mwenyewe na mali zake. Ipo sheria, nina hakika Waziri mwenye dhamana anaifahamu ambayo inakusanya vipengele vitatu muhimu. Kipengele cha uhujumu wa uchumi, mauaji na uhaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ikubali kwamba kulingana na hali ya ujambazi ilivyo katika nchi hii ambapo watu wanauwawa, mali zinaharibiwa, watu wanatekwa, gharama kubwa sana inatumika katika kuwafutilia majambazi basi kiongezeke kipengele cha nne kuhusu majambazi sugu wanapopatikana na wengi wanajulikana kwa sababu kumbukumbu zao zipo katika vituo vya Polisi, Mahakama zote nchini, wasipewe dhamana kama hivyo vipengele vitatu vya kwanza vinavyoelekeza.

Watu hawa ni wahujumu, wauaji, wahaini wanaiweka nchi katika hali mbaya inakosa utulivu, inakosa amani, muda wa kufanya kazi za maendeleo unakosekana kwa sababu ya watu wachache ambao wanaichezea sheria na Serikali bila kujali.

Sasa umefika wakati tuitazame kama ni huruma basi imekuwepo huruma ya kutosha. Tulifikiri kwa kuendelea kuwa na uhuru wetu watu wa aina hiyo wangejifunza kuwa na aibu, wastaarabu na heshima lakini badala yake inaonekana wimbi hili linaendelea kukua, unamkuta mharibifu aliyeko Dar es Salaam ana rafiki yake wako Mwanza, Kigoma, Namanga sasa nchi inatengeta. Naomba kabisa Serikali ilione hili na wala isilifumbie macho kama ni kutaka tutunze heshima na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la wakimbizi katika Tanzania. Ninafahamu kabisa kwamba hili ni suala la Kimataifa. Yako maazimio mengi katika Jumuiya ya Kimataifa kuhusu Wakimbizi. Lakini naomba wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho aliambie Bunge kwa miaka hususani 11 sasa nchi hii imetumia gharama kiasi gani kuwahudumia Wakimbizi? Upo wakati miaka kama ya 1996 na 1997 nchi hii ilikuwa na Wakimbizi zaidi ya milioni moja.

Nchi maskini, nchi ambayo wananchi wake wanaishi katika umaskini uliokithiri, hawana elimu, hawana chakula cha kutosha, hawana madawa hospitalini, hawana njia nzuri za mawasiliano lakini inajitwika mizigo mikubwa ya namna hiyo kutoka Mataifa mbalimbali ndani na nje ya Bara la Afrika. Mzigo kama huu ni kwa sababu Tanzania ni kisiwa cha amani watu wote wanakimbia kuja Tanzania. Hali ya wananchi wa Tanzania imekuwa mbaya zaidi kwa sababu ya mengi lakini hili la Wakimbizi likiwemo. Naomba iwezekane kabisa nchi yetu kwa heshima yake, uwezo wake na kuaminika kwake basi kuweko na Kifungu kuhusu Wakimbizi katika Katiba ya nchi ya Tanzania, tumeteseka kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Ngara wanaponisikia nikizungumza wanashukuru Serikali kwamba Wakimbizi wamepungua sana katika Wilaya ile na wanarudi kwao Rwanda na Burundi lakini bado kuna matatizo makubwa na makovu ambayo yameachwa na yataendelea kuwepo kwa muda mrefu. Hiyo ni sawa na ilivyo kwa Kigoma, Rukwa, Mwanza, Tanga hatuwezi kuendelea kufanya kitu kama hiki kama Jumuiya ya Mataifa inaona umuhimu wa kutusaidia.

Kila inapojitokeza suala la Wakimbizi basi Jumuiya ya Kimataifa iwawekee kambi katika nchi zao au ikionekana kwamba nchi zao zimevurugika kiasi kikubwa haiwezekani basi Mataifa mbalimbali duniani wagawane ili kila mmoja achukue nafasi ya kusaidia badala ya kuchukua mzigo mzito wa namna hii ikaurundika juu ya nchi moja na hasa nchi moja maskini kwa sababu tu ni nchi inayoheshimu haki za binadamu, inayoamini kuwa binadamu wote ni sawa basi inakuwa watu kuteseka lakini inapofika tuombe misaada katika Jumuiya inakuja kwa kususua na wakati mwingine haiji. Naomba Katiba ya nchi ifikirie kuweka suala hili la wakimbizi katika mlolongo wa mambo muhimu ambayo nchi yetu inapaswa kujilinda nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhuru wa kuabudu. Mimi nakubali kabisa kwamba Taifa letu halina dini na Serikali yetu yetu haina dini lakini mtu mmoja mmoja ana dini. Kuachia tu hivi hivi bila sheria ya kulinda na kusimamia dini nafikiri ni sehemu nyingine ya hatari. Tumeshuhudia katika nchi hii ziko dini zimefufuka au zilikuwa zimekufa au zinaishi ambazo zinakataza watoto wasiende shule, wagonjwa wasiende hospitali, watu wasifanye kazi, wasisalimiane, mambo ya namna hii ni uvunjaji wa sheria.

Ukishakuwa na dini zinazofanana hivi zikatambaa katika Mikoa yote 26, nina hakika kwamba badala ya nchi hii kuendelea itarudi nyuma. Badala ya nchi hii kuwa na amani vita ya wenyewe kwa wenyewe inaweza kuzuka. Sitaki kulizungumzia sana kwa sababu waliotangulia wamelizungumzia sana.

Nafikiri ni wajibu sasa wa Serikali kuona kwamba kama kuna sababu ya kuwa na vipengele vya kulinda na kusimamia dini ambazo zinazuka na kuwa na taratibu zilizo kinyume na sheria kuu ya nchi na sheria nyingine zinazofuata basi kipengele fulani kiongezwe katika Katiba ya nchi kwamba mipaka ya dini na viongozi wa dini na hata waumini inafanana hivi na vile amani itakuwepo, kuabudu kutakuwa katika hali ya usalama na kunakoeleweka badala ya kusema basi tu kwa kuwa kila mtu anaweza kuabudu kwa sababu ana uhuru wa kuabudu basi afanye anavyotaka, kupitia nyumba za watu wanapomoa, kutukana viongozi Misikitini, Makanisani, huu sio uhuru wa kuabudu ni uhuru wa kufanya fujo, ni uhuru ambao ni hatari kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi napenda nimshukuru au niishukuru Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kuzuia maandamano yaliyokuwa yanategemewa kuwa kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sijui kwa kweli kuna nini kinachotaka kutokea katika hali kama hiyo. Tunaazimisha miaka 28 ya Chama cha Mapinduzi, Chama ambacho ni mkombozi wa nchi hii, Chama ambacho kimetupa sifa Taifa hili katika ulimwengu mzima leo watu ambao pengine hata hawajui Chama kilichotangulia kama vile *TANU* kilivyoanza na wengine vijana tu watu wabichi ambao wameelimishwa na Chama kama hicho basi wanaota mapembe, wanavimba mashavu, inabakia ni kuchezea nchi hivi hivi. Hivi kweli wanaandamana kwamba wananchi hawajui kinachofanyika leo ili wafike wapi na wafanyeje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba hali hii sio ya kawaida, wenzetu hawazuiwi kuwa Wapinzani lakini pia wajue kwamba wanayoyafanya sio kwa sababu ya wananchi peke yao ambao wanasema kwamba hawajui kitu kwanza ni dharau na wanawatukana wananchi ambao wamewaweka madarakani na bado wale wale ambao wanawategemea watawapa kura wanawafanya wawaone kwamba hawafai kitu.

Sasa sijui wanategemea kupataje uongozi au hata kutaka kwenda Ikulu watakwendaje kama wanaowategemea kuwapeleka wanaonekana kwamba ni wa kudharauliwa?

Lakini siyo hilo tu wanapofanya vurugu ya namna hii ni kwamba maafa yanayojitokeza nayo pia yanawaguza, nimeshuhudia hilo mwaka wa 2001 kwamba walioanza kukimbia walikuwa ni wao hawa hawa waliokuwa wameleta vurugu za namna hiyo na kuumbua mauaji. Sasa nafikiri wajifunze kuwa watulivu na watumie njia ambazo ni za kistaarabu, watumie njia za kisheria ili kuweza kufikisha malalamiko au angalau hoja zao Serikalini na katika meza na majukwaa ya siasa vinginevyo wanatuweka mahali pabaya na baadaye watalaumiwa zaidi kwa matendo yao ambayo hayana mahesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba tena kwa mara ya pili kuunga mkono hoja hii iliyaoko mbele yetu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hoja hii ya leo.

Awali ya yote niungane na wenzangu kuwapa pole wananchi wa Kasulu Mashariki kwa msiba wa Ndugu yetu Marehemu Frank Mussati na kwa familia yake kwa ujumla. Sisi Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa kweli imekuwa pigo kubwa kwetu, Kamati ya Miundombinu kwa kipindi hiki inakuwa imepoteza Wabunge wawili, Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika mwaka huu mpya wa 2005 niwatakie Waheshimiwa Wabunge wenzangu heri na fanaka ya mwaka mpya na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ametujalia tumeuona na tumeanza Bunge hili la mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo naomba niungane na wenzangu kwa kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, lakini naomba kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa sababu Serikali ya CCM ni sikivu inaelewa nini inachofanya kwa hiyo imeandaa Muswada makini, mimi nawahimiza Watanzania wote wanaosikiliza Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Naibu Spika waelewe kwamba wawakilishi wao ambao ni Wabunge ndiyo waliopewa wajibu kwa niaba yao ya kuchambua Muswada huu na kuutolea mapendekezo na Serikali sikivu ya CCM imeshasikiliza mambo mengi mfano mmoja mzuri ni kule kufuta kwa Baraza la Ushauri wa Rais.

Mimi naamini Serikali imefuta siyo kwamba imasimamisha kwa kusikiliza maelezo ya Waheshimiwa Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi, kwa hiyo wale wanaopiga kelele nje ya Bunge kwamba marekebisho haya si sahihi na wanataka *forum* nyingine ambayo sijui kwa kutumia sheria gani au Katiba ya nchi gani, kwa sheria na taratibu za nchi hii Bunge ndiyo linalojadili baada ya kusikiliza maoni ya wananchi na kwa kweli tunaipongeza Bunge kwa kuiandalia Kamati hii ya Katiba na Sheria kuzunguka mikoani na kukusanya maoni. Kwa sababu Muswada ulitolewa mapema wadau walikuwa na nafasi ya kutoa maoni yao, sasa Roma haikujengwa kwa siku moja na ndivyo hata sisi tunaendelea kuijenga nchi yetu kwa utaratibu. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali ya CCM na tuendelee na msimamo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali vilevile kwa kuongeza nafasi za wanawake, kufikia asilimia 30 katika viti maalum, kama walivyoeleza wenzangu waliotangulia, kwa kweli, imefikia wakati sasa wanawake wapate uwakilishi zaidi katika chombo hiki cha kutunga sheria kwa sababu kwa Sensa ya 2002 wanawake ni zaidi ya asilimia 52 wa Watanzania lakini wawakilishi waliopo ndani ya Bunge lako Tukufu ni asilimia 22 tu ambayo si sahihi. Kwa hiyo, hivi tutakapopata asilimia 30 tunashukuru kwamba angalau ule mkataba walioridhia wa Beijing na *SADC* utakuwa umetekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza vile vile walivyopendekeza kwamba Wabunge wanaotoka Baraza la Wawakilishi wanaokuja katika Bunge lako Tukufu basi angalau wawili kati ya wale watano basi wawe wanawake na wale wa kuteuliwa basi wawe nusu kwa nusu. Mimi naunga mkono kabisa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wengine wanasema tumwachie uamuzi rais, lakini kuna ubaya gani kuweka bayana ndani ya Katiba? Kwamba katika kumi watano wawe wanaume na watano wawe wanawake ili akiamua kwa sababu inasema si zaidi ya kumi akiamua kuteua sita basi watatu wanawake na watatu wanaume. Akiamua kuteua wanane basi wanne wanaume na wanne wanawake, akiamua kuteua saba basi wanne wanawake na watatu wanaume. *(Makofi)*

Mhehimiwa Naibu Spika, mimi nina hakika pendekezo hili limekuja kwa sababu Serikali imetambua mchango muhimu wa wanawake katika Tanzania, sina haja ya kuorodhesha mchango wao lakini mchango wao unafahamika ni muhimu sana na kama nilivyosema awali wako zaidi ya asilimia 52, kwa hiyo, ni vema vitu hivi vikaandikwa kikatiba ili wakati wowote historia iweze kurejea na kuona kwamba maamuzi ya busara yalifanyika katika Bunge lako Tukufu lilipoketi Dodoma kipindi cha Februari mwaka 2005.

Kwa hiyo, wanawake Watanzania watafahamu kwamba wao wamethaminiwa kwa kuongezewa nafasi za asilimia 30 za wale wanaotoka kwenye Baraza la Wawakilishi na zile za kuteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kukupongeza kwa nafasi hizo nilikuwa naomba basi aidha ni Katiba au kanuni iweke wazi wajibu na utaratibu wa kazi wa Wabunge hawa wa viti maalum. Wabunge wa viti maalum kuna kwao walikozaliwa, wanakoishi na wanapokuwa Bungeni ni Wabunge na wakirudi makwao ni Wabunge sasa isije ikafika mtu anakwenda nyumbani kwake ambako ni Jimbo la Mheshimiwa Akukweti halatu Akukweti akasema kwa nini Watondoha amekuja. Sasa mimi nimuulize aende wapi? Hivi inawezekana mimi kwetu Tunduru niende likizo Monduli? Inawezekana mimi kwetu Mbeya halafu niende likizo Tarime? Lazima mtu uende kwako ulikozaliwa *(Makofi)*

Mimi ninachoomba ni kwamba Wabunge wa viti maalum wawekewe utaratibu wao wa kazi na bahati mbaya ukifika kule una mjomba, una shangazi, una binamu, una ndugu na hata marafiki na una mashabiki wanaokupenda. Maana kwa mujibu wa utaratibu wa chama changu Mbunge wa viti maalum anapitia kwenye chujio, unapigiwa kura na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa wa UWT ambao wametoka katika kila kata. Sasa na mimi ninakoishi kuna kata.

Hao mashabiki wakija kukuomba msaada Mbunge wa viti maalum kuna kosa? Huna haki ya kuwasaidia? Kwa hiyo mimi naomba sana hii iwekwe wazi na sasa tunaongeza viti vya uwiano na hawa Wabunge wa viti vya uwiano nao wana mahali wapoishi na wenyewe watataka wawasaidie wananchi sasa isije ikawa Wabunge hawa wa viti maalum na Wabunge wa uwiano ni Wabunge wa Bungeni tu, wakitoka nje ya Bunge hawana shughuli za Bunge, itakuwa ni kichekesho kwa sababu wanalipwa mishahara ya walipa yaani ya fedha za walipa kodi wa Tanzania. Kwa hiyo wana haki ya kuwatumikia kokote wanapokuwa. Kwa hiyo, naomba sana pamoja na marekebisho haya suala la

wajibu na nafasi ya Wabunge wa viti maalum na Wabunge wa uwiano nje ya Bunge liwekwe wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ningependa kugusia ni suala la kukaimu urais, kweli katika Dola letu tuna *Executive,* Bunge na Judiciary, hawa wote wana uwiano lakini kila mmoja ana kazi yake.

Mimi naamini pendekezo lilikokuja kwamba Waziri Mkuu akaimu nafasi ya urais wakati Rais ambapokuwa hayupo na Makamu wa Rais hayupo ni kwa sababu yeye anafahamu majukumu ya utendaji katika mikoa, majukumu ya utendaji katika maeneo mbalimbali ya nchi lakini nilikuwa naomba tujiulize tu, hivi nafasi ya Waziri Mkuu kutambuliwa kama Rais kwa upande wa Tanzania Visiwani unakuwaje? Maana yake huyu ni Waziri Mkuu wa Serikali ya Muungano na shughuli zake kubwa anafanyia Tanzania Bara, Je, haitaleta mgogoro wa kikatiba wanapotakiwa Watanzania visiwani wamtambue huyu kama Mkuu wa nchi? Kama haileti mgogoro mimi hilo ninaliafiki kabisa.

Ninauliza hivyo kwa sababu pamoja na kwamba yeye ni mkuu wa shughuli za Bunge lakini ni Bunge lile lililopo hapa na Spika alikuwa hivyo hivyo na Jaji Mkuu alikuwa na nafasi hiyo maana Jaji Mkuu anakaa Tanzania Bara, sijui kama ana uhusiano na kule Visiwani isipokuwa kwenye Mahakama ya Rufaa. Kwa hili suala naomba tuliangalie vizuri kwa sababu Muungano wetu ni muhimu sana tusije tukaongeza mianya ya malalamiko yasiyo na msingi.

Lakini kwa ujumla, kwa kweli ni vema Waziri Mkuu akasimama kwa sababu *at least* ana uzoefu wa shughuli na anakuwa karibu na Rais na Makamu katika shughuli zao za kila siku. Kama haileti Mgogoro wa kikatiba kati ya Bara na Visiwani mimi sina tatizo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ningependa kugusia suala la uhuru wa kuabudu. Naungana kabisa na mabadiliko yale ya Ibara ya 19 (2) kwamba nchi haina dini na imeelezewa vizuri pale lakini sielewi kwa nini kifungu kile kidogo cha tatu kimeondolewa sasa.

Uhuru wa dini ni muhimu lakini dini vilevile inaweza kuleta uchochezi, watu wakafarakana, wakauana, wakazozana vibaya sana na uhuru wowote ni lazima uwe na mipaka yaani mtu anakuwa na haki na uhuru lakini anao wajibu vilevile kwa Taifa lake na kwa wananchi wenzake anaoishi nao jirani. Kwa mimi suala hili naomba sana waliangalie upya kwa nini wameondoa kifungu hiki ambacho kwa kweli kilikuwa kinasaidia sana kudhibiti maeneo ambayo tumeona mizozo sehemu nyingi.

Mkristo anasimama anahubiri Injili lakini badala ya kuhubiri Injili anakashfu Msahafu. Vile vile Mwislamu badala ya kuhubiri juu ya Msahafu anakashfu Injili ambao hawa wote kwa kweli maana ya dini ni kumtafuta Mwenyezi Mungu isipokuwa kila mtu ana njia yake ya kumfikia Mwenyezi Mungu.

Sasa kama kila mtu ana njia yake ya kumfikia Mwenyezi Mungu basi awe na uhuru wa kuabudu vile anavyotakiwa lakini awekew mipaka ambayo inamwajibisha kwa Taifa, kwa mwananchi mwenzake ili tuweze kuendelea na amani na utulivu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ningependa kugusia suala la *DPP* kumtia kwenye Katiba, tusipeani umaarufu. Katiba ni Sheria Mama na hii tukiiandika kwa kujifikiria kwamba naiandika kwa kumlinda Watondoha haitusaidii, Katiba ni Sheria Mama kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo, mimi ninaomba sana tuyaweke mambo muhimu kwa ajili ya maslahi ya Taifa kwa ajili maendeleo ya nchi yetu, kwa ajili ya usalama na amani ya nchi yetu. Tusiweke mambo ambayo kwa kweli baadaye yanaweza kutusuta tukarudi tena kurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu la haula haitangulii unasema amah! unaposema amah! basi umeshadondoka chini mambo yameharibika lakini unapojiinua tu basi mambo yako mabaya. Basi tusifikie hapo, tuitengeneze Katiba kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu, kujenga Taifa letu, kujenga umoja wa nchi yetu ili tuendeleze hii amani ambayo tunayo, ni lulu ambayo majirani zetu wanaililia.

Ndugu yangu Mheshimiwa Sebabili hapa amezungumzia juu ya wakimbizi, kwa kweli wale wangepata lulu hii ambayo sisi tunayo wangeweza kuikimbilia lakini Mungu amewatupa mkono lakini sisi tunayo, sasa tusiichezee tukaiharibu, Naomba tuitengeneze Katikaba kwa lengo la kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo naunga mkono hoja nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu muhimu na kwanza kabisa napenda niseme ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, yapo mambo machache ambayo nitayasema, la kwanza ni kubadilisha Katiba ni kitu muhimu sana katika Taifa, kwa kuangalia tulivyojadili mabadiliko haya sikuliona vuguvugu lililobeba nchi nzima kama tulipokuwa tunabadilisha Katiba katika nadhani mabadiliko ya 12, kulikuwa na vuguvugu zaidi la kila mtu kuhusika katika kulijadili. Kwa hiyo nafikiria kwamba wakati mwingine ni vema kujipa nafasi na kuwapa wananchi nafasi hiyo.

Pamoja na magazeti tuliyonayo *Television* na *Radio* vuguvugu hili lingekuwepo kubwa zaidi kuliko kuishia miongoni mwa wachache au wanaoongoza vyama au sisi kama Waheshimiwa Wabunge ambao tunapata nafasi ya kulizungumza. Najua wazi Tume imepita lakini Tume ni Tume na mjadala wa wazi ni mzuri zaidi na ndiyo maana utaratibu katika sehemu nyingine unakuta kuna kitu kama *White Paper* inazunguka. Watu katika vikundi mbalimbali wapate nafasi ya kucharuka tu na kutoa pumzi. Kwa hiyo hilo ni moja ningependa niseme pamoja na kazi nzuri iliyofanywa lakini ni vema kama tungekuwa na vuguvugu zaidi.

La pili, nafikiria kwamba wakati tunabadilisha badiliko hili kwa sababu si vyema tukawa tunabadilisha tungekuwa tumeangalia na mambo muhimu ya dunia inavyokwenda leo. Ukiangalia Katiba tuliyoibadilisha, kuna mahali hata neno maslahi ya umma limebadilishwa na ni sahihi kwa sababu wakati Katiba inatungwa, tulikuwa katika mazingira ya kuangalia maslahi ya Umma badala ya mtu mmoja mmoja ilikuwa ndio wakati wake ule. Sasa tumetoka hapo kwa hiyo na maneno yanabadilika na mimi ningependa kusema kwamba kwa wakati sasa ambapo nayo dunia inabadilika kwa kasi kubwa tungekuwepo nakutazama Katiba katika kuitengeneza hasa kuangalia haki za binadamu katika mtazamo huo wa kwamba je tunakwenda na wakati je, tunaenda na msukumo wa maendeleo yanayokuja je, tunaweka nafasi ya Mtanzania katika maendeleo haya na kwa hapo ningependa kutoa mfano mmoja kwamba hali tuliyonayo sasa Tanzania tumekuwa na wageni wengi sana ambao nao wanapata haki sawa kama sisi kama siyo zaidi. Hili suala ni la Kikatiba tumefika mahali unakuta asiye Mtanzania anamiliki mali ya Tanzania kuliko Mtanzania mwenyewe. *(Makofi)*

Hili ni lazima lisemwe ndani ya Katiba ninapoambiwa mimi ni Mtanzania, na ninalindwa na Katiba lazima Katiba hii iweze kuainisha kwamba huyu siyo Mtanzania na hiyo itatokea tu kama nitaona haki ninazozipata mimi na haki anazozipata mtu mwingine ama fursa anazozipata mtu mwingine ambayo siyo Mtanzania inakuwa vigumu kwake. Tukiangalia mashamba kuna watu hapa wanamiliki ardhi ambao siyo Watanzania na Watanzania wengine hata robo heka hana. Tukiangalia hapa wa nguvu zaidi ndani ya madini yetu kuliko Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Sasa Katiba isipoweza kulinda haki zangu, nikatembea ndani ya nchi ya Tanzania nikasema mimi ni Mtanzania kwa hiyo nina haki zaidi. Mimi ni mtoto wa ndoa siyo mtoto wa haramu. Kwa hiyo inafika mahali mtoto haramu na mtoto wa ndoa ikishakuwa ni sawasawa ndoa haina maana. Kwa nini nijifunge katika ndoa kama naweza kuzaa ninavyotaka na haki zikawa sawasawa. Kwa hiyo tukitaka kulinda Utanzania na Uzalendo ni lazima Katiba iangalie uraia na katika Uraia kuna jambo lingine ambalo pia nitalisema leo akizaliwa mtoto na mimi suala la baba linaulizwa. Lakini akizaa Mheshimiwa Makwetta suala la uraia wa mama haliulizwi, huo ni ubaguzi. Katiba yetu hiyo haikuitengua ya kwamba mtoto ambaye mimi nimembeba miezi tisa na ushahidi upo anaulizwa zaidi kama ni Mtanzania kuliko baba ambaye wakati mwingine amesakiziwa kwa sababu ana cheo. Naona mtani wangu kule anageuka geuka kaa vizuri na kipara chako. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa nataka niendelee kwa kusema kwamba haya ndio mambo ambayo ni ya kwenda na wakati katika wakati huu mgumu ambapo Mtanzania anapaswa kufahamika na haki zake zikalindwa kikatiba ni lazima katiba iwe wazi. Lakini tuna matumaini ya kwamba labda hilo litatizamwa baadaye lakini ni suala la msingi kwa sababu ni kutokea katika msingi wa kuwa Mtanzania ndipo ninapoheshimu Katiba hii. Mtu mwingine ambaye siyo Mtanzania hapaswi kuiheshimu hii Katiba wala haimuhusu. Kwa hiyo, hilo moja ambalo ningependa pia niliseme kwa ufupi.

Suala lingine ambalo nataka kwanza nipongeze lililoletwa ni juu ya Majaji na namna ya kuwatafuta Majaji. Hapo ni hatua ya mbele tunaanza kuona ya kwamba nafasi

fulani fulani si suala la kujaza nafasi ni suala la kutafuta watu makini ambao wataweza kukaa katika nafasi hizo ili kuwahudumia Watanzania na mimi ningependa hili liendelee katika ngazi zote. Tusipofanya hivyo, tumeyaona katika *Local Government* ya kwamba tumezoana zoana tukapatikana u-*DED* tukapatikana kila kitu sasa hivi Wilaya kule zina-*collapse*. *(Makofi)*

Afisa Mipango sio Afisa Kilimo, kwa hiyo tunakuwa na *concept* ya kujaza nafasi na siyo kutafuta mtua ambaye anakaa kwenye nafasi hiyo. Kwa mfano katika nafasi za kutoa haki ambazo ni nyeti na tunaendelea sasa tunafika hapo napongeza hii ni hatua ya kwenda huko mbele ya kwamba tutafute watu wenye makini ndio maana tumeingia kwenye *corruption.* Mtu ambaye hana shida ya kupoteza heshima na sifa zake atakuwa *corrupt* Atakuwa amekwenda kule hana cha kupoteza. Wazungu wanasema; *he has no face to loose.* Kwa hiyo, hata akinywa gongo au kuhongwa hana kingine anachokipoteza kwa sababu hana hiyo sifa ya kuwa pale. Kwa hiyo, mijadala mingine imezungumza juu ya Mawaziri wasiwe Wabunge au Mawaziri wawe Wabunge mimi sina tatizo. Tatizo langu ni *quality* ya kwamba tufike mahali Mawaziri wanaletwa hapa awe ameteuliwa ni Mbunge awe si Mbunge. kwa sababu sisi tunabariki na kumpa support kwa kazi ambayo inaifanyia nchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, akiwa ni Mbunge mwenzetu wameona anatosha pale aje hapa tumbariki akiwa siyo Mbunge akateuliwa akiwa Waziri tumbariki tuwe na uhakika. itatuondolea majungu na kusemana ndani ya magazeti kwa sababu kuna kitu kinaitwa unapofikia hatua fulani ya cheo lazima uwe *above scissors wise* usiwezi kusemwa hayo yanayoweza kusemwa kwa mtu mwingine yeyote. Mimi hapa Mama Mongela mke wa Mongela nikianza kusemwa nimekutwa niko kwenye danguro mimi natoa mfano tu imeshaniteremsha kiasi ambacho hata nyasi wanazoshika nimezidhalilisha. Kwa hiyo, lazima nijitahidi nisionekane karibu na mlango wa danguro, lazima nijitahidi nisionekane karibu na mlango wa danguro usiseme ya kwamba nilikuwa napita tu unaenda wapi. Ndivyo tunataka viongozi wa aina hiyo ya kwamba hatupati taabu ya kumtetea mtu kwa sababu amepita karibu na danguro ama amekaa kwenye *bar* mpaka saa tisa usiku anasema nilikuwa nawasindikiza Waheshimiwa Wabunge wenzangu ama wapiga kura wangu. Mara moja sawa lakini mara mbili! tufike mahali tuna viongozi hawasemwi machafu lakini wakishakuwa ni wa kusemwa machafu tunapata taabu kuwatetea na tunaharibu Chama cha Mapinduzi, *So you must be above scissors wise* usipite karibu na danguro usikae kusindikiza wapiga kura mnakunywa nao mpaka majogoo yanawika eti niko na wapiga kura hiyo ni mifano midogo tu naitoa lakini nadhani mnanielewa. *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Sana. Waambie hao.

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Kabla muda haujaisha nataka niseme tunakokwenda, Katiba yetu lazima ifike mahali unaposema huyu ana nafasi hii anafanana kwa vyovyote na kwa jitihada akiwa na kasoro, ni kasoro za kibinadamu lakini sio za kujitakia. Huyo hatufai na hasa sisi wana CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka niliseme ni la akinamama. Waheshimiwa Wabunge kati ya jambo hasa kipindi hiki mnapaswa kuliunga mkono bila hata kuguna ni la asilimia zaidi ya thelathini ya wanawake. Wamewabeba, wamewapigia kura, wamewapigia vigelegele, hivi cha mno cha kutishika tunaposema yawekwe ndani ya Katiba! Akinamama huko mlipo mnasikia. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Wanasikia.

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu sisi tumewabebeni, tumewapa vyeo vyote walivyotaka. Kinachosemwa hapa na dunia na wala sio Tanzania na dunia ni kwamba wakati umefika tushirikiane bega kwa bega katika kufanya maamuzi, tuweze kusonga mbele zaidi. Kwa Tanzania hili tunapaswa kulielewa vizuri zaidi kwa sababu akinamama hawa ndio wamebeba uchumi wa nchi hii. Kwa hiyo, kupata wachache miongoni mwao wakaongezeka kuja hapa na wao wakajisikia kuona sura za wenzao ziko hapa lisiwe ni suala la kupata kigugumizi. Ni suala la kushangilia, tulikubaliana Beijing na Tanzania ilikuwepo na aliyeendesha alikuwa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeendelea na mkakati huo, tumeridhia Mikataba mbalimbali ikiwemo *CEDAW* ambayo ni *Convention on Elimination of All Forms of Discrimination Against Women.* Hata hiyo *percent* tunayoisema ni katika kusema ya kwamba twende hatua kwa hatua, usimpe mtoto kande kabla hajaota meno. Kwa hiyo, kwa sababu mila zetu na desturi zilikuwa ndio hivyo tunapaswa twende hatua kwa hatua tukifikia *percent* ishirini na tano tumefika *percent* thelathini tukizidi *percent* thelathini tutafika mahali *issue* sio mwanamke au mwanaume, suala litakuwa uwezo wa mtu basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama litapata wanawake wengi wenye uwezo na wakashindana wakapata wataingia Bungeni, lakini sasa kama mkakati ni lazima tukubali kama sisi tunakubali demokrasia haiwezi mtu kukwambia nakubali demokrasia ndio tuliyopambana *South Africa* kwamba huwezi kunibagua kwa sababu mimi ni mweusi. Ndio kinachosemwa kwamba mila na desturi zimembagua mwanamke kwa sababu ni mwanamke, kwa hiyo tunajaribu kuondokana na hilo na Marais wetu wa Afrika wenyewe wamekwenda hatua mbele. Katika kikao cha Juni, mimi ndio nilikuwa Mwenyekiti wa kikao cha Marais hao, waliozungumza wakatumia neno *equality* (usawa), wakasema kama *Commission ya Africa Union ina Commissioners* kumi, watano wanawake na watano wanaume, shida iko wapi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge akinamama wanangoja kuwapigia vigelegele, wanangoja kuwapigia kura, hili mlipitishe bila kigugumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache katika hoja hii ya mabadiliko ya Katiba. Naomba kwanza nianze kwa kutoa pole kwa wenzetu wa Kasulu Mashariki kwa kumpoteza mpendwa wao na ndugu yao Mheshimiwa Mussati aliyepoteza maisha bila shaka katika

harakati za kuhangaikia Watanzania wenzake kwa sababu Morogoro bila shaka alikuwa katika harakati za kufuatilia masuala muhimu ya Jimbo lake. Vile vile natoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Ntagazwa kwa kumpoteza mwenzake ambaye walizoeana naye. Mungu awapumzishe wote na awape amani huko walikotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawatakia pia kila la kheri Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka huu 2005 na hata nikiwatakia kila lililo jema katika harakati za uchaguzi zinazokuja ambapo sasa hapa tunaelekea katika tamati ya Bunge letu la miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda kuchangia katika hoja mbili tu. Hoja ya kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wote alioshauriana nao katika kuliona suala zima la kufikisha sasa asilimia thelathini kwa nafasi za wanawake katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake kufikia asilimia thelathini katika Bunge hili hakika si jambo la upendeleo kama ambavyo wengine pengine wanapenda lionekane, ni suala ambalo ni haki yao. Akinamama ni katika mengi ambayo wamekuwa wanashiriki katika Taifa ndani ya uzalishaji na uchangiaji uchumi na mambo mbalimbali. Kwa msingi huo basi ni historia tu inaonyesha kwamba akinamama pengine uwezo wao ulikuwa katika yale machache ambayo walishirikishwa lakini mwanamke anayeandaliwa sawasawa akipewa madaraka hata akitakiwa kuwakilisha wenzake hata kusimamia utekelezaji uwezo huo kwa hao wachache ambao wameweza kutangulia umeonekana wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo hili mimi nalipongeza na nasema kwa kweli asilimia thelathini ni mwanzo mzuri au hatua nzuri ambayo tumefikia lakini ikiendelea au ikiwa zaidi ya hapo bado hakuna jambo lolote ambalo litakuwa limeharibika. *(Makofi)*

Naomba pia kutoa changamoto kwa Vyama vya Siasa kwamba asilimia thelathini itatokana na Katiba kwamba isipungue asilimia thelathini ya wanawake katika Bunge, lakini vile vile ningeshauri sana kwamba katika kila chombo chochote kinachojitokeza kuwa na zaidi ya mtu mmoja. Kama ni watu wawili basi mmoja awe mwanaume na mwingine awe mwanamke na kama ni uteuzi kama nafasi ambazo tunazipendekeza Mheshimiwa Rais abaki nazo kumi hakuna ubaya wowote kwamba Rais ateue nafasi tano wanawake na tano wanaume kwa sababu mapendekezo mengi au niliyoyasikia yanasema kwamba Rais aachiwe nafasi. Mimi nakubali lakini mbona sasa hivi katika nafasi kumi wapo wanawake wawili tu. Mbona *thirty percent* haikufikiwa. Ni utaratibu tu tunaojiwekewa, tunafahamu kwamba hakuna malaika lakini ni utaratibu tunaojiwekea ili tuweze kuuheshimu kwamba Rais naye atakapokuwa anateua azingatie kwamba asilimia hamsini na mbili ya Watanzania ni wanawake basi asilimia hamsini ya Wabunge kumi iwe ni wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kwenye Vyama vya Siasa zipo nafasi pia za kugombea za Majimbo. Historia na ukweli unaonyesha kwamba wanawake waliosimama mwaka 1995, nitatolea mfano Chama cha Mapinduzi, walikuwa wanawake

saba waliopata uteuzi ndani ya Chama cha Mapinduzi kwenda kugombea Majimboni. Wote waliweza kuchaguliwa na kuingia Bungeni. Mwaka 2000 Chama cha Mapinduzi kiliteua wanawake kumi na nne. Bahati mbaya mmoja akapoteza maisha, mmoja akapoteza Jimbo kwa maana hakuchaguliwa. Lakini ukimwondoa yule ambaye hakuchaguliwa ambaye alifariki kabla ya kupigiwa kura wanawake kumi na mbili waliobaki waliweza kushinda kwa kuchaguliwa na kuingia Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ukizingatia kwamba hata wale walioteuliwa kumi na mbili si wote waliokuwa wamepata nafasi ya kwanza kwa kura za maoni. Wengine walipata nafasi za pili na wengine nafasi za tatu hata wengine zaidi ya hapo, lakini walipopewa nafasi kule walikubalika. Kwa msingi huo basi kama Vyama vya Siasa vitakuwa na makusudi mazima ya kuwatetea wanawake na kuwapa nafasi ya kuwapeleka mbele ya wananchi nina imani kabisa kwamba wanawake wanaweza kuchaguliwa kuingia ndani ya Bunge kwa kura za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba wanawake kwa wanawake wanapigana vita na wala si kweli wanawake hawapati kura, hapana. Hili jambo linakuzwa tu lakini linapokuwa limenyimwa nguvu linaendelea kupewa nafasi. Wananchi wapo tayari kutoa kura zao kwa wanawake wanaopelekwa mbele yao na hasa wanawake wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, mimi nashauri sana Vyama visaidie kuona kwamba wanawake watokee kila maeneo wale watakaotokea katika upande wa Majimbo wapewe msukumo, watakaokuwa wametokea katika viti maalum vile vile wapewe nafasi yao na hata katika *PR* na kwenyewe vile vile wanawake wapewe nafasi yao. Sasa basi niombe Vyama kuweka utaratibu mzuri wa nafasi ambazo zinatoka kikatiba ili kuhakikisha kwamba wanawake wanapopata nafasi kusiwe na manung’uniko ya namna yoyote kati ya wao kwa wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo lilikuwa la kwanza nililotaka kulichangia la nafasi za wanawake katika Bunge na kuomba kwamba ni haki ya akinamama na ni haki ya Watanzania hawa wa kike ambao wametubebea Taifa hili kwa mambo mengi na sasa tukiwapa uongozi hakuna tatizo lolote. Hata Rais asijisikie vibaya kwamba tunampangia, hatumpangii bali tunamkumbusha tu kwamba tupo na uwezo tunao, sababu tunayo na nia tunayo na tuko tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninalopenda kulisema ni kwamba, ninaipongeza sana Serikali kwa suala hili la kuona umuhimu wa kuweka mabadiliko kuhakikisha kwamba Waziri Mkuu sasa anaweza kukaimu Urais badala ya Mheshimiwa Spika ama Jaji Mkuu. Ni kweli kwamba wakati mnapofanya jambo lolote la mabadiliko kunakuwa na sababu lakini jinsi muda unavyokwenda kweli sababu nyingine zinakosa nguvu. Kwa umuhimu wa nafasi ya Rais ambaye anachaguliwa pamoja na Makamu wake msingi mkubwa ni Chama chao, wanatoka Chama gani. Kwa hiyo tuna imani kabisa kwamba Rais yule anayechaguliwa naye atampendekeza Waziri Mkuu ambaye ni mwaminifu na kutoka ndani ya Chama chake.

Mheshimiwa Spika, si lazima tena kwa heshima zote kabisa kabisa kwamba pengine Rais wa nchi ya Zanzibar awe anatokana na Chama kile kile ama Rais wa

Jamhuri awe anatokana na Chama kile kile inawezekana hapa kukawa na tofauti. Kwa hiyo, inaweza kusaidia sana Rais akikaimiwa na msaidizi wake ambaye ni Waziri Mkuu kuliko tukiliweka suala la kwamba ama akaimiwe na Spika au Jaji Mkuu au Rais wa Zanzibar. Mimi nadhani ni kwa msingi huo wa kuweka jambo hili likakaa vizuri kwamba watu walio katika mkondo mmoja basi washirikiane kufanya kazi za aina moja na kama ilivyo kukaimu hakumaanishi kuwa ni kuchukua madaraka yote ya Rais, hakumaanishi *total delegation of powers of the President to the Prime Minister,* lazima tu anakuwa na madaraka kiasi aliyoachiwa ambayo yana mipaka yake na akiyavuka yale ni *ultra violence* ambayo anatakiwa na mwenyewe awe anayo haki ya kuyapeleka mbele ya wenzake wakasema hiki ni kinyume cha utaratibu. Kwa hiyo, naye anafahamu lakini inapokuwa watu walio katika mikondo tofauti au walio katika madaraka yanayotaka kufanana, mimi nafikiri linaweza kuwepo tatizo. Kwa hiyo, mimi napongeza sana, nami naungana na wenzangu wote ambao wanaunga mkono suala la Waziri Mkuu kuwa anakaimu nafasi ya Rais wakati anapokuwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema kwamba nitachangia mambo mawili na kwa kweli ni hayo tu ambayo ningependa nichangie kwa sababu mengi yameshachangiwa na wote waliotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudisha shukrani zangu kwako na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ambayo sikuwa nimeitegemea. Nilikuwa na ukosefu wa nidhamu, sikuwa nimeomba lakini naona busara yako imetumika kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia mambo matatu tu ambayo mimi binafsi nafikiri ni muhimu. Nianze na la kwanza la Tume ya Uchaguzi *(Electoral Commission). Electoral Commission* kama ilivyoandikwa katika mabadiliko yetu kweli kabisa tunaitafutia nchi hii matatizo makubwa ambayo sisi wote tutayajutia. Uchaguzi huu mdogo uliofanyika ambao utaratibu wake kidogo haukuwa na mipaka ya kueleweka, taabu iliyotokea pale tusingependa itokee tena. Leo unachukua Vyama ambavyo vina tabia ya kila mtu kujiona mimi, mimi, mimi, unaviweka katika Tume ya Uchaguzi, ni kwamba nchi hii haitakuwa imefika mahali tunatamka kwamba leo tuna Rais ama kuna Wabunge. Kutakuwa na malumbano ambayo tutashindwa na kwa tabia ile ni kwamba mtu atatoka nje ya Tume pengine na kusema uwongo kwamba nilivyofika kule nimekuta kura wameiba, nami nimeziona na watu wakaamini hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walio wengi ambao hawapo mle ndani ya Tume watamwamini yule aliyekwenda hata kama anasema uwongo, kwa hiyo itafika mahali nchi hii haitatawalika. Nami sioni sababu ya msingi hata moja ya kupeleka Vyama vya Siasa ndani ya Tume. Hizo sababu sijazipata. Sababu hizo hatujazipata. Tunachotakiwa tuna mfano wa Namibia, kuna wenzetu walikwenda kusimamia uchaguzi, kinachotakiwa Vyama hivi vinakaa peke yao na vinajadili majina aliyopendekeza Rais kwamba yateuliwe, yakishateuliwa, yanakuja Bungeni, Bungeni sio tu tunapitisha

inakuwa Tume ya sisi wote wala haina Chama chochote na inafanya kazi yake bila kujali nani ni Chama gani, ni yule aliyeshinda na kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa kwa ajili ya kusimamia uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata bahati ya kupata statement ambayo imeandikwa na *Commonwealth Secretariat* pale walipokwenda ku-*observe* uchaguzi wa Msumbiji. Mnajua jinsi ilivyochukua siku nyingi kuweza kukubaliana na matokeo. Tarehe 24 Desemba wamekaa pamoja tena wakafanya *review,* Chama cha *RENAMO* chini ya Rais wake Dlakama pamoja na Vyama vingine 24 vya Upinzani viliandika yafuatayo, wanasema naomba nisome kwa Kiingereza maana yake ndio ilivyoandikwa humu: *"They would call for the dissolution of the Electoral Commission because of alleged partsanship and press for an Independent Electoral Commission to be constituted with no representation of Political Parties.* Haya yanazungumzwa na Chama cha *RENAMO* ambacho mnajua msituni kimekaa, kupigana wamepigana, mpaka juzi tu mara ya pili wamefanya uchaguzi wanasema kusiwe na *representation* ya Vyama ndani ya *Electoral Commission.* Wenzetu wamepigana na wanajua vile ni Chama cha *RENAMO* pamoja na Vyama vingine 24 vya Upinzani, ndivyo vilivyosema maneno haya. Leo Tanzania mlango wa pili tunasema tuingize Vyama ndani ya *Electoral Commission! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari ambayo inaonekana kabisa lakini sisi tuna-*entertain,* tunachotafuta si Vyama ndani ya *Electoral Commission ni Independent Electoral Commission,* hicho ndicho tunachotafuta. Sasa *Independent Electoral Commission* haiwezi kupatikana kwa kupeleka Vyama kule, maana Vyama vya kwetu vina ubinafsi tu, hakutakuwa na uchaguzi. Tutacheleweshа tamko la Tume kwamba kuna mshindi wa Urais na Wabunge watachelewesha na ukishachelewesha nchi haitakuwa na kiongozi kwa muda mrefu kwa sababu tu tuna Tume ya muundo huu, amani haitakuwepo. Si hivyo tu tutasababisha hali ya kutokuelewana ndani ya nchi na kutakuwa na makundi makubwa makubwa. Kwa kweli hiki ni kifungu cha hatari kabisa na mimi nafikiri kuna watu wanakusudia au tunakusudia kukifanyia marekebisho hiki kifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hii ni hatari. Hata yale waliyokubaliana katika muafaka Zanzibar basi tu ilikuwa ni hali ya hatari kwa hiyo waondoke katika matatizo yaliyokuwepo, lakini nayo pia itawashinda, haitachukua muda, lazima watashindwa. Hiyo si kweli wala sio halali wala haitawezekana, tutafute namna ya kupata *Independent Electoral Commission* na njia nyingine ya kupata hiyo ni kuleta majina ya hao watu hapa Bungeni na tukayapitia. Namibia wamefanya hivyo na inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoka hapo mimi naomba nipongeze suala moja la Mahakama. Kwa kweli tulikuwa tunaita Idara ya Mahakama haikuwa sahihi kwa sababu huwezikuwa na *pillar* mojaukaiita Idara ndani ya *Executive.* Hii nayo ilikuwa abnormal kabisa nilikuwa nimechukua hii Katiba nikawa nazungumza na watu wengine wakasema *is that right* ndivyo ilivyokuwa kwamba ninyi Mahakama nzima mnasema ni *pillar* mojawapo ya Serikali kinakuwa kitengo cha Idara nyingine ya *Executive!* Kwa hiyo, hili nadhani ni badiliko zuri na tunapenda kulipongeza kwa kweli ni badiliko zuri

hasa kwa sababu sasa wale wanaweza kufanya kazi yao hata lawama zote ziwapate wao wenyewe kwa sababu watakuwa hawakutumia utaratibu wao lakini tumewapa nafasi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ninalopenda kuzungumza tunaomba wenzetu Waheshimiwa Wabunge kaka zetu mtuvumilie. Yamezungumzwa mengi hapa kuhusu nafasi za Viti Maalum na wengine wakasema isiwekwe kwenye Katiba. Jamani taarifa tuliyonayo, katika nchi inayopigiwa mfano kwamba ni nchi pekee katika *Affirmative action,* hivi Viti Maalum wanaita *affirmative action* ambao wameweka kwa uhakika kwamba wanawake watakuwepo Bungeni ni Tanzania. Tulikuwa tunatolewa mfano kwa Katiba hii tunayofuta kwamba ni nchi peke yake tumeiweka kwenye Katiba ya nchi. Wengine ilikuwa ni Vyama vya Siasa tu. Kwa mfano hata *South Africa* wale wanawake wengi wanaoingia katika Bunge la *South Africa* ni wa Chama cha *ANC* kwa sababu *ANC* ndio yenye utaratibu na mpango wa kutambua akinamama kwamba walitoa mchango sahihi wakati wa vita. Kwa hiyo hata *ANC* sasa hivi wana-argue kwamba wangeweka kwenye Katiba, sasa tatizo lao ni kwamba Vyama vingine havijaridhia hilo lakini wanatafuta njia ya kuingiza humo. Kwa hiyo naomba sana msijione wanyonge na kusema kwamba mmekosea kuweka katika Katiba ya nchi, hapana mmefanya vizuri sana kwa sababu aje nani au nani hilo lipo ndani ya Katiba, mkitaka kubadili *two third* lazima ipatikane sasa hiyo siyo kazi rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninachosema tunatakiwa kuomba asilimia hamsini. Ukweli ni kwamba tulitakiwa tuombe katika mabadiliko iwe asilimia hamsini kwa hamsini. Sasa tumeyaona haya mnayosema ninyi kwamba hivi viti sio vya kudumu, hivi viti ni mahali kama pa kujifunzia namna ya kwenda huko kwenye Majimbo, hatuombi hamsini kwa sababu tunatakiwa tutafute viti vya Majimbo pia. Kwa hiyo, lengo letu sisi ilikuwa pamoja na hivi tupate viti vingine vingi vya Majimbo. Sasa kuna kaka zetu wengine hapa kidogo wanalalamika, jamani ikifika tarehe ya uchaguzi, Bunge likivunjwa hapa, kila kiti kitakuwa na zaidi ya watu kumi. Hata cha kwangu kile kitakuwa na watu zaidi ya kumi wanaume kwa wanawake kama watakuwepo wanakaribishwa. Kwa hiyo naomba sana ndugu zangu Wabunge mjue hata kama si huyu mnayemjua leo, lakini wapo wengine watakuja. Kwa hiyo kikubwa kama unakitaka kiti chako kitetee kwa nguvu zako zote, kama ilivyowahi kutokea kwangu. Kwa hiyo naomba sana. Mtukubalie mapendekezo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwakumbushe historia. Mwaka 1965 historia inatwambia kulikuwa na wanawake Wabunge wa Majimbo saba, miaka ya 80 walitoka saba akaja mmoja, mwaka mwingine akawa mmoja Mheshimiwa Shamim Khan, huo mwaka wa Shamim Khan walituzidi wenzetu wa Zanzibar akinamama walikuwa sita. Lakini akinamama wa Zanzibar waliokuwa sita mwaka uliofuata wote hawakuwemo humu ndani. Sasa mwaka 1995 tulikuwa nane pamoja na mwenzetu wa Upinzani wa *CUF* mama Maghimbi. Mwaka 2000 ndio tukawa kumi na mbili. Mimi nina wasiwasi mwaka 2005 kama hatutegemei viti maalum tunaweza kurudi watatu au wangapi. Kwa hiyo mtuelewe tatizo tulilonalo, si kwamba watu wanaogopa kwenda huko watakwenda na tuna mkutano karibuni wa kuwaandaa wanawake waende huko Majimboni, lakini mapambano si rahisi. Wanasema ile *level play ground* ya kuchezea haipo sawa,

kwingine ipo chini chini na kwingine imeinuka, hakuko sawa. Kwa hiyo tuacheni tu tugombee humu ndani tuwe na uhakika wa angalau asilimia thelathini, halafu ndio tukajaribu huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakwenda kujaribu wala wasiwe na mashaka, lakini hakuna uhakika. Tukipata basi tutashukuru, lakini lengo letu ni kwamba tukiweza kupata wengi wale watakaokuwa na Majimbo baada ya miaka mingine ijayo kwa kweli hakuna sababu ya viti hivi, maana watu watakuwa wamezoeleka na ndio lengo letu kwamba kila anayepita huku afanye kazi nzuri ili watu waelewe kwamba kwa kweli akinamama sio wadhaifu kiasi hicho. Kwa hiyo, tunaomba sana wasiwe na wasiwasi, hivi vitu ni vya lazima, tungeweza kuomba asilimia hamsini na wala msingeweza kukataa ni haki yetu tu. Lakini tukasema hapana tuombe thelathini, vingine tukajaribu ndio tunachoomba hapa. Naomba kwa kweli isiwe issue wala msitwambie tupeleke kwenye sheria tu ya uchaguzi, hapana, ikae humu humu kwenye Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tunaomba tutakapofanya mabadiliko ya Sheria ya Uchaguzi vile viti vya Madiwani na vyenyewe itabidi tufanyie mabadiliko kidogo vifike kama asilimia arobaini, halafu vingine watatafuta wenyewe. Kwa hiyo, hilo naomba tu mlikumbuke. Ila kwa hakika hili suala la Tume ya Uchaguzi tunaomba hiyo mtuelewe tunaleta mabadiliko kusudi tuhakikishe kwamba hatuwi na hii vita tunayoitengeneza sisi wenyewe maana Bunge hapa itakuwa imetengeneza vita. Kwa hiyo, lazima tufanye marekebisho katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hoja iliyopo kuhusu Marekebisho ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nitoe pole kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Marehemu Frank Mussati na pia natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao wamepatwa na misiba na matatizo mengine ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo natangulia kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote. Ningependa mchango wangu niuelekeze mahsusi kwenye eneo la Viti Maalum. Viti hivi vimeendelea kufahamika kama viti vya upendeleo, lakini mimi ningeshawishi kwamba viwe ni viti maalum kwa sababu kwa kweli tukianza kuzungumzia suala la upendeleo ni kama tunazungumzia kitu ambacho si haki au si sahihi. *(Makofi)*

Napenda kusema hivyo kwa sababu viti hivi vililetwa au viliwekwa maalum kwa ajili ya kurekebisha upungufu wa kihistoria ambao tayari Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameshauzungumzia upungufu huo, nisingependa kuurejea. Lakini cha msingi ambacho ningependa kukisema ni kwamba uamuzi wa kuwa na viti maalum ulikuwa ni uamuzi sahihi sana. Huu ni uamuzi ambao ulikuwepo tangu tulipokuwa na

demokrasia ya Chama kimoja na Waheshimiwa Wabunge natumaini watakumbuka vizuri kwamba wakati ule tulikuwa na viti maalum vya aina nyingi. Kulikuwa na viti vya wanawake, viti vilivyotokana na Jumuiya ya Wazazi na viti vilivyotokana na Jumuiya ya Vijana. Lakini baada ya mfumo wa Vyama Vingi ilionekana kwamba kuna upenyo wa makundi hayo mengine kuweza kuwakilishwa vizuri katika mfumo mpana wa Vyama Vingi isipokuwa kama nilivyosema kwa sababu za kihistoria ilionekana kwamba ni muhimu kuwepo na viti maalum vya wanawake na viendelee kuwepo. Kwa hiyo, Waziri wa Katiba anapokaribia kuhitimisha hoja yake, nadhani tuna kila sababu ya kujivunia kwamba kwa kauli moja Waheshimiwa Wabunge katika Bunge lako Tukufu wanaunga mkono suala la viti hivi kuongezeka hadi kufikia angalau asilimia thelathini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami ningependa kuongeza sauti yangu katika mapendekezo haya na kuyaunga mkono kwa misingi mizuri kadhaa. Sitaweza kuitaja yote, lakini kwanza linalonipa nguvu ya kuunga mkono hoja hii ni Katiba yetu wenyewe ambayo ilipitishwa katika Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge hata kabla ya harakati hizi tunazozizungumzia leo kupamba moto. Katiba yetu inatambua usawa wa wananchi wake wote bila kujali tofauti za rangi dini au jinsia. Kwa upande wa jinsia kama nilivyosema ndipo Serikali iliona umuhimu wa kuweka utaratibu huu wa viti maalum, utaratibu ambao Waheshimiwa Wabunge waliunga mkono wakati ule na leo hii wanaunga mkono.Kama ambavyo ametangulia kusema Mheshimiwa Makinda, Bunge letu hili ni Bunge la Kimapinduzi sana. Ni Bunge ambalo limeweka historia sio tu katika eneo la *SADC* lakini katika Bara la Afrika.

Hakuna nchi nyingine ambayo imeweka utaratibu huu katika Katiba. Bahati nzuri katika mjadala hapa ndani ya Bunge lako Tukufu tumeonyeshwa na tumeelezwa umuhimu na uzito wa Katiba. Katiba ni sheria mama na ni sheria ambayo sio rahisi kuichezea. Kwa hivyo tunavyoomba na kusisitiza kwamba viti hivi viendelee kubakia ndani ya Katiba ni kwa kutambua kwamba viti hivi vitakuwa salama zaidi ndani ya Katiba kuliko nje ya Katiba. Kwa kweli msingi uliowekwa wa kuweka uwakilishi huu ndani ya Katiba ndio msingi ulioiwezesha nchi yetu kuendeleza utaratibu huo katika ngazi ya Halmashauri na Manispaa na vile vile katika ngazi za Mabaraza ya Ardhi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana alipokuwa akichangia Mheshimiwa Dr. Mzindakaya alisema na leo imerejewa pia na Mheshimiwa Makinda kwamba mwaka wa 1965 tulikuwa na Wanawake saba waliotokana na Majimbo. Lakini leo hii tuna Wanawake kumi na mbili tu waliotokana na Majimbo. Ni suala la kujiuliza hivi kweli tumepiga hatua ya kutosha toka mwaka 1965 hadi hivi leo kuwa na Wabunge kumi na mbili tu katika Majimbo ni jambo ambalo kwa kweli tunapaswa kuliangalia upya. Lakini pamoja na hayo nchi yetu pia imeridhia Mkataba wa Kimataifa wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya Wanawake. Kwa kweli Bunge lako Tukufu ndilo lililopitisha Azimio la kuwezesha nchi yetu kuridhia Mkataba huu. Sasa Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuchukua hatua mahsusi za kuhakikisha kwamba kunakuwa na kiwango fulani cha uwakilishi katika ngazi za maamuzi sio Bungeni tu peke yake lakini katika ngazi za maamuzi na ngazi nyingine za uongozi. Kwa hivyo sisi Tanzania kama

nilivyosema hapo awali kwa kweli ni watu ambao tumeonyesha njia kwa kuitikia wito huu lakini pia kwa kuweka viti hivi ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Hali kadhalika lipo Azimio la Wakuu wa Nchi za *SADC* la mwaka 1997. Hili ni Azimio ambalo limeridhiwa na viongozi wetu wa nchi za *SADC* Tanzania ikiwa mojawapo na ndio Azimio lililozitaka nchi wanachama kufikia kiwango hiki cha angalau asilimia 30 ya uwakilishi wa Wanawake katika ngazi za maamuzi na ngazi za uongozi. Kwa hivyo tunapokaribia hoja hii kuhitimishwa nadhani bado Bunge lako Tukufu litaweka tena historia kwa kutimiza lengo hilo kabla ya mwisho wa mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kipengele hiki vile vile kwa kuzingatia pia kwamba nchi yetu imekuwa na mchango wa pekee katika mchakato wa kuanzisha Umoja wa Afrika. Katika michango ambayo imetolewa na Tanzania mmojawapo ni wa kusisitiza kuwepo na uwakilishi wa kutosha. Hivi sasa nchi za Umoja wa Afrika zimeweka msingi wa uwiano kuwa ni asilimia 50. Tayari hili limefanyika kwenye Kamisheni ya Umoja wa Afrika na linaendelea kuzingatiwa katika ngazi nyingine. Kwa hiyo ni imani yetu kwamba tunaporidhia mapendekezo yaliyoletwa hapa tunajijengea pia njia nzuri kuelekea kwenye uwakilishi wa juu zaidi wa Wanawake sio tu kwenye Bunge kama nilivyokwishasema bali kwenye maeneo mengine ya utendaji na maeneo ya uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo wengine wamesema imeelezwa hapa kwamba wako wachache waliokuwa na wasiwasi kwamba kuwekwa kwa nafasi hizi kutatufanya Wanawake kubweteka au kutegemea viti hivi zaidi badala ya maeneo mengine. Kwa kweli kwa asili na historia na hata mantiki ya viti hivi haiwezekani viti hivi vikawa vya kudumu. Kwa kweli nia ni kujenga mazingira mpaka hapo tutakapofikia mahali ambapo tayari jamii zetu zitakuwa zimekubali kwamba Wanawake wanaweza. Kwa hiyo hizi ni hatua za muda tu na lengo lake ni kuondoa mapengo ya kihistoria. Ni vyema nafasi hizi zikaendelea kuwepo na inatia moyo kwamba Bunge lako Tukufu linakubali kwamba ziendelee kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunavyosema hivyo tukumbuke kwamba kuendelea kuwepo kwa nafasi hizi au umri wa kuwepo kwa nafasi hizi kutategemea vile vile kasi ya mabadiliko ndani ya jamii zetu. Jamii zitakapokuwa tayari na jamii ni Wanawake na Wanaume zitakapokuwa tayari basi suala hili la nafasi maalum nadhani litatoweka lenyewe.

Hivi sasa suala la usawa au uwiano wa kijinsia sio suala jepesi tu ni suala pia ambalo linatumika kama nyenzo muhimu sana ya maendeleo. Hapa ningependa kumnukuu kwa ujumla tu Mheshimiwa Rais Mkapa ambapo alikuwa anahutubia kikao cha Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika huko Durban mwaka 2002. Kama nilivyosema hapo awali nchi yetu imetoa mchango mkubwa sana katika eneo hili la maendeleo ya Wanawake na usawa wa kijinsia. Mheshimiwa Rais Mkapa wakati ule alipewa fursa kutoa mada inayohusu *Gender Main Streaming.* Ni nafasi ya pekee na sisi Wanawake

wa Tanzania nadhani Watanzania kwa ujumla tuliona fahari sana kwamba Kiongozi wa juu wa Taifa letu ameweza kuzungumzia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais Mkapa alibainisha wazi kwamba suala la usawa wa kijinsia ni suala la maendeleo. Ni suala la kukidhi sawa na hilo ni muhimu, lakini pamoja na lengo hili usawa wa kijinsia una uwiano wa karibu sana na kasi ya kuongezeka kwa maendeleo na kukuza uchumi wa Taifa letu. Kwa sababu unapokuwepo usawa wa kijinsia na kunavyokuwepo fursa sawa za ushiriki katika masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na uongozi basi tunaona kwamba kuna mtiririko wa moja kwa moja kati ya ushiriki wao na ukuaji wa uchumi ukuaji wa raslimali na hali kadhalika matumizi na mgawanyo wa raslimali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapochukua hatua kama hizi za kuongeza ushiriki wa Wanawake kama ambavyo tunategemea kufanya kwa kuyapitisha mabadiliko haya tutakuwa pia tunaharakisha mchakato wa maendeleo na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Cha msingi baada ya kuchukua hatua hizi kama vile kuongeza nafasi za uwakilishi katika Bunge, Mabaraza au Kamati ni kujenga mazingira ambayo yatatufanya tuondokane na nafasi maalum badala yake ushiriki sawa wa Wanawake na Wanaume uwe ni jambo lililojengeka ndani ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapofikia hatua hiyo tutakuwa tunazungumzia mambo mengine hatutakuwa tunajadili tena kama tuwe navyo au tusiwe navyo, viwekwe ndani ya Katiba au nje ya Katiba.

Kati ya mambo ambayo Serikali inayafanya ambayo yatatusaidia sana kuhakikisha kwamba mazingira hayo yanajengwa ni kuimarisha kwa mfano utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii, kama vile utoaji wa elimu kupitia mpango ambao wengi tunaufahamu mpango wa MMEM na MMES, kuimarisha huduma za afya hususan kwa mama na mtoto na mipango mingine ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaifahamu vizuri. Kwani mwanamke anapokuwa amepata elimu, na mwanamke anapokuwa na afya na anapokuwa na makazi mazuri anakuwa na utulivu, amani na anakuwa na nafasi nzuri sana ya kuchangia maendeleo ya nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo napenda kumalizia kwa kusema kwamba haya tunayoyafanya Waheshimiwa Wabunge ni mstari sahihi. Bunge letu ndilo limeshika kibendera na watu wanatoka nchi nyingine kuja kujifunza sisi tulifanyafanyaje, tuliwezaje kuingiza suala hili ndani ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nyimbo alipokuwa akichangia jana alisema kwamba wakati mwingine si vyema kujilinganisha sana na nchi za nje. Ni kweli lakini hivi sasa Tanzania ni nchi ambayo hata Wamerikani wanakuja hapa, Waingereza wanakuja hapa kuangalia ni namna gani uwakilishi wetu umo katika vyombo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa hoja ya Muswada huu kila aliyeomba na kuwa Bungeni amepata nafasi. Mtaona hawa watatu wa mwisho waliomalizia wameleta sasa hivi maombi lakini bado walipata nafasi. *(Makofi)*

Sasa kabla sijaahirisha Shughuli za Bunge ningependa tu kuwakumbusha nadhani mlipatapata zile barua za mwaliko leo jioni pale *Dodoma Hotel*. Sasa sina uhakika kama wote tulipata maana mimi nilipata na baadhi ya wengi nimewauliza walipata kuna mwaliko wa *Dodoma Hotel* kwamba watu wa *CRDB* wametualika na Mheshimiwa Spika atakuwa mgeni rasmi pale. Kwa hiyo, kwa wale ambao tumealikwa na nadhani ni wote tumealikwa twende tukamuunge mkono Spika wetu ambaye atakuwa mgeni rasmi.

Bado sijamaliza kusema yote haya yamo katika kusema. Kwa hiyo saa 2.00 usiku leo wote tunatakiwa tushiriki nao pale. Sasa baada ya tangazo hilo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.42 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu*
*Tarehe 7 Februari, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*